Kikao cha Nane – Tarehe 24 Febuari, 2017

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Ustawi wa Jamii: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2016/2017. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 112

Uchakavu wa Jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini – Pemba

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba liko katika hali mbaya na linahatarisha usalama wa wafanyakazi na watumiaji wa jengo hilo.

Je, ni lini Serikali italifanyia matengenezo jengo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 112 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la msingi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua ikichukua hatua mbali mbali za kuhakikisha kwamba, taasisi za Serikali ikiwemo Idara ya Mahkama inakuwa na mapengo ya kisasa ili kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeyafanyia ukarabati mkubwa baadhi ya majengo ya Mahkama Unguja na Pemba. Miongoni mwa majengo hayo, ni pamoja na Jengo la Mahkama Kuu Pemba lililopo Chake Chake mkoa wa Kusini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italifanyia matengenezo jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kadri hali ya Uchumi itakavyo ruhusu. Tayari Wizara imeshaanza mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuona uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahkama hiyo katika mwaka wa fedha ujao iwapo hali itaruhusu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa umeahidi kwamba serikali ina mpango wa kufanya matengenezo makubwa jengo hili pale hali itakaporuhusi.

(a) Je, unajua matengenezo makubwa kama haya yanafanywa lakini ni muda mchache ambao kuwa tayari jengo lile linapoteza haiba yake ya matengenezo kama haya. Je, ni sababu zipi zilizofanya Mahakama ya Mkoa ya Ardhi vile vile nayo iko katika hali mbaya. Je, ni sababu zipi za msingi zilizofanya hii ambayo imehamiwa kwa karibuni na sasa hivi iko hali mbaya Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini ya Ardhi. Ahsante sana

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba huo wakati ambao utakaofanya matengenezo ya Mahakama hiyo na nyenginezo ambazo nyengine sasa hivi ziko mbioni katika mategenezo hayo. Nimuhakikishie kwamba tutakuwa na wakandarasi ambao wenye kufanya kazi nzuri wenye kujenga Mahakama zetu katika kiwango kikubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakilishi asijali kwa hilo tutakikisha kwamba Mahakama zetu zote tunazijenga kama tulivyozijenga hizo nyengine tutazijenga katika kiwango kizuri na ziweze kudumu kwa muda mrefu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Nam. 84

Kutokidhi malengo ya Vyombo vya Habari vya Umma:

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:-**

Zanzibar ni moja ya nchi katika bara la Afrika iliyoona umuhimu wa kuanzisha vyombo vya habari ikiwemo TV na Radio ili wananchi wafaidike kupata habari za uhakika na kuona maendeleo yanayofanywa na Serikali. Lakini dhana hiyo inaonekana kuondoka kwani pamoja na vyombo hivyo kuanzishwa kwa muda mrefu sana, bado havijakidhi malengo na inaonekana ndio vyombo vya mwisho katika kutoa huduma hii.

a) Je, ni sababu gani zilizopelekea vyombo hivyo kushindwa kwenda na wakati na ile dhana iliyokusudiwa kutofikia lengo.

b) Je, vyombo hivi viliwezaje hapo zamani kuonekana Unguja na Pemba na sehemu nyingine za Tanzania bara kwa ufanisi hata leo hii inashindikana.

c) Je, Serikali haioni umuhimu kufanya juhudi za makusudi kuviwezesha vyombo vya habari vya Umma kuingia katika ushindani wa sekta hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu **:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari 84 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Sababu ziizopelekea vyombo vyetu kuonekana viko nyuma katika dhana iliyokusudiwa kufikia lengo kwa wakati wa sasa ni kwamba vyombo, studio, mitambo yetu ni vya muda mrefu ambapo kwa asilimia kubwa haviendani na mabadiliko ya teknologia iliyopo sasa *Digital*.

b) Hapo zamani vyombo viliweza kufikia malengo kwa asilimia kubwa ya kuwapa habari za uhakika wananchi wake kutokana na mfumo wa Analogia ambao ulienda sambamba na uwezo na mitambo, zana na vyombo vilivyotumika Unguja na Pemba kuwapatia habari wananchi wake.

c) Serikali imeona umuhimu huo na tayari jitihada kubwa zimeshachukuliwa. Aidha shukrani za pekee tunampa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi Dkt Ali Mohamed Shein kwa kuona umuhimu huo mapema zaidi na kusimamia ipasavyo upatikanaji wa vyombo vipya, mitambo na vifaa vya kileo pamoja na kuweka mfumo wa studio mpya na mazingira yake kufanyika bora zaidi kwa kutengeneza majengo ya vyombo hivyo jambo ambalo linaendelea hivi sasa na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuhakikisha tutabadilika. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, chombo chetu hichi cha *ZBC* ambacho ndio chombo cha Taifa kwa taifa letu kwa upande wa Zanzibar tunakitegemea sana kwa kutoa habari za uhakika ambazo watu wengi mitando sasa hivi wanatuchafua.

(a) Je, kutokana na umuhimu wake ipo sheria ya kuwaambia au kuwalazimisha vyombo vyote ambavyo vinafanyakazi au vinatangaza katika nchi hii kwamba *TV* ya *ZBC* inaonekana bila ya usumbufu wowote na kama hapana ni hatua gani ambazo zinachukuliwa ili wananchi wafaidike na habari ambazo zinatoka *ZBC*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, katika Sekta ya Habari zipo sheria ambazo zinaongoza Vyombo hivi vya Habari.

(a) Vyombo hivi tutaendelea kuvihamasisha ili vifuate taratibu sahihi za kuonekana taarifa hizi ipasavyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Habari, Utalii, Uwezeshaji na Mambo mengineyo.

Lakini tulipotembelea katika wizara hii tuliwakuta vijana fulani wanaendesha vipindi mbali mbali ambao wanajitolea kwa muda mrefu kama karibu miaka kumi sasa hivi na katika taarifa hiyo tulipokea kwamba wenyewe wameridhika kutokana na mwenendo wao mpaka *ZBC TV* wameridhika nao.

(a) Je, hivi sasa kuna taarifa rasmi kwamba vijana wale wote wamesimamishwa kazi na huku nyuma tumepata taarifa kwamba ni vijana wazuri ambao wanaweza kufanya kazi zao kwa mihimili yoyote wanayotaka wenyewe Shirika la *ZBC TV*. Ni kitu gani kilichosababisha kuhamishwa vijana hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, *ZBC TV* hili ni shirika na shirika hili au mashirika yote yanaongozwa na Bodi.

(a) Ni kweli vijana wale walikuwepo pale na kama ipo taarifa ya kusimamishwa sasa hivi nimjibu kwamba huu ni uamuzi wa Bodi kwani uajiri wa vijana hawa Bodi nayo itoe uamuzi wake.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Mwenyekiti, Ikiwa wakati wa Bunge likiwa linaendelea kipindi cha maswali na majibu tumeona kwamba wakalimani wamekuwa wakionesha maswali na majibu kuashiria watu wenye ulemavu kupata habari zao wanazoulizwa majimboni. Lakini cha kushangaza *ZBC* haioneshi wakalimani wakati wa maswali na majibu katika Baraza la Wawakilishi.

(a) Je, kuna sababu gani za msingi ambazo zinazopelekea kuwa wakalimana hao washindwe kuonesha kipindi cha maswali na majibu kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, samahani naomba arudie swali lake.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba maelezo ambayo nimeanza kuyatoa tumekuwa tukiona Bunge linavyoendelea katika kipindi cha maswali na majibu. *TBC* imekuwa ikionesha wakalimani kuashiria kwamba kuwaona watu wenye ulemavu wanapata taarifa za majimboni mwao ambazo zinazouliza maswali na majibu.

Lakini cha kusangaza *ZBC* imekuwa haioneshi wakalimani wakati wa kipindi cha maswali na majibu.

(a) Je, kuna sababu gani za msingi ambazo zinazopelekea kuwa wakalimani hao kipindi cha Baraza la Wawakilishi kuwa haoneshi kipindi cha maswali na majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, suala ambalo ameliuliza Mhe. Zaina Abdalla Salum naomba nimjibu kwamba yeye ni shahidi tumo ndani ya Baraza na sisi tunawaona wakalimani wale wapo wanaonesha vipindi vile moja kwa moja kupitia Baraza hili tukufu.

Lakini pia wananchi wetu wote sasa hivi wapo wanaangalia Baraza hili na yupo mkalimani au wapo wakalimani wanaonesha moja kwa moja kipindi hichi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 37.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani umeomba kuhusu utaratibu lakini usubiri nikuruhusu. Haya Mhe. Abdalla Maulid Diwani endelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 37 Waziri au Mjumbe yoyote anaeuliza swali ambalo ana mamlaka nayo atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo.

Mheshimiwa muuliza swali la nyongeza Mhe. Zaina Abdalla Salum aliuliza kwa nini wakati wa maswali na majibu wale watu wanaoonesha lugha za ishara wakalimani wa lugha za alama wanakuwa hawapo kipindi kile. Asitwambie kuwa wanakaa baada.

Kwa nini wakati wa maswali na majibu wanakuwa hawapo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niombe samahani kwa kutolifahamu swali hili. Lakini naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kwa faida ya Wawakilishi wote lakini na jamii inayotuangalia pia kwamba suala hili tutalichukuwa na tutalifanyia kazi ili tuone kwamba wakati wa kipindi cha maswali na majibu wakalimani hawa wanakuwepo na wanaonekana katika maswali na majibu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Nam. 87

Ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Zanzibar inaitangaza lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha halisi ya Zanzibar na Kiswahili fasaha lakini maelezo hayo hayalingani kutokana na kutokipa kipaumbele lugha hiyo kipaumbele kama lugha ya taifa na kukithamini kama nchi nyengine zinavyodhamini lugha zao na kukiacha Kiswahili kuwa ni lugha ya mitaani na badala yake kuzipa kipaumbele lugha za wageni kama kiingereza n.k.

a) Je, ni kwanini katika vyombo vya Sheria au maeneo ya mikataba na maeneo mengine Kiswahili kinazidiwa na Kiingereza katika uandishi na mazungumzo.

b) Kwanini Serikali haijakipa nafasi Kiswahili kuwa lugha yake Kiswahili ndio lugha ya Taifa.

c) Kwanini viongozi wetu wanapokwenda nchi za nje katika mikutano ya kimataifa hawaoneshi kuwa wanatoka Zanzibar au Tanzania na kutumia lugha ya Kiswahili ili iwe ni moja ya utambulisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu **:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari **87** lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, ieleweke kuwa Sheria na Katiba zetu zilizopo Tanzania na Zanzibar zimeeleza kuwa Kiswahili na Kiengereza ni lugha rasmi. Hata hivyo, Katiba pendekezwa ya Tanzania imebainisha kwamba Kiswahili ni miongoni mwa tunu za Taifa la Tanzania. Baraza la Kiswahili la Zanzibar linaendelea kuhamasisha taasisi zote kuitumia lugha ya Kiswahili zaidi kuliko Kiengereza, na ndio maana taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimepelekewa barua na Baraza la Kiswahili kuzitaka zitumie Kiswahili katika mazingira na shughuli zote za kitaifa kama vile majina na matangazo yao. Halikadhalika, tutumie Kiswahili wakati wanapotoa huduma kwa jamii kwa njia ya kimazungumzo au kimaandishi.

b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeipa nafasi lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya Taifa kutokana na kuiundia lugha hiyo taasisi yake ya kusimamia maendeleo yake nje na ndani ya Zanzibar. Pia, taasisi hiyo hupatiwa bajeti yake ya kusimamia na kuhamasisha matumizi ya Kiswahili. Katika kusimamia hili Baraza hutoa taaluma kwa taasisi za Serikali na jamii kwa ujumla juu ya matumizi ya Kiswahili.

   Aidha taasisi nyingi zinazosimamia sheria tayari zimetafsiri sheria na vipeperushi vyao zilizokuwa zimeandikwa kwa Kiengereza kuwa katika lugha ya Kiswahili. Sheria hizo ni kama vile;

   - ❖ Kanuni za Utumishi wa Umma
   - ❖ Mwongozo wa utayarishaji mpango wa rasilimali watu katika Kanuni za Utumishi wa Umma
   - ❖ Fomu za Sheria ya maadili ya viongozi wa Umma
   - ❖ Mwongozo wa Mpango wa Uandaaji Viongozi katika Utumishi wa Umma n.k.
   - ❖ Katiba na Sheria ndogo ndogo zimeandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza.

   Halikadhalika, Kiswahili kinatumika katika hotuba mbali mbali za kitaifa, kisiasa na kijamii

c) Mhe. Mwenyekiti, Viongozi wetu wa kitaifa kwa sasa wanaonesha mfano bora wa kutumia lugha ya Kiswahili kila wanapokutana na viongozi wenzao wanaotoka nje au viongozi wa kigeni. Pia, wanapohudhuria mikutano ya kitaifa na kimataifa kama vile mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkutano wa Umoja wa Afrika. Halikadhalika, baadhi ya waheshimiwa mawaziri wetu wa Zanzibar wameanza kuchukua juhudi za kukitumia Kswahili katika mikutano yao ya kitaifa. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Bi Riziki Pembe aliwahi kutumia Kiswahili katika mkutano wake alipotembelewa na balozi mdogo wa Iran aliyepo Zanzibar. Pia, Wairani na Wasudan walipowatembelea viongozi wa Wizara ya Elimu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri walitumia Kiswahili ingawa walikuwa na mkalimani. Huu ni mfano hai wanaotuonesha viongozi wetu kuwa kutumia Kiswahili inawezekana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee zimuendelee Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa jitihada zake za makusudi za kuweza kukitangaza kiswahili.

(a) Mhe. Naibu Waziri mmehamasishaje kwamba viongozi wetu watakapokwenda nje ya nchi hata kama kiengereza anajua tukachukuwa mkalimani kwa mantiki ile waziri asizungumze lugha yoyote zaidi ya kiswahili na atafsiriwe. Mmechukuwa hatua gani kwa uhamasishaji.

(b) *ZBC* ndio chombo cha habari nataka kukuuliza Mheshimiwa watangazaji wako wana viwango gani vya lugha ya kiswahili, kiengereza na kiarabu fasaha na kama hawana je, umechukuwa hatua gani za kuwasomesha.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba hatua ambazo tumezichukuwa kwa viongozi wetu ambao wanakwenda katika mikutano ya kimataifa.

(a) Kama nilivyojibu katika swali mama kwamba sasa hivi viongozi wetu wamehamasika kutumia kiswahili na mfano mzuri hata Mhe. John Pombe Magufuli Rais wa Tanzania amekuwa akitumia kiswahili katika mikutano yake ya kimataifa.

Lakini kama hiyo haitoshi naomba nilichukuwe kwamba kwa ushauri wake ambao amesema tuchukuwe wakalimani hiyo tutaifanyia kazi na hatima yake tutaona matunda yake *in shaa Allah*.

(b) Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba elimu za vijana wetu wale kwa kuwa ametaka kujua kila idadi ya mfanyakazi wetu kwamba ana elimu gani kiswahili na kiengereza. Naomba hili nilifanyie kazi na hatika yake nimletee majibu rasmi. Ahsante.

Mhe. Panda Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa lugha ya kiswahili ni utajiri mkubwa katika Tanzania yetu na kwa kuwa hapa Zanzibar ndipo kinapopatikana kiswahili fasaha chenye lahaja mbali mbali ambazo lahaja hizo zinazidi kukipamba kiswahili chetu kuwa kizuri.

(a) Je, lini serikali itatumia utajiri huu kwa kukienzi kiswahili chetu kisiharibiwe kwa kubadilishwa maneno ambayo yanaondoa haiba katika kiswahili chetu.

(b) Kwa kuwa sisi ni walimu wazuri ambao tunaweza kufundisha vizuri kiswahili, je, ni lini serikali itafungua matawi katika nchi mbali mbali ambazo zinahitaji kujifunza kiswahili ili tuweze kuingiza tija katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba:

(a) Sasa hivi wizara imehamasika na inatoa elimu kwa jamii juu ya matumizi ya kiswahili kwa kuwa ni lugha yetu ya taifa na nahili naomba nimjibu kwamba ushahidi wa hili tumeunda mabaraza ya Kiswahili mwa mfano BAKIZA, lakini kwa upande wa Tanzania Bara kuna BAKITA ambazo taasisi hizi zimewekwa rasmi kwa ajili ya

kukitangaza kiswahili na kuona kwamba kuthamini pia kwamba ni lugha yetu ya taifa letu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali hili inalichukuwa na italifanyia kazi kufungua matawi katika nchi mbali mbali ili kutoa elimu hii na wale wageni wanaokuja hapa waone kwamba lugha hii ni lugha yetu ya taifa ili na wageni waweze kuitumia lugha hii. Lakini hata hivyo wapo walimu wetu kutoka Tanzania kwa mfano kama Uingereza wapo walimu wanatoka hapa na wengine samahani naomba nimtaje kwa jina kuna ndugu Yussuf anatokea Wingwi Mapofu huyu yuko Uingereza na anasomesha kiswahili.

Kwa hiyo, huu ni ushahidi kwamba tutakuwa na utaratibu maalum wa kufungua matawi haya na kuonekana kwamba lugha yetu inafanyakazi vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, kiswahili ni lugha ya taifa na kiswahili kila anaezaliwa kwa Unguja hii na Pemba anakijua bila ya kufundishwa ingawa kuna somo maalum la kufundishwa taratibu tu nyenginezo.

Kwa kuwa nchi za wenzetu hasa China na nchi nyenginezo wamepiga hatua kubwa sana kwa kutumia lugha yao ya taifa ile katika nchi yao na ufanisi wao kuanzia miaka 60 na kuendelea imeonekana kuwa ni pato la nchi, uwezo wa nchi umeongezeka kutokana na lugha yao ya taifa.

Je, kwa kuwa na sisi Zanzibar tunategemea lugha ya kiswahili ni lugha ya taifa, lakini katika nchi za kati mara nyingi huwa lazima utokee uzungumze kiengereza au ufundishe kiengereza ili upate usahihi wako.

(a) Wizara kwa makusudi ina wito gani hasa ukizingatia Mhe. Waziri wa Elimu, Waziri wa Habari, Mhe. John Pombe Magufuli kiswahili kakiweka mbele kuliko mambo mengineyo ili kujua umuhimu wa lugha hii. Wizara ina mpango gani wa kutoa agizo katika wizara zetu na katika taasisi nyengine wanapokuja wageni wazungumze lugha ya kiswahili ili wananchi wetu waelewe kinachozungumzwa pale kwa faida ya nchi yetu na linalozungumzwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi naomba atambue kwamba kuna lugha rasmi na lugha ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, lugha rasmi ni ile ambayo inatumika sehemu rasmi za kitaifa yaani kwenye mikutano maalum na ile lugha ya taifa ni ile lugha ambayo tunaitumia sisi wenyewe Watanzania. Lakini pia tunaitumia kwa nchi nyengine yaani Afrika Mashariki tunatumia lugha hii.

Kwa hiyo, naomba niseme kwamba huu ni mpango maalum wa wizara kuona kwamba lugha hii inatumika kwa nchi zote na sasa hivi nimwambie tu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kama miezi mitatu iliyopita nyuma tulikwenda Nairobi kwa ajili ya kuona kwamba tufanye makubaliano ionekane kwamba katika mikutano yetu ya Afrika Mashariki kwa kuwa sote tunakijua kiswahili tufanye kwamba katika mikutano hii tutumie lugha ya kiswahili. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 64

Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi

Mhe. Makame Said Juma - Aliuliza**:-**

Serikali imekuwa na utaratibu wa kuongeza nguvu za wakulima pamoja na wavuvi kwa kuekeza kwenye mipango mbali mbali.

Je, kuna mpango gani kwa Wizara kuekeza samaki baharini ili wavuvi wadogo wadogo wafaidike.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari 64 kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inaendelea kuimarisha Hifadhi za maeneo ya bahari kwa kuyaongeza na kuyatanua ikiwa pamoja na ushirikishwaji wa wananchi kwa madhumuni ya kuyalinda na kuyahifadhi kwa lengo ambalo Mheshimiwa amelisema. Pia Wizara yangu inaendelea kuhamasisha wananchi kuweka matumbawe bandia kwa ajili ya kuongeza samaki katika maeneo hayo ya hifadhi. Aidha, Wizara inaendelea kutoa taaluma kwa wavuvi wadogo wadogo kuhusu uvuvi bora ili wafaidike zaidi na mipango hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaona mashirikiano ya pamoja na Waheshimiwa kutunza mazingira yetu hasa ya baharini na kuwaelimisha wananchi wetu kutoharibu matumbawe na kuacha kutumia uvuvi haramu. Ahsante.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakumbukia sana au nafahamu sana mambo ya uvuvi ni fani yangu kubwa sana ambayo kuwa naweza kuiangalia bahari kuanzia mchana mpaka usiku na hivyo nimeitembelea bahari tena sana.

(a) Wizara inakusudia sana kuboresha uvuvi na kuwaboresha wavuvi ili wapate mapato yao kwa wakati wote kwa sababu ni masikini. Lakini wizara yenyewe inakataza sana kutumia vioo na mvuvi hawezi kufanya kazi kama hana kioo, mvuvi hawezi kufanya kazi kama hatapata viatu vya kuogolea. Lakini wizara hiyo imemzuia mvuvi huo kufanya hivyo na wakati mvuvi huyo huyo atakapoweka hifadhi zake au eneo lake la kuvua inalazimika kuogolea kwenda na akatia nyavu kuwakata wale samaki ambao kuwa ameekeza. Lakini sasa wizara inazuia kuzama sijui hapo imekusudia kitu gani.

(b) Wizara pia imesema kama itawaboresha wavuvi wadogo wadogo na itaekeza maeneo mbali mbali. Sijui imeekeza sehemu ngapi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu swali lake (b) kwa sababu swali lake la (a) sijalielewa baada ya maelezo yake marefu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hadi sasa wizara kama nilivyosema jana maelezo yake Mhe. Waziri katika mchango wake wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwamba tuna mpango sasa hivi kuna mradi umeanzishwa wa kuleta vifaranga na mpaka sasa tumeweka

Hatchery moja pale Maruhubi na sasa hivi *plan* inayoendelea ni miundo mbinu ya kutengeneza hiyo na mradi huu *in shaa Allah* Agosti utaanza kuleta vifaranga vyake milioni kumi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Naomba Mhe. Makame Said urejee swali lako la (a) ambalo Mhe. Naibu Waziri anasema hajalisikia.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti, swali langu niliulizia serikali imezuia kuvulia miwani, kwa viyoo maana yake nimekusudia na viatu. Je, ina malengo gani ya kuwaboresha wavuvi hawa au wavuvi hawa watawavua vipi wale samaki wakati wameshawekeza yale maeneo, watakuwa hawapati kuzama kwenye maeneo yale. Hilo ndio lilikuwa swali langu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake aliyoyatoa kwenye swali (b). Lakini napenda kuchukua fursa hii kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake (a) kama alivyozungumza.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba ajira nyingi zinazotoka na uvuvi huwa zinatumia miwani na viatu na zana nyengine za uvuvi na kuna uvuvi huwezi kuuendeleza bila ya kutumia vifaa hivi. Lakini katika sheria ya uvuvi, vilivyopigwa marufuku sio zile zana za kiyoo na viatu, ni aina ya uvuvi ndio inayopigwa marufuku.

Mimi nataka nimpe mfano mzuri tu Mhe. Mjumbe kwamba wageni wetu watalii wanapokuja hapa huwa wanatumia michezo kwenye bahari, wanafanya uogeleaji, wanafanya *snapping* wanafanya *diving*, vitu vyote hivyo vinatumia miwani na viatu, na havikupigwa marukufu kufanya hivyo. Kwa hivyo, katika ule uvuvi ambao umeruhusika hauna tatizo kuvua, hata kama unatumia nyavu zinazoruhusika ambazo ni lazima ukatazame samaki halafu ndio uweke zile nyavu, uvuvi ule huwa unaruhusika na wavuvi wale wanaendeleza ajira yao kwa kutumia viyoo na viatu. Kwa hivyo, tatizo lililokuwepo hapa sio utumiaji wa kiyoo na viatu na sio tatizo la kwamba ukivaa kiyoo, ukivaa viatu umepigiwa marufuku katika uvuvi. Kwa hivyo, aina ya uvuvi, uvuvi maarufu wa kutumia mabunduki yanayoharibu matumbawe hayo ndio yaliyopigiwa marufuku, makorokoro ambayo yote yanatumia zana hizo za viyoo na viatu. Lakini uvuvi wa makorokoro kutumia niseme neno gavu, lakini nataka kusema zile nyavu ambazo zina macho madogo, hizo ndizo zilizopigwa marufuku.

Kwa hivyo, kutokana na hali hiyo napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba watumiaji wavuvi waweze kutumia viyoo na viatu katika uvuvi halali ambao umeruhusiwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Mhe. Viwe Khamis kwa swali la nyongeza.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake alisema wizara yake inaendelea kutoa taaluma kwa wavuvi wadogo wadogo. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi hizi pamoja na wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, wavuvi hawa wadogo wadogo wapo kwenye visiwa ambavyo vimeizunguka nchi yetu. Kwa mfano, Kisiwa Panza, Kokota, Kojani, Tumbatu, na Fundo. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuweza kuwafikia wavuvi hawa wadogo wadogo ambao wako katika visiwa

hivi, na wavuvi hawa wanategemea zaidi uvuvi huu mdogo mdogo katika mahitaji yao ya kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu sio ina mpango tu, bali inawafikia wavuvi wa visiwa hivyo kote kama sio mimi basi waziri, katibu mkuu, ama mkurugenzi muhusika ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri ni maeneo mangapi ya hifadhi kwa Unguja na Pemba ambayo kwamba yamezuiwa ili kufanya hifadhi kwenye kuonesha masuala ya utalii.

(b) Kwa kuwa wavuvi wengi ni wadogo wadogo na kuna sheria nyingi ambazo zinawabana. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wamewapatia vyombo vya kuvua bahari kuu wavuvi hawa wadogo wadogo, ili kuondokana na hii kadhia inayowafika kila siku ya kunyanyaswa kule baharini badala ya kuvua ule uvuvi ambao unakatazwa na waweze kufikia kule kwenye bahari kuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti,

(a) Mhe. Mjumbe anataka kujua uhalisia wa maeneo mangapi ambayo sasa hivi tumeyahifadhi kuzuia. Maeneo ya hifadhi ambayo tumezuwia uvuvi haramu, naomba nikujibu kwa maandishi.

(b) Serikali kama ilivyosema kwamba, na kama jana ulisikiliza vizuri majibu ya Mhe. Waziri, tuna mpango wa kuanzisha hawa wavuvi wadogo wadogo kuwawezesha ili kuvua katika maji marefu. Vile vile tutakaponunua hizo boti ndipo tutakapowachukua wavuvi hao wadogo wadogo na kuwapa taaluma ya kuvua bahari kuu, ili na wao waweze kujiongezea kipato chao zaidi. Ahsante.

Nam. 49

Ahadi ya Rais ya Kupeleka Umeme Kiwani

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Moh'd Shein alipokuwa katika ziara zake kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, katika jimbo la Kiwani, aliahidi kwamba atakapochaguliwa atapeleka umeme katika vijiji ambavyo havijafikishiwa umeme kama vile Kitondooni, Mtakafu, Mivumoni na vyenginevyo.

a) Je, Mhe. Waziri ahadi hii unaifahamu.

b) Ni lini vijiji hivi vitapatiwa umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 49 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, napenda ifahamike kwamba, ahadi zote anazozitoa Mhe. Rais ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika kipindi husika. Miongoni mwa sera kuu za serikali ni kuwapatia huduma za kijamii wananchi wa Zanzibar popote walipo ikiwemo huduma hii ya umeme. Utekelezaji wa ahadi na sera hizo hufuata mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kutegemea na aina ya mradi husika.

Aidha, vijiji alivyovianisha Mhe. Mwakilishi katika swali lake, napenda kumfahamisha kuwa vijiji hivyo vimo katika mpango wa wizara yangu wa usambazaji umeme vijijini kwa mwaka ujao wa fedha 2017/2018. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Je, kwa kuwa vijiji hivi nilivyovitaja viko katika Jimbo la Kiwani, na vijiji hivi ni vikubwa. Je, Mhe. Waziri keshawahi kuvitembelea na akavijua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, tayari vijiji hivi nimevitembelea katika safari yangu niliyokuwa nimerudi Pemba hivi karibuni ahsante.

TAARIFA YA MWENYEKITI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaendelea nina taarifa mbili hapa. Taarifa ya kwanza, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *CPA* ya Baraza la Wawakilishi anawatangazia wajumbe wote wa kamati husika kuhudhuria kikao cha kamati hiyo saa 5:00 asubuhi katika ukumbi wa kamati nambari 2.

Taarifa ya pili inahusu wageni wetu wa leo, ni wageni wa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pemba Juma. Hawa ni wanafunzi waliopata daraja la kwanza, yaani *Division One* mwaka 2017 *Form Four*. *(Makofi)*

Wanafunzi wenyewe ni kama hawa wafuatao.

1.	Khadija Rashid Omar	-	Lumumba
2.	Abdul-razak Machano Hassan	-	Lumumba
3.	Nasma Talib Saleh	-	SOS
4.	Said Amour	-	SOS
5.	Munnir Seif Khamis	-	High View
6.	Salum Salaha Salum	-	High View

7.	Fahad Bakari Hassan	-	Kiembesamaki
8.	Ahlam Abdalla Mohammed	-	Istikama
9.	Yussuf Said Masoud	-	Istikama
10.	Daud Arnest Maige	-	Francis Maria
11.	Sara Nuhu Salanya	-	Francis Maria
12.	Suleiman Gavas Mbili	-	Glorious
13.	Khairat Omar Kombo	-	Glorious
14.	Abdul-wahid Khamis Masoud	-	Biashara
15.	Abdalla Salum Abdalla	-	Biashara
16.	Mohammed Ali Ali	-	Kiponda
17.	Shufaa Khamis Mussa	-	Kiponda
18.	Yusra Ayoub Saleh	-	Vikokotoni
19.	Ibrahim Mwalim Ali	-	Vikokotoni
20.	Arafa Mohammed Mbarouk	-	Tumekuja
21.	Yussuf Salum	-	Tumekuja
22.	Asha Mohammed Mabrouk	-	Ben bella
23.	Ahlam Abdi Suleiman	-	Ben bella
24.	Sumaiya Omar Mussa	-	Feza
25.	Ramadhan Mwinyi Pembe	-	Feza
26.	Safia Halal Hemed	-	Laurent
27.	Ahmed Khatib Pandu	-	Laurent

Wanafunzi hawa wamefuatana na walimu wao watano na maafisa watatu kutoka Wizarani, karibuni sana lakini tunawapongeza sana kwa jitihada zenu *(Makofi)*

Nam. 69

Usumbufu kwa Abiria Watoto Katika Mapinduzi II

Mhe. Ali Khamis Bakar - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi inastahili pongezi kwa kuwaondolea usumbufu wananchi kwa kununua meli ya MV Mapinduzi II ili kutoa huduma bora. Hata hivyo, tumeshuhudia usumbufu mkubwa kwa abiria pale wanapo safiri na watoto kwa kutakiwa wakate nusu tiketi.

(a) Ni umri gani wa mtoto anaesafiri unaotakiwa kukatiwa nusu tiketi kwa mujibu wa Sheria za usafiri.

(b) Ni kwa nini Shirika la Meli haliweki kiwango cha kima cha pesa tu cha mtoto na umri unaofaa kulipa kima hicho cha pesa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 69 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Usalama wa Vyombo vya Baharini ya mwaka 2008, wafuatao watatakiwa kulipia kama ifuatavyo:-

(a) Mtoto mchanga na mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano (5) hawapaswi kulipia nauli.

(b) Mtoto mwenye umri wa miaka mitano (5) mpaka miaka kumi na moja (11) anatakiwa kulipia asilimia hamsini (50%) ya bei atolipia mtu mzima kwa mujibu wa bei ilyopangwa siku ya safari hiyo.

(c) Watoto wa miaka zaidi ya kumi na moja (11) pamoja na watu wazima watalipia bei kamili ya tiketi kama iliyopangwa siku ya safari hiyo.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza suali la nyongeza.

Kwanza nazipongeza juhudi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuondoshea wananchi shida katika taasisi mbali mbali hapa Zanzibar, baada ya pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia Meli hii ya MV Mapinduzi II pamoja na AZAM, siku za safari wananchi wanapata shida wanasokotwa na watoto kwa kulipishwa nauli kinyume na sheria.

a) Je, Mhe. Waziri umeshawahi kufanya ziara za safari za meli hizi kwenda kujionea hali halisi.

b) Mhe. Naibu Waziri hatuoni kwamba mtoto huyu ambaye ana umri wa miaka 11 tunamkosesha haki yake y msingi kwa kumlipisha nauli ya mtu mzima kabla hajatimia umri wa miaka 18.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Nataka kumhakikishia kwamba watu wetu wote wanakuwepo pale watu wa mamlaka ya usafiri baharini, kwa hivyo iwapo kutatokea kitendo chochote kile cha kuzidishwa bei basi wao wanachukua hatua haraka kuzuia tatizo hilo.

Lakini nataka kumhakikishia kwamba tiketi zote zinakuwa zinakatwa sehemu husika, kwa hivyo pale wanapokwenda watu wanakwenda kupanda, kama kuna tatizo hilo nitamuomba mimi tukae pamoja tuliangalie.

Lakini suala lake la (b) Kwa nini mtoto analipishwa nauli miaka 11 nauli kamili, nataka kumwambia kwamba hizi ni kanuni ambazo tumeziweka, lakini vile vile hizi kanuni sisi wakati wowote kama tunahisi kuna uhitaji wa kufanya marekebisho basi tutazifanyia marekebisho.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wasafiri wengi wa meli ni wanawake na kwa kuwa wanawake wanaposafiri huwabeba watoto wao wote, na huenda ikawa wanawake hao wengi ni wajane na wajane hao huwa hawana wa kuwahudumikia.

Je, Serikali haioni haja ya kuondoshea nauli watoto wenye umri chini ya miaka saba 7.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama tulivyosema hizi ni kanuni ambazo zimewekwa na ambazo sisi tunatakiwa tuzifuate, kwa hivyo sasa kama nilivyosema kwa Mhe. Ali Khamis Bakari, kama kuna mambo mengine tutayachukua kwa ajili ya ushauri na baadae hali itakaporuhusu kutokana na kuangalia vile vile tija inayopatikana katika gharama za usafiri kwa hali ya chombo husika, na vile vile faida ambayo inatakiwa kwa chombo kile kipate basi tutalichukua hili. Kama litawezekana tutalifanyia kazi.

Nam. 74

Ukarabati wa Barabara za Chambani

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:

Wananchi wa Chambani wanampongeza Mhe. Rais kwa kuzifanyia matengenezo barabara za Unguja na Pemba. Pamoja na jitihada hizo zipo baadhi ya barabara ambazo zinahitaji matengenezo ili ziweze kutumika vizuri

Je, barabara za Mgagadu – kwa Mkoba, Temi, Kalani – Sisimizi, Ngwachani - Tangaani ni lini zitafanyiwa matengenezo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Barabara za Mgagadu – kwa Mkoba, Temi, Kalani- Sisimizi, na Ngwachani – Tangaani ni za ndani na kwa mujibu wa Sheria barabara hizi zinasimamiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Licha ya hivyo kama nilivyojibu hapo kabla kama kutaonekana kuna uwezekano wa kuzitengeneza barabara hizi hali inaporuhusu basi tutakaa na Waheshimiwa Wawakilishi, ili kuhakiha kwamba zile barabara tunazifanyia matnengenezo ili zipate kupitika kwa urahisi, na mimi kweli nimeziona hizi barabara ziko katika hali ngumu lakini nitamuomba sana Mhe. Muwakilishi tushirikiane pamoja katika kuhakikish kwamba angalau zinapitika barabara zile hasa barabara ya Ngwachani ambako kuna Skuli kule ambako wanafunzi wetu wanakwenda kusoma.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri, mwaka 2010 Mhe. Rais wa Zanzibar aliweka ahadi nyingi kutengenezwa kwa barabara zote Unguja na Pemba, mojawapo ikiwemo barabara ya Matale/Chambani na mpaka leo barabara ile bado haijatengenezwa.

Naomba kujua kwamba barabara ile iko Tawala za Mikoa au iko katika Mawasiliano, na kama ipo Mawasiliano naomba uwaambie wananchi wa Matele lini barabara hiyo itafanyiwa matengenezo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama ulivyosema ahadi zote za Mhe. Rais basi kwetu zinakuwa ni agizo na hatuna budi kuzitekeleza, nitakaa na Mhe. Muwakilishi ili anambie ahadi hiyo ilitolewa wapi ili baadae sisi tukae pamoja, ahadi zote kama nilivyosema zile zilizo katika ilani na nyengine zilizotolewa na Mhe. Rais basi zinakuwa chini ya Wizara yetu, kwa hivyo tutahakikisha kwamba kama hiyo ahadi imetolewa na Mhe. Rais basi tutakuwa pamoja tuhakikishe kwamba tunaifanyia kazi, kwa hivyo kipindi gani namuomba anipe muda kwa sababu tunataka barabara zote tuzitengeneze kwa kiwango cha lami, lakini hali ya fedha kwa hivyo tunamuomba tukae pamoja aniambie hiyo barabara na baadae tutalifanyia kazi suala lake.

Nam. 98

Mikakati Zaidi ya Kudhibiti Malaria

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali imekuwa na juhudi kubwa ya kupambana na malaria kwa kupiga dawa majumbani na kutoa vyandarua kwa wananchi wake wa Zanzibar. Na kwa kuwa taarifa zinaonesha kuwa malaria imepunguwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 lakini watoto wenye umri wa miaka 6 na kuendelea ripoti inaonyesha kwamba bado malaria ipo kwa asilimia ndogo.

(a) Ni sababu gani inayopelekea watoto kuanzia umri wa miaka 6 hadi 14 kuendelea na tatizo la kupata malaria.

(b) Je, ni hatua gani za msingi ambazo Serikali imeamua kuchukuwa juu ya kuzuia tatizo hilo pamoja na mpango wa kuwaangamiza mbu wanaosababisha malaria aina ya **cutex.**

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuangamiza mazalio ya mbu nje ya majumba ambapo kwa sasa dawa hizo hupigwa ndani ya nyumba tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye kifungu (a), (b) na (c) nitajibu kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ningependa pia kufanya marekebisho kidogo kwenye suala No. C ambapo sehemu ya maelezo ya suala yanasema naomba ninukuu.

"Pamoja na mpango wa kuangamiza mbu wanaosababisha malaria aina ya *Culex* Mhe. Mwenyekiti, naomba nirekebishe kidogo hapa kwa kusema mbu aina ya Culex hana nafasi katika maambukizi ya ugonjwa wa Malaria basi mbu huyu huwa anaambukiza maradhi ya matende. malaria huambukizwa na mbu jike aina ya *Anopheles.*

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya kitengo cha kumaliza malaria Zanzibar kimejipanga kuendeleza mpango wake wa kutia dawa za kuua vilui lui katika mazalio ya mbu wanaoambukiza malaria hasa hasa katika maeneo yenye maambukizi endelevu, kama tunavyofahamu kwamba Malaria hivi sasa yamepungua kwa kiasi kikubwa na kubakia katika baadhi ya maeneo. Hivyo shabaha yetu ni kuangamiza vilui lui kama maeneo hayo na sio sehemu zote za Unguja na Pemba, hii inatokana na maelezo ya Shirika la Afya Ulimwenguni *WHO* kwamba ni vigumu kuangamiza viului lui wa mbu katika kila eneo hasa ukizingatia kwamba dawa hizi zinatiwa kila wiki au kila baada ya wiki mbili kutegemea na aina ya dawa inayotumika. Lakini pia hali halisi ya upatikanaji wa fedha na gharama za kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa jamii tunatoa wito kwa wananchi kusafisha mazingira ya maeneo ili kupunguza uwezekano wa kuwepo mazalio ya mbu kwenye maeneo yanayotuzuguka tunawashauri wananchi kutupa taka taka kwa utaratibu unaokubalika na sio kuziacha ovyo ovyo makopo, mipira ya magari pamoja vitu kama hivyo ambavyo hutuwamamisha maji na kusababisha mbu kuzaliana. Wananchi pia tunawashauri kufukia vidimbwi na kutumia vifusi vya udongo au kuyatiririsha maji kutoka kwenye vidimbwi vidogo vidogo katika maeneo yetu, kazi hizi zinaweza kufanyika na kufanyika na kusimamiwa ngazi ya Kijiji/Shehia, nawaomba wananchi tusikae kuisubiri Serikali ije kutusafishia maeneo yetu yaliyotuzunguka jambo ambalo limo ndani ya uwezo wetu.

Mhe. Omar Said Abeid: Asante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye vipengele a, b na c kama ifuatavyo.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini nina suali langu linasema kwa kuwa Mhe. Naibu umekiri kuwepo kwa maambukizi hasa kwenye jibu lako mama la watoto wa kuanzia miaka sita na kuendele.

a) Je, Wizara haioni kwamba iwapo itashindikana kupiga dawa kwenye mazalio ya hivyo vilui lui vinavyosababisha kuzaliwa hao mbu wanaoleta malaria Wizara haioni kwamba ile adhma ya Serikali ya kuwa Zanzibar bila ya malaria inawezekana itakuwa imepotea.

b) Je, kwa kuwa kumetajwa kwamba ni maeneo maalum ambayo yanapigwa dawa haya kwa ajili ya kuangamiza maeneo yenye vimelea vya mazalio ya mbu, je ni maeneo gani hayo maalum ambayo yamepangwa kupigwa dawa kuteketeza hayo mazalio ya mbu wa malaria ambayo inaonekana kwamba malaria yaop kwenye hayo maeneo.

c) Mpango huo wa kupiga dawa kwenye hayo maeneo tayari umeanza na kama bado ni lini utaanza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Waziri naomba ujibu suala lake moja lenye kitoto A na B kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kazi hii ya upigaji dawa katika nchi yetu hivi sasa inaendelea kwenye maeneo yetu, Serikali hivi sasa inaendeleza upigaji wa dawa katika baadhi ya maeneo na ni maeneo maalum ambayo yanaonekana kwamba ugonjwa wa Malaria upo, hii inaonekanaje ni baada ya hospitali zetu kupokea wagonjwa wengi kutoka katika maeneo hayo basi takwimu huwa zinatwambia kwamba katika maeneo hayo ugonjwa wa Malaria upo na Wizara huzielemea zaidi sehemu hizo katika kupiga dawa na kutoa elimu kwa wananchi.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Asante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika majibu yake alisema kuwa wanaendelea kutia dawa hasa katika maeneo yenye maambukizi endelevu, Je, ni maeneo gani hayo ambayo yana maambukizi endelevu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe.Bahati Khamis Kombo swali lake la nyongeza ambalo aliliuliza Mhe. Omar Seif, lilikuwa ni (c) lakini sikuweza kulijibu na Mheshimiwa kauliza tena. Mhe. Naibu Spika, katika Kisiwa cha Unguja tuna maeneo 6 ambayo kwetu tunayaita ni *pilot area,* maeneo yenyewe ni kama haya yafuatayo; Cheju, Uzi, Ng'ambwa, Kilimani, Kwabint Hamran na eneo la Tunduni. Hayo mengine matano yameshapigwa dawa lakini hili la Tunduni wakati wowote kuanzia sasa litaanza kupigwa dawa.

Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba maeneo yake ni; Kisiwa Panza, Tibirinzi, Wambaa na kwa Kaskazini Pemba ni Tumbe. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 24

Kutokuwepo kwa Chumba cha ICU Hospitali ya Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Hospitali ya Chake Chake haina Chumba cha wagonjwa mahututi (*ICU*).

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga chumba hicho pamoja kuweka vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 24 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Hospitali ya Chake Chake haina chumba cha wagonjwa mahututi (ICU). Hali hii si kwa hospitali ya Chake Chake tu bali hospitali zote za Wilaya na Vijiji kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali pekee iliyokuwa na huduma hii kwa Unguja ni hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja na kwa Pemba ni hospitali yetu mpya ya Abdalla Mzee. Hivyo wagonjwa wote wanaohitaji huduma hiyo kwa mujibu wa muongozo wa daktari hufikishwa katika hopitali hizo mapema ili kupata huduma hizo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na ahsante Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri. Mheshimiwa awali ya yote nasema nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Ali Muhammed Shein kwa kupandisha mji wa Chakechake kuwa Mji Mkuu nambari mbili Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali iliyokuwepo Chakechake sasa hivi itakuwa ipo kati kati ya Mji Mkuu, na watu wote takriban huwa wanatoka majumbani asubuhi wengi wao kuelekea Mji Mkuu. Huoni umuhimu wa kuwekwa ICU Chakechake mpaka mtu atoke pale kupelekwa Mkoani wakati masafa zaidi ya kilomita 20.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hilo tunalichukua kama ni shauri hali itakaporuhusu ni kweli upo umuhimu wa kuweka ICU katika hospitali ya Chakechake lakini pia katika hospitali ya Wete, Kivunge na hospitali nyengine za Wilaya. Ahsante.

Mhe. Zulfa Omar Mmaka Omar: Asante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri swali langu lenye kitoto (a) na (b). Katika hospitali ya Chakechake tunaona kwamba ni hospitali ambayo inachukua wagonjwa wengi kutoka maeneo mengi. Lakini katika hospitali hii katika chumba cha kuzalia kumekuwa kunatatizo ambalo linajirejea mara kwa mara nao ni ukosefu wa vifaa tiba katika wodi ile. Pia katika wodi ile ile kuna tatizo ambalo linasumbua la AC na tunajua hali ya wazazi wakienda kwa ajili ya kujifungua.

a) Je, ni lini suala hili litamaliza
b) Katika hospitali hiyo hiyo ya Chakechake maeneo ya bondeni kuelekea Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuna eneo ambalo mnalitumia hospitali ya Chakechake kwa ajili ya kuhifadhia takataka zenu eneo lile kwa sasa hivi lina tatizo la harufu mbovu harufu ile inatokana ma- *placenta* ambayo yanapelekwa pale kwa ajili ya kuhifadhiwa au sijui kwa ajili gani. Je, ni lini tatizo lile la harufu mbovu mtalitatua kwa kuyaweka sehemu salama madude yale na kuhatarisha hali ya wafanyakazi ambao wanakwenda kuyatia madude yale katika sehemu ile, na vijana ambao wanatumia eneo lile kwa ajili ya mazoezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, suala la AC pamoja na vifaa katika wodi ya *maternity* hospitali ya Chakechake. Vifaa kwa wakati huu vipo isipokuwa ni vichakavu, lakini Wizara yangu inampango maalum wa kurekebisha au wa kuweka vifaa vipya katika hospitali zote ikiwemo Hospitali ya Chakechake. Mpango huo tayari unatayarishwa kwa ajili tumegundua kwamba vifaa vingi baadhi ya hospitali zetu ni vya muda mrefu. Huwa tunabadilisha baada ya kupata taarifa kwamba hali ya hapa ni hivi na hivi. Lakini kwa sababu tumeshapata taarifa ya Chakechake na nilitembelea nikaona na nikatoa maagizo kwamba vifaa vile virekebishwe.

Baadhi ya sehemu walirekebisha, lakini sina hakika vizuri katika *maternity ward*. Namuahidi kwamba tutafatilia kama huko bado hawajabadilisha kuweka vifaa vyengine basi tutalichukua na utalifanyia kazi.

Kuhusu suala la AC tunamatatizo katika hospitali zetu ya AC nyingi. Kwa bahati nzuri wizara ina mafundi, sasa hivi tumo katika ukarabati wa kufanya AC zote ambazo zimegoma ili kugundua ni zipi ambazo zitakubali kuendelea na kazi tuzifunge katika sehemu mbali mbali na pale ambapo zitagoma kabisa basi tumo katika kufanya mpango wa kutafuta AC nyengine kuzi *fit* katika sehemu ambazo zinahitaji AC.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi, yeyote ambaye ataguswa na jambo hili na uwezo anao hii ni sadaka, mnajifanyia wenyewe kwa maisha yetu ya baadae, akhera. Nawaomba sana pamoja na kwamba mnatoa misaada mingi katika sehemu mbali mbali basi mlione pia na tatizo hili la AC katika hospitali zetu ikiwemo hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Kama alivyofanya Mheshimiwa Mama Asha Balozi Mke wa Mhe. Makamo wa Pili, yeye alitembelea na kwa bahati nzuri akaliona lile tatizo ambalo hata sisi Wizara tumeshaliona na kulipangia mikakati kwamba katika pesa ambazo tutazipata katika kipindi hichi basi tukasimu

tuache kufanya hili na hili lakini tuhakikishe tunalifanya hili la AC ni muhimu. Yeye alipoliona hakusubiri hilo alitoa tu alichonacho. Maana kutoa si utajiri, kutoa ni moyo wa mtu na yeye Mwenyezi Mungu alimjaalia akatoa na tukapata AC mbili ambazo sasa hivi zinawashughulikia wagonjwa.

Pia Mhe. Makamo wa Pili alifanya ziara katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja na hili nalo akaliona katika kipindi hicho hicho yaani *even two days* baada ya kutembelea Mheshimiwa Mama, basi akaliona na alipoliona na yeye akatwita akatupa maelekezo na kwa bahati nzuri maelekezo yale yalikuwa ni maelekezo bora zaidi ya yale ambayo niliyatoa miye, aliboresha zaidi basi tunayaendeleza, tunayatekeleza na sasa hivi wakati wowote kuanzia sasa tunaweza tukapunguza tatizo hili la AC.

Lakini bado nawambia tunahitaji AC 24 katika hospitali zetu kwa hivyo tunaomba sana atakaeguswa na jambo hili na ni lazima liwaguse kwa sababu ni AC ambazo zitawasaidia wagonjwa ambao ni wananchi wetu ambao wametupigia kura. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimesikia kuhusu utaratibu, lakini nakuomba ukae tuendelee na shughuli zetu. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kuna tangazo hapa limeletwa kwa wale washabiki wote ya Yanga African Team na saidia Yanga ishinde wanatakiwa wakutane mara tu baada ya kipindi cha Maswali kuna jambo la kujadili hapo nje kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Haji Omar Kheir. Naomba tuendelee Mwenyekiti wa Ustawi wa Jamii.

HOJA ZA KAMATI

Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2016/17

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba sasa kuchukua wasaa huu wa kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa uwezo wake wa kutukutanisha katika ukumbi huu tukiwa na nguvu, wazima wa afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kuwawakilisha wananchi kupitia chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa katiba, sheria na Kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na wewe kwa kuniruhusu kusimama hapa mbele ya Wajumbe wako, na kwa niaba ya Kamati kuwasilisha kwa ufupi hotuba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ikihusu ripoti ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inasimamia Wizara mbili ambazo ni Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Kwa kipindi cha mwaka mzima

Kamati imefanyakazi na Wizara hizi kwa ukaribu sana. Nachukuwa fursa hii adhimu kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Harous Said Suleiman na watendaji wao wote kwa ushirikiano wanaoipa Kamati katika kipindi chote cha mwaka mmoja, pamoja na watendaji wakuu wote akiwemo na Afisa Mdhamini wa Wizara ya Afya Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nawashuru pia kwa dhati kabisa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Riziki Pembe Juma na Mhe. Naibu Waziri wake Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, Katibu Mkuu, Manaibu wake akiwemo pia Afisa Mdhimini Pemba pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Elimu, kwa mashirikiano yao makubwa wakati wa kazi za Kamati. Tunawapongeza kwa kuwa pamoja kila mahala Kamati inapowahitajia.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nikiri kuwa kazi za Kamati ni ngumu na zina changamoto nyingi, lazima kuwepo mashirikiano baina ya Ofisi yako, Ofisi ya Baraza na Wajumbe wa Kamati na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Nakupongeza na Naipongeza Ofis ya Baraza ambayo inatumia kila nyenzo zilizopo katika uweozo wake kuhakikisha kuwa kamati zinafanikisha kazi zake katika muda na wakati uliopangwa. Aidha, naomba nimpongeze Mhe. Spika, kwa miongozo anayozipa Kamati za Kudumu za Baraza ambayo wakati wote inasaidia kupunguza changamoto mbali mbali zinazokabili Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii wamekuwa pamoja karibu katika kila kazi za kufuatilia utendaji wa Wizara na mara kadhaa wamefanyakazi hizo kwa kujitolea zaidi. Hali hiyo imetokana na uchapakazi, ukomavu na umakini wa Wajumbe wa Kamati hii, ambao kutokana na umuhimu wa sekta wanazosimamia za afya na elimu, imewalazimu kusahau malipo na kutumia nguvu na nyenzo zao katika kufanyakazi bila kuchoka ili kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma za afya na elimu kama inavyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, naomba kuchukuwa nafasi hii kuwatambua wajumbe hao wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame	Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hidaya Ali Makame	Mjumbe
4. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mjumbe
5. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
6. Mhe. Makame Saidi Juma	Mjumbe
7. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	Mjumbe
8. Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, wakati wote wa kazi za Kamati yetu, tumekuwa pamoja na Makatibu wetu wawili ambao ni watendaji katika Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, ambao ni:-

1. Ndg. Aziza Wazir Kheir
2. Ndg. Khamis Hamadi Haji

Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru sana makatibu wetu hawa ambao wanashirikiana vizuri na Mwenyekiti na Wajumbe katika kupanga na kuratibu kazi za kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti yetu ya kamati imejielekeza katika mambo mbali mbali ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambayo kamati imeyaona wakati wa kazi zake za kawaida. Katika sekta hizo mbili muhimu katika ustawi wa jamii, Kamati yetu imeziweka katika namna tatu.

- Kwanza, kamati imetambua mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya na elimu. Kamati imetembea na kukagua kazi na shughuli mbali mbali za Wizara kama inavyoonekana kwenye ripoti na kuona hatua za maendeleo zilizopatikana.

  Hatuna budi Kamati kupongeza kwadhati kabisa juhudi ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi Mhariri wa Rais Dokta Ali Muhammed Shein kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta hizi mbili.

- Pili, ripoti ya Kamati imetaja changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi, aidha kamati inatambua juhudi, mipango na mikakati ya Serikali katika kuzitatu changamoto hizo.

- Na tatu, ripoti ya Kamati imeweka maoni na ushauri wa Kamati kuhusu namna ya kuzitatua changamoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, lengo letu ni kuishauri Serikali, sote tunajenga nyumba moja tukiwa na wajibu wa kushauriana ili tufanikishe lengo kuu la Serikali la kuleta ustawi wa maisha ya wananchi wake. Kwa msingi huo Kamati imetoa maoni, ushauri na ilipobidi tumejaribu kuagiza hatua muafaka zichukuliwa ili kukabili changamoto ambazo haziwezi kusubiri muda mrefu hasa katika huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo mfupi naomba sasa uniruhusu nitowe muhutasari wa ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ambayo kwa kirefu imewekwa katika kitabu ambacho Waheshimiwa Wajumbe wako wamepatiwa, naomba sasa kwa ruhusa yako nianze na Wizara ya Afya.

Wizara ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Kamati tumetambuwa hatua zilizofikiwa za kuimarisha sekta ya afya. Nichukuwe fursa hii kwa mara nyengine tena kama nilivyosema awali kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa juhudi zake kubwa zilizopelekea kufikiwa mafanikio katika sekta ya afya katika kipindi cha uongozi wake, uhakika vision yake ya mabadiliko katika sekta ya Afya ni ya kuungwa mkono na sisi sote na hasa kwa kuzingatia kwamba tunaufinyu wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inakiri kuwa licha ya vipaumbele vingi katika kuimarisha sekta ya afya, Mhe. Dkt. Shein amejitahidi kufanikisha mambo muhimu na ya msingi ambayo yatabakia kumbukumbu ya wakati wa uongozi wake, na mimi kwa heshima kubwa naomba uniruhusu niyatambuwe baadhi yao kama ifuatavyo:-

- Mhe. Rais Dkt Ali Muhammed Shein amefanyakazi kubwa katika kufanikisha ujenzi mpya wa Hospitali ya Abdalla Mzee, Mkoni Pemba, ambayo imejengwa upya na ndugu zetu Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, na Hospitali hiyo inaendelea kutoa huduma ikiwa na vifaa vya kisasa kabisa.

- Ujenzi wa jengo jipya la Wodi ya Mama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi mmoja, likiwa la kisasa zaidi, umethibitisha kuwa Serikali bado inawekeza kadiri inavyoweza katika afya za wananchi wake.

- Kuimarisha huduma za mama wajawazito kwa kuondoa malipo ya huduma hizo, pamoja na kuimarisha miundombinu ya *ICU* kuwa ya kisasa, kwa hili pia Kamati yetu inampongeza sana Mheshimiwa Rais.

- Kuendelea kupata mafanikio katika mradi wa *"kumaliza malaria Zanzibar"*, ambapo nchi yetu imeendelea kuwa mfano wa kuigwa katika juhudi za kupambana na ugonjwa huo.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona niyataje hayo machache kuliambia Baraza lakona wananchi kwa ujumla kuwa Serikali ya Dkt. Ali Mohammed Shein inatekeleza kwa vitendo ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015-2020 ya kuimarisha huduma za jamii katika sekta ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya kamati imeonesha pia mafanikio yaliyofikiwa katika mageuzi ya kitaasisi ya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kuelekea Hospitali ya Rufaa. Kamati yetu imepitisha Mswada wa Sheria ya kuanzisha Taasisi hiyo na baadaye Baraza hili kupitisha kuwa sheria kamili tunakupongezeni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi hiyo. Hivi sasa Taasisi ya Hospitali ya Mnazimmoja imekuwa wakala kamili wa Serikali unaojitegemea kwa baadhi ya mambo ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka huu kamati yetu pia imepitia mswada wa marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambayo sasa itakuwa Wakala wa Serikali wa Chakula na Dawa ambayo itakuwa ni taasisi inayojitegemea. Hatua hii nayo ni kubwa kwa kuwa inakipa nguvu chombo hiki katika kufanikisha kazi zake mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo ambayo nimetangulia kuyaeleza, kamati yetu imeendelea kufutilia utekelezaji wa vipaumbele vya Bajeti inayotumia Programu (PBB) ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Utekelezaji wa vipaumbele hivyo umewekwa katika programu kuu nne ambazo ni Programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Programu ya Tiba, Programu ya Usimamizi wa Sera ya Afya na Utawala na Programu ya Hospitali ya Mnazimmoja.

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Kamati imeonesha jinsi Kamati ya Ustawi wa Jamii ilivyopata fursa ya kutembelea vituo mbali mbali vya afya Unguja na Pemba na kuona utoaji wa huduma za afya kwa wananchi unavyofanyika.
Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilitembelea vituo vya afya vya msingi, daraja la kwanza na la pili ambavyo kwa ujumla vinatoa huduma zake vizuri licha ya changamoto za hapa na pale. Katika kupitia na kuvikagua vituo hivyo, kamati imeona changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha na

vitendea kazi hasa kwa upande wa Pemba kama inavyoelezwa katika ripoti ya Kamati. Kamati imetoa mapendekezo yake ya namna ya kutatua changamoto hiyo kuhakikisha kwamba bajeti kwa ajili ya vituo vya afya inapatikana kama ilivyopangwa ili vituo hivyo viweze kukabili changamoto ndogo ndogo ambazo hazihitaji fedha nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya afya ni suala la msingi sana ni muhimu kwa wananchi katika kupambana na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Kamati yetu imejifunza kuwa maradhi yasiyoambukiza kama vile shinikizo la damu, kusukari, saratani, ajali za barabarani na pumu ni miongoni mwa maradhi yanaoongoza kwa vifo nchinimwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inatoa wito kwa wananachi sote kuchukuwa tahadhari kabla ya athari, na kutongoja mpaka maradhi yawasibu ndo waende Hospitali badala yake, kama tunavyoelimishwa na wataalamu wa afya, tuwe na utamaduni wa kujikinga maradhi hayo kwa kufanya mazoezi, kuepuka matumizi ya pombe na tumbaku na kuzingatia ulaji bora ambao una lishe kamili.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ya Ustawi wa jamii inasisitiza sana wananchi wawe na tabia ya kupima afya zao kila mara, ili kujihakikishia hali zao za kiafya na kuchukuwa hatua mapema pale yanapobainika matatizo. Utamaduni wa kusubiri kwenda Hospitali mpaka mtu aumwe umepitwa na wakati katika zama hizi ambazo maendeleo ya kijamii na kiuchumi yamekuwa makubwa na huduma za afya zimefika kila mahala.

PROGAMU YA HUDUMA ZA TIBA

Mhe. Mwenyekiti, huduma za tiba katika Hospitali zetu zimeimarika hasa baada ya kukarabati miundombinu ya majengo ya Hospitali kama vile Mnazimmoja, Abdalla Mzee na Hospitali za Wilaya. Ripoti ya Kamati imebainisha changamoto ya fedha na vitendea kazi ambavyo vinahitaji kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma hasa kwa Hospitali za Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imetembelea Hospitali ya Kivunge na kuona namna inavyoelemewa katika utoaji wa huduma. Itakumbukwa kwamba Hospitali ya Kivunge awali ilikusudiwa kuhudmia shehia saba tu, lakini hivi sasa kutokana na sababu mbali mbali, Hospitali hiyo inahudumia Mkoa mzima wa Kaskazini. Kamati imeshauri katika ripoti yake kwamba Serikali ifanye juhudi ya kuongezea fedha na vifaa au vitendea kazi ili Hospitali ya Kivunge iweze kumudu kuhudumia ongezeko hilo la wagonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeona pia kuwa baadhi ya vituo vya Afya vipo katika hali mbaya na vinahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa kama siyo kuvunjwa na kujengwa upya. Tunapongeza Taasisi zisizokuwa za Kiserikali ambazo ni wahusika wakubwa kuchangia maendeleo ya sekta ya afya, na kwa kuweza kusaidia ukarabati na ujenzi wa vituo hivyo, kamati yangu inawapongeza ndugu zetu wa *Milele Foundations* ambao bado wapo bega kwa bega na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kusaidia uimarishwaji wa vituo vya afya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Kamati yetu imejaribu konesha changamoto za Bodi mbali mbali katika sekta ya afya kama vile Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, ambayo hivi karibuni Baraza hili limepitisha kuwa sheria, mswada wa Marekebisho ya Bodi hiyo. Kamati imesisitiza maslahi ya watendaji wa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kuwa wafanyakazi wake wanakuwa katika hatari ya kurubuniwa endapo watakuwa hawatazamwi vizuri kwenye maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeripoti kuhusu Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala ambalo kuna mapendekezo Kamati imetowa yafanyiwe kazi. Lakini kubwa ambalo kamati inasisitiza Baraza lipewe nyenzo na uwezo wa kusimamia vizuri kazi zake. Kamati imegunduwa kuwa wapo baadhi ya watu wanajihusisha na tiba asili bila ya leseni wala kusajiliwa vilinge vyao. Kamati pia imebaini zipo dawa asili zinauzwa katika maeneo ya ibada, kwenye mikusanyiko na mitaani ambazo hazijafanyiwa uchunguzi na wananchi wanaendelea kuzitumia.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inachukuwa nafasi hii kutoa wito kwa wanachi kuacha kutumia vipodozi na dawa za miti shamba ambazo hazijafanyiwa uchunguzi wala hazina alama za ithibati ya matumizi ya Mamlaka zinazohusika kama vile Bodi ya Dawa na Chakula, Baraza la Tiba Asili na Mkemia Mkuu wa Serikali. Matumzi ya dawa hizo yana athari kubwa kwa afya ya mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wakunga na Wauguzi ni miongoni mwa vyombo muhimu katika kusimamia usajili na mwenendo wa kazi za Wakunga na Wauguzi. Kamati imeonesha kwenye ripoti jinsi gani Baraza hili linavyofanyakazi zake kwa weledi licha ya kuanza na changamoto mbali mbali kama vile uhaba wa fedha na vitendea kazi kama vile usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, Wauguzi na Wakunga wanafanyakazi ngumu na katika mazingira magumu, Kamati yangu inashauri Serikali kuwazingatia katika maslahi yao kwa kuwapatia posho za mazingira magumu, posho za zamu za usiku, posho la sare na kuimarisha uwezo wao kwa kufanyakazi kwa kuwapatia fursa za elimu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali Binafasi zimekuwa na changamoto kubwa katika kuunga mkono sera ya Serikali ya kuimarisha huduma za afya kupitia sekta binafsi. Hospitali binafsi ambazo kamati imepata wasaa wa kuzitembelea ni pamoja na Ataskhtaa (*Global*), Hospitali ya Mina, Hospitali ya Machui na Vituo vya Afya vya *Dira Cooperative* ya Chake Chake. Kamati inapongeza sana Sera ya Serikali yetu Mapinduzi ya Zanzibar ya kufungua milango kwa sekta binafsi kutoa mchango wao kwa upande wa afya na kuipunguzia mzigo Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la msingi kamati inalisisitiza ni kuzifanyia unafuu wa kodi Hospitali binafsi kwa vile ingawa wanapata malipo lakini lengo kubwa ni kutoa huduma kwa wananchi na siyo kufanya biashara. Hili tunaomba kusisitiza sana kwamba hospitali binafsi zaidi zijikite katika suala zima la kutoa huduma kwa wananchi, suala la biashara iwe ni sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeshauri katika ripoti kwamba hospitali binafsi zisitozwe kodi kubwa kama zinavyotozwa taasisi nyengine za biashara. Kamati inasisitiza tena Wizara ya Afya kukaa pamoja na Wizara ya Fedha kuona namna gani wanaweza kusawazisha changamoto hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeshauri Bodi ya Hospitali binafsi kupitia upya viwango vya leseni za malipo ya mwaka kuweka daraja maalumu kulingana na hali na hadhi ya Hospitali husika badala ya utaratibu wa sasa wa kuweka viwango sawa kwa Hospitali zote. Huwezi kuchukua hospitali ya binafsi ya *Global* ukai-*charge* kodi ya mwaka ya laki mbili, ukalingalisha na Hospitali ya Asaakheri ambayo kwa kweli ndi ndogo mno. Lazima tuweke category tofauti katika leseni zao.

TAASISI YA HOSPITALI YA MNAZIMMOJA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inatambua jitihada kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali katika Kuimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali Mnazimmoja, Mwembeladu na Kidongo Chekundu. Changamoto kubwa ni bajeti ambayo inayotolewa ukilinganisha na kuongezeka mahitaji ya huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, bado changamoto zipo katika Hospitali ya Mnazimmoja hasa katika utendaji wa kazi ambako ndiyo kimbilio la wanachi wetu wengi kama ripoti yetu inavyoeleza kwa undani. Aidha, Hospitali Mwembeladu licha kuimarisha huduma zake zipo changamto za uhaba wa fedha na ufinyu wa jengo katika wodi ya akinamama. Kamati imependekeza bajeti iongezwe na maslahi ya watendaji yaimarishwe hasa kwa kuzingatia kwamba hiyo ndio hospitali yetu kubwa ya wazazi na kongwe ukiacha Mnazimmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kero ya kituo cha daladala kilichopo mbele ya mlango wa mkubwa wa Hospitali ya Mwembeladu, Kamati imeshauri hatua za dharura na za haraka zichukuliwe za kukiondoa kituo hicho, na tunaiomba Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ, kupitia Baraza lake la Manispaa, kuchukua hatua za haraka ya kukihamisha kituo hicho na kukihamishia mahala pengine. Tatizo kubwa kwamba pale ndio mlango mkubwa na *umberlance* ndio zinapotoka kukimbia Mnazimmoja. Sasa utakuta pana tatizo la daladala pale muda wote.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kutambua umuhimu wa huduma ya usafiri lakini vile vile tunatambuwa umuhimu wa maisha na afya ya mama wajawazito wanaowahishwa kujifungua au kupatiwa rufaa katika Hospitali ya Mnazimmoja, na ambao wanakuwa katika hali ya hatarishi kuwahishwa kutokana na msongamano wa gari za abira mbele ya mlango wa Hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya Hospitali ya Kidongo Chekundu tumeielezea kwa kirefu katika Hotuba ya Kamati yetu katika Mkutano wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati inatambua hatua na mipango kabambe ya Serikali kuimarisha Hospitali ile kupitia ufadhili wa Kuwait, hata hivyo, Kamati inakumbusha kuwa wakati tukisubiri ufadhili huo, hatua za dharira hapana budi zichukuliwe kutatua changamoto zilizopo hasa usafi, wafanyakazi na fedha za kuendesha kazi za kila siku kama vitendea kazi na chakula na hasa ukuta wa Hospitali ya Kidogochekundu. Kwa kweli ukuta ule ni mbovu na majambazi yanabirukia ukuta ule kwenda kutoa hujuma kwa wagonjwa wa akili akinamama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi nimeona nayaeleze hayo kwa upande wa Wizara ya Afya, lakini haina maana kwamba Kamati imeyaona hayo tu, mambo mengi tumeyaweka kwenye ripoti

hivyo nawaomba sana waheshimiwa wajumbe watapochangia waisome kwa kina ripoti ya Kamati ambayo imeweka kwa kirefu maeneo karibu yote tuliyofanya kazi na Kamati.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Kamati imefanyakazi ya kusimamia utekelezaji wa kazi na majukumu ya Wizara ambayo utekelezaji wake umewekwa katika programu Kuu sita. Programu hizo ni Maandalizi na Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu ya Juu, Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali, Elimu bora na programu ya Utawala Uongozi na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba pia hapa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa muono wake mkubwa na maelekezo yake kwa upande wa Sekta ya Elimu hasa suala zima la kuondoa michango kwa wananfunzi wetu wa Shule za msingi na sekondari. Tunampongeza kwa kuendeleza suala zima la mnyonge kupata elimu bila ya malipo nchini mwetu.

PROGRAMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Mwenyekiti Kamati ya Ustawi wa Jamii imepata fursa ya kuona kazi ya kuandaa vijana wetu kuanzia maandalizi na Msingi. Kamati imeona changamoto kubwa katika maandalizi ni wingi wa wanafunzi katika madarasa na uchache wa walimu. Hali hii inapelekea walimu kushindwa kumudu kuwaandaa vizuri wanafunzi, kinyume na Skuli binafsi ambazo Kamati ilipata fursa kuona mingoni mwa Skuli binafsi zikuwa na wanafunzi wachache wa maandalizi katika darasa ambao mwalimu anamudu kumshughulikia kila mwanafunzi kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeshauri katika ripoti yetu kuwa Serikali iweke mkakati maalum wa kuimarisha skuli za maandalizi na msingi kwa kujenga madarasa ya kutosha na walimu, na kusaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani. Sote tunafahamu kwamba elimu ya maandalizi ni muhimu kwa kuwa ndipo mwanafunzi anapoanza alifu kwa ujiti mpaka anajua kusoma, kuandika na kuhesabu kabla ya kuendelea katika madarasa ya msingi na sekondari. Mwalimu wa hapa anahitaji kuwa mstahmilivu na muadilifu, kwa hivyo tunawapongeza sana walimu wanaojitolea kwa kweli kufanya kazi katika skuli hizi za chekechea msingi na sekondari.

PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, imeonesha hatua tuliyofikia katika elimu ya Sekondari ya kawaida na Sekondari ya Juu. Wajumbe mtaona kwenye ripoti tumeainisha changamoto ya matokeo yasiyoridhisha ya mitihani ya kidato cha nne na kidato cha sita. Matokeo siyo mabaya lakini bado hayaridhishi tunahitaji kuongeza juhudi ili tupate viwango vya juu vya ufaulu. Kwa miaka mingi Skuli zetu zinashika namba za chini kwenye jumla ya Skuli zinazofanya mitihani ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, tunaeleza kwa nia njema kabisa kwa kwamba elimu siyo jambo la mzaha, ndiyo roho ya nchi, ndipo tunapotegemea kupata wataalamu mbali mbali katika nchi yetu, lazima tuengeze juhudi za kweli kuhakikisha tunafanikiwa lengo hilo. Ripoti yetu imeelezea sababu

mbali mbali zinazopelekea skuli zetu kutopata matokeo yasiyoridhisha na Kamati imetoa ushauri na maoni yake ya nini kifanyike ili kutatua changamoto hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imetembelea skuli mbali mbali za msingi na Sekondari Unguja na Pemba, kama ripoti inavyoeleza, tumeona mambo mengi sana ambayo kweli yasiporekebishwa hatutaweza kupata matokeo mazuri. Kuna uhaba wa walimu hasa wa masomo ya Sayansi, ipo Skuli tumeikuta wanafunzi hawana mwalimu wa somo ambalo wanategemea kulifanyia mtihani wa taifa. Kuna tatizo la uhaba wa vifaa vya maabara ambavyo wanafunzi wanapatiwa vifaa hivyo muda mfupi kabla ya kufanya mitihani ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upekee kabisa nimeona nieleze tatizo la ukosefu wa dakhalia hasa kwa wanafunzi wa kike, Kamati imetembelea skuli ya wasichana ya Ben Bella tumeona watoto wa kike wakiwa na ari kubwa ya kusoma na kujiendeleza ili kutimiza ndoto zao katika maisha. Tatizo kubwa mazingira ya kusoma, wanafunzi wengi wanaishi mbali sana na mji na wanalazimika kusafiri masafa marefu kuifuata Skuli. Kamati imekuta baadhi ya wanafunzi wanatoka Mkokotoni wanakuja mjini kila siku kufata Skuli, hayo siyo mazingira mazuri ya kusoma hasa kwa mtoto wa kike.

Mhe. Mwenyekiti, tunaishauri Serikali ifanye juhudi na mikakati ya makusudi kurejesha dakhalia katika Skuli zetu ili kuwawezesha wanafunzi wetu kusoma katika mazingira ya utulivu. Aidha, Serikali iongeze fedha za bajeti katika elimu na kutoa kilichokubaliwa kwa wakati katika bajeti kwani kuwekeza zaidi katika elimu hupotezi bali unajenga zaidi.

PROGRAMU YA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu imepiga hatua katika maendeleo ya elimu juu kwa hasa baada ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), tunapongeza sana tunampongeza Mhe. *Chancellor* wetu ambaye ndio Rais wa Zanzibar kwa kukiongeza vyema chuo kile, vile vile Chuo Kikuu cha Al-Sumait cha Chukwani, Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu na Chuo Kikuu Huria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hizi ni hatua kubwa katika maendeleo ya elimu ya juu kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Kamati imeonesha mafanikio tuliyopata SUZA lakini changamoto kubwa ni ukosefu wa bajeti ya fedha za maendeleo, tunaiomba sana Serikali yetu ilichukuwe na katika mwaka wa fedha ujao iweze kulitanzua. Kamati itapenda kuona Serikali imezingatia kuweka kasma ya fedha za maendeleo kwa SUZA hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa SUZA imeongezewa taasisi nyengine chini yake kama vile Chuo cha Sayansi ya Afya, Chuo cha Utalii na Taasisi ya Usimamizi wa Fedha ya Chwaka.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti yetu tumegusia kwa masikitiko hali ya Chuo cha Kiislamu cha Micheweni Pemba, ambacho kwanza kipo katika hali mbaya ya majengo yake yote kuvujiwa, tumetowa mapendekezo ya hatua kuchukuliwa kurekebisha hali hiyo. Lakini kubwa zaidi ni mgogoro baina ya baadhi ya wanajamii wa Micheweni kilipo chuo hicho na Chuo kukataa ujenzi wa ukuta wa uzio wa chuo hali inayopelekea eneo la chuo kuwa wazi na kusababisha uharibifu wa mali za chuo. Tunaiomba Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kuharakisha kumaliza

mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo ili ukuta wa uzio wa chuo hicho umalizwe na shughuli ziendelee.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Sayansi ya Karume ni miongoni mwa vyuo muhimu katika kutayarisha wataalamu wetu wenyewe wa fani za sayansi. Kamati ya Ustawi wa Jamii inaiopongeza sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa jengo jipya la Chuo ambalo litakuwa na madarasa, Karakana, ofisi n.k, ujenzi ambao unaendele vizuri hivi sasa. Changamoto kubwa ambayo Kamati imeona ni ukosefu wa fedha za ruzuku kwa ajili ya kukamilisha mipango mbali mbali ya Chuo kama vile kuanzisha masomo ya ngazi ya shahada, kufanya utafiti na kusomesha walimu wake katika ngazi za juu.

Mhe. Mwenyekiti, hiki ndiyo chuo pekee Zanzibar kinachotoa fani za ufundi na uhandisi katika kiwango cha juu kinachoshindana vizuri katika soko la ajira. Wataalamu wengi wa fani za uhandisi na umakenika wamepatikana hapo, wanafunzi wetu wanaozalishwa hapo wanaweza kushindana sawa na wenzao wa maeneo mengine ikiwemo Tanzania bara katika soko la ajira. Kamati yetu inaiomba sana Serikail kukipatia ruzuku chuo hicho ili kikamilishe mipango yake tuliyoitaja hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, Tumekumbana pale na tatizo la muda mrefu suala la umeme kati ya chuo pamoja na ZECO mgogoro huu umekuwa wa muda mrefu na kwa kweli mpaka leo haujaweza kutanzuliwa tunaiomba sana serikali lingilie kati suala hili kati ya ZECO na Chuo cha Ufundi Mbweni. Tunawapongeza sana Mbweni wamepunguza wao matumizi ya mradi kwa kuanzisha maradi wao wa *solar* lakini sasa inaelekea bado kuna mgogoro suala la umeme, malipo ya umeme kati ya Chuo na ZECO.

PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa sana na maendeleo ya programu hii, ni moja ya maeneo ambayo Wizara na Serikali kwa ujumla inafanya kazi vizuri na kwa kweli tunawapongeza sana. Kamati imetembelea vituo vya Mafunzo ya Amali vya Mkokotoni na Vitongoji na kuona kazi kubwa na nzuri inayofanywa na walimu kuwapa ujuzi wa vitendo vijana wetu katika fani mbali mbali ambao wakitoka hapo wanaweza kujiajiri wenyewe au kushindana vizuri katika soko la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imetembelea vituo vya elimu mbadala na watu wazima vya Forodhani na Rahaleo na kuona kazi kubwa inayofanywa na kuwapatia ujuzi vijana wetu pamoja na kuwarejesha wale ambao waliacha masomo kwa sababu mbali mbali. Kwa kweli kazi inayofanyika ni kubwa na ngumu, Kamati yangu inashauri sana Maslahi ya walimu wa vituo hivi yaimarishwe kwa kuwa kazi wanayofanya ni ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi na mafanikio yanayopatikana katika programu hii kuna changamoto kadhaa ambazo tumeziweka kwa kirefu katika ripoti ya Kamati. Hata hivyo, Kamati imeona kuwa tatizo linalokwamisha utatuzi wa changamoto hizo ni upatikanaji wa fedha. Na hili siyo tatizo la kuwa fedha hizo hazipo, fedha za kuviendeleza vituo vya elimu mbadala na mafunzo ya amali zipo, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mtakumbuka kwa Baraza hili limepitisha sheria ya makusanyo ya *"fedha za maendeleo ya ukuzaji ujuzi*", yaani

Skills Development Levy (SDL) ambazo wanakatwa waajiri katika na wachangiaji wakubwa ni sekta binafsi. Fedha hizi zinatakiwa kupatiwa vituo hivi lakini tokea sheria hiyo ilipotungwa fedha hizo hazijawahi kupatikana hata mara moja na badala yake fedha hizo zinaelekezwa katika mfuko wa hazina kwa matumizi mengine. Kamati yangu inaomba sana inasisitiza kwamba sheria ifuatwe kwa kuhakikisha kuwa fedha hizo zinapelekwa katika vyuo hivyo ili kutatuwa changamoto zao. Kamati yangu imeona kwamba endapo fedha hizo zingekuwa zinapelekwa kama inavyostahiki basi vituo hivyo vingekuwa vinaweza kujiendesha katika kazi zake mbali mbali bila kutegemea nguvu nyengine za kifedha za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tumetaja katika ripoti yetu kuhusu changamoto ya ukosefu wa uzio katika dakhalia za wanafunzi wanawake wa Kituo cha Amali Vitongoji ambazo zipo karibu na dakhalia za wanafunzi wa kike wa Skuli ya Fidel Castro. Kutoka na kutokuwepo uzio wanafunzi wa kike wanapata usumbufu wa kuvamiwa nyakati za usiku na wahalifu, Kamati imesikitishwa na kulaani vitendo hivyo vya kihalifu dhidi ya wanafunzi na kubwa tunaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya kila inaloweza kuhakikisha eneo hilo linajengwa uzio na Serikali iongeze nguvu kutafuta fedha kwa njia mbali mbali ikiwepo kupitia miradi ya wafadhili ili vijana wetu hao wasome bila ya usumbufu.

PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojuwa ni muhimu kupima uwezo wa wanafunzi wetu katika kujuwa maendeleo yao. Baraza la Mitihani limekuwa likifanyakazi yake vizuri isipokuwa Kamati imeona kucheleweshwa fedha kunarudisha nyuma mipango yao hasa ratiba ya mtihani, hivyo Kamati imeshauri Baraza la Mitihani lipatiwe fedha kwa wakati kwa kuwa kazi zake zinategemea sana ratiba na muda wa kuandaa mitihani ya ndani ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, ubora wa elimu unategemea mambo mbali mbali ikiwemo ubora wa walimu wenyewe. Kamati imeona juhudi za Serikali za kuimarisha uwezo wa walimu wetu kupitia Vituo vya Walimu (TCs), vituo hivi vinafanyakazi vizuri, na tunawapongeza sana washauri wa vituo hivyo kamati imetembelea baadhi ya vituo hivyo kama vile Kituo cha Walimu Mkwajuni, Kituo cha Walimu Dunga na Kituo cha Walimu Kiembe Samaki na tunategemea kutembelea vituo vya walimu kwa upande wa Pemba. Kamati imeona kuwa vituo hivi havifikishiwi fedha za matumizi mengineyo yaani (O/C), badala yake vituo vinategemea fedha za miradi yake ya ndani, michango ya walimu na wanafunzi ambayo nayo imepungua baada ya kufutwa kwa michango katika shule za msingi. Kamati inashauri kuwa Wizara ifanye juhudi za makusudi kufikisha fedha za O/Cs kwa vituo hivyo vya walimu ili viweze kuwanoa walimu wetu kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine kubwa kwa vituo vya walimu ni ukosefu wa usafiri, vituo hivi vinahitaji kupatiwa usafiri wa uhakika kwa kuwa kazi zao nyingi ni za kufatilia walimu katika Skuli mbali mbali na nyengine zipo maeneo ambayo hakuna usafiri wa umma, Kamati inasisitiza sana Wizara kuwasaidia washauri wa vituo hivi wafanye kazi zao katika mazingira yasiyo na changamoto zinazoweza kuepukika.

Mhe. Mwenyekiti, Maktaba ni moja ya Taasisi muhimu katika maendeleo ya nchi kielimu. Kamati yetu imepata fursa ya kutembelea Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar na wanafanyakazi zao vizuri tunawapongeza sana. Kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa maji

safi katika Maktaba kuu yetu ya Zanzibar, ingawa wamechimba kisima lakini maji yaliyopatikana yana chumvi nyingi, hivyo wanalazimika kununuwa maji na huku wakiwa na uhaba wa fedha. Kamati inashauri kwa Wizara pia ishirikiane na ZAWA kuona namna gani maji safi yanaweza kufika Maktaba Kuu, kwa kuwa eneo hilo linatumiwa na watu wengi na huduma ya maji ni lazima.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeona changamoto ya wizi wa vitabu katika Maktaba kuu yetu, lakini kilichotusikitisha ni kuwa uongozi wa Maktaba unachukuwa hatua ya kuwa kamata wahalifu na kuwapeleka Polisi wakiwa na vielelezo kamili lakini wahalifu hao wakifika Polisi wanaachiwa. Kamati imepata taarifa kuwa kuna mwizi maarufu wa vitabu ambaye anatoka Tanzania bara amekamatwa na vitabu akiwa njiani kuvisafirisha, hata hivyo mwizi huyo baada ya kukamatwa Polisi wamemwachia kwa dhamana na kukimbia. Mbaya zaidi mwizi huyo huyo amekamwata tena katika Maktaba ya Chuo cha Kikuu cha Elimu Chukwani lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na Polisi.

Mhe. Mwenyekiti, wapo baadhi ya wafanyabiashara wa maduka ya vitabu wamekamatwa wakiuza vitabu vyenye nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambavyo haviuzwi. Lakini wanapokamatwa na Polisi baadae waachiwa kuambiwa kwamba hawana hatia.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hizi zimeisikitisha sana Kamati yetu kuona kuwa wenzetu wanafanya juhudi za kupambana na wahalifu halafu jeshi la Polisi halitowi ushirikiano kama inavyopasa. Kamti yangu imeshauri Serikali kupitia Ofisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kukaa na jeshi la Polisi kuelekezana taratibu na hatua thabiti za kuchukuwa pale ambapo wizi wa vitabu vya Serikali wanapokamatwa. Kamati pia inashauri Maktaba iongezewe kamera za ulinzi yaani (CCTV) kwani zilizopo ni chache.

Mhe. Mwenyekiti, Maktaba haina usafiri nyenzo za usafiri na kwa upande wa Pemba Kamati inataarifa kuwa hakuna kompyuta hata moja licha ya kuwa ana chumba na jengo jipya. Kamati imeshauri kwenye ripoti kumaliza changamoto hizi ndogo na zipo kwenye uwezo wa Serikali kuzitatuwa.

PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati inaridhika na kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali licha ya changamoto nyingi zinazokabili. Kamati inatambuwa kuwa tatizo kubwa na upatikanaji wa fedha lakini hata hivyo, tunaiomba na kuishauri Serikali kuzingatia sana kuipatia Wizara ya Elimu fedha kama si za kutosha basi angalau ile kasma wanayopangiwa kwenye bajeti ingekuwa inapatikana kikamilifu, ili waweza kusukuma mbele kazi na mipango mingi ya kibajeti waliojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza hatua ya Wizara ya kujenga Skuli mpya za Sekondari za kisasa katika Wilaya mbali mbali, hata hivyo, bado maeneo mengine ujenzi wake unasuasua. Kamati imeona Maendeleo ya Ujenzi wa Skuli ya Kibuteni hayaridhishi na ujenzi huo ulianza sambamba na ujenzi wa Skuli ya Mkanyageni Pemba ambayo imeshamaliza na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein ameshaifungua katika sherehe zetu za Mapinduzi zilizopita, lakini bado ujenzi wa Skuli ya

Kibuteni umelala. Kamati imetembelea tena kabla ya kuwasilisha ripoti hii na imekuta hakuna shughuli yoyote inayotendelea ya ujenzi. Kamati inashauri Wizara kuchukuwa hatua madhubuti kukamilisha ujenzi huo kama mjenzi yule ameshindwa kazi basi tuvunje mkataba tutafute mwengine kazi iendelee.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo kamati pia imekwenda kuona maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Amali, Makunduchi kabla ya kuwasilisha ripoti hii. Ujenzi huo upo katika hatua ya kufukiwa msingi na kamati inataarifa kuwa ulichelewa kidogo nje ya wakati uliopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imepata wasiwasi kutokana maelezo ya mkandarasi kuwa ujenzi huo unaweza kuchelewa tena hivi sasa baada ya kutokea upungufu wa mchanga wa ujenzi nchini mwetu. Kamati inaiomba Serikai kuzingatia hatua yake ya kudhibiti uchimbaji wa mchanga usiathiri miradi ya maendeleo ya ujenzi wa miradi ya Serikali ambayo kwa mujibu wa mikataba ya ujenzi inatakiwa kumalizika kwa wakati.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, namalizia muhutasari huu wa ripoti yetu kwa kuwaomba wajumbe wako waisome kikamilifu ripoti ya Kamati kwa vile mambo mengi ya msingi katika sekta ya elimu na afya yanawagusa moja kwa moja katika majimbo yao ya uwakilishi. Kamati yangu kila ilipopita imepata salamu kutoka kwa wahusika na wananchi na sisi tumeahidi kuzifikisha salamu hizo kwa Wawakilishi wao, na nachukuwa fursa hii kufikisha salamu hizo kwa kuwataka Wajumbe wasome ripoti na wajuwe changamoto zinazokabili sekta ya afya na elimu katika majimbo yao, ili wasaidiane na Serikali katika kuzitatua.

Mhe. Mwenyekiti, nimetoa maelezo ya muhutasari wa ripoti kwa kuanisha maeneo muhimu kwa kila sekta, hivyo nawaomba wajumbe watakapochangia wajielekeze zaidi katika ripoti ya Kamati ambayo imekusanya mambo mengi ambayo siyo yote nimeyaeleza katika muhutasiri huu.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kuwashukuru waheshimiwa wajumbe wa Kamati kwa kunipa fursa ya kuwasilisha muhtasari huu kwa niaba yao, aidha niwashukuru tena makatibu wetu kwa kutushauri na kuratibu kazi zetu mpaka hatua hii ya kuwasilisha ripoti na muhutasiri wake mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwashukuru Watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wakiongozwa na Katibu Mkuu Mwalimu Bi. Khadija Bakari Juma, na Naibu Katibu Mkuu wake Mwalimu Bi. Madina Mjaka Mwinyi, Wakurugenzi wao, Wakuu wa Taasisi mbali mbali, walimu na watendaji wa wizara Unguja na Pemba. Kwa mashirikiano yao na kamati wakati wote, licha ya kuwa na majukumu ya kiwizara waliweza kuhakikisha tunafanyakazi pamoja mpaka tukakamilisha majukumu tuliyopangiwa. Tunawashukuru sana, sana, kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika naomba kwa dhati kabisa kuwashukuru watendaji wa Wizara ya Afya, wakiongozwa na Katibu Mkuu wao aliyepita Dkt. Juma Malik Akil na Naibu Katibu Mkuu wake Bi. Halima Maulid Salum, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi mbali mbali, Madaktari, Wauguzi na watoa huduma wote wa Wizara ya Afya ambao tumeshirikiana bega kwa bega na kamati katika ufanikisha kazi yetu pamoja na ripoti hii. Nia yetu ni kushirikiana pamoja ili

kuisaidia serikali yetu kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa wananchi wake. Tunawashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nitumie nafasi hii ya kumalizia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, ndugu Asha Abdalla kwa kuteuliwa kwake. Hili ni jembe na jembe linalima popote ni mategemeo yetu kuwa wataendelea zaidi mashirikiano baina ya wizara na kamati.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naishukuru Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Katibu wa Baraza na Watendaji wake kwa kufanikisha kazi za kamati, kupiga chapa Ripoti ya Kamati na hatimaye kufanikisha ripoti hii iliyoniwezesha mimi kuiwasilishwa leo hii mbele ya Baraza hili la Wawakilishi, wote tunasema ahsanteni sana.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena wewe, Waheshimiwa Wajumbe kwa usikilizaji wao makini sana na nasema ahsanteni sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwakumbushe kitu kimoja, dakika zetu ni 15 nawaomba sana wajumbe mwende kwenye hoja na mchangie zile *point* ambazo mnahisi mtazichangia kuliko maelezo mengi ya kapoteza muda na mkaona muda wenu kama umebanwa. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe twende kwa utaratibu huo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuichangia Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelekezo yako mazuri lakini natoa pongezi kwa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa hospitali yetu ya Mkoani ambayo kwa kweli ni kioo cha jamii kuiona kwamba serikali ya awamu hii imefanya jambo moja kubwa sana kule Pemba. Mheshimiwa nimeisoma sana hii ripoti nataka niwashukuru wana kamati kwamba kwa kweli wamejitahidi kufafanua kwa kila hali, hali halisi ya maelekezo yaliyotoka Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza na Wizara ya Afya kwa maelekezo kidogo ambayo nahisi tu kwamba yatakuwa kama ni maoni au ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Abdalla Mzee katika ripoti yake niliyoisoma ni kwamba inakabiliwa na tatizo la umeme. Mheshimiwa nataka tuchukue hadhari hospitali ile imegharimu pesa nyingi sana, lakini tuhakikishe mambo madogo madogo tukiyaacha ndio yataweza kutuharibia. Mimi sijafahamu hasa tatizo la umeme lakini kama ni *transformer* ambalo linaikabili pale basi serikali haraka iwezekanavyo na Wizara ya Afya jambo lile liondoke kwa kuzinusuru mashine zetu mpya na za kisasa zilizopo pale. Kwa hivyo, nilikuwa natilia mkazo kwamba kitu cha shilingi 50,000,000 kisije kikatuharibia vitu vya mabilioni. Mheshimiwa hilo nilikuwa na mimi nachangia ile hali halisi ya nini kifanyike.

Mhe. Mwenyekiti, lakini humu katika ripoti kitu kimoja sikukiona ambacho Mhe. Waziri wakati anatoa hoja zake sana kipindi cha nyumba, wakati wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoani alituahidi

sana kwamba pale atachukua wafanyakazi wa hospitali ile karibu 400. Sikupata ripoti kwamba wale watu wameajiriwa au hawakuajiriwa na hospitali imeshaaza kazi. Lakini pia alituahidi sana Mhe. Waziri kwamba watu wengi watakuwa wanatoka maeneo ya Mkoani kwa wale wafanyakazi wa sekta ya pale pale ambao wafaidike na eneo lile. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atapokuja ana uwezo tu kidogo wa kuweza kuiweka sawa kama pindipo ataona lina haja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika Hospitali ya Chake-Chake. Mhe. Mwenyekiti, hospitali hii ndio nilisema namshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein kwani tayari mji ule umeshakuwa mji mkuu katika miji mikuu ya Zanzibar ni miwili iliyoteuliwa mmoja ni huo uliopo Zanzibar na mmoja ule wa Chake-Chake. Mheshimiwa Hospitali ya Chake-Chake ni hospitali kama wanavyozungumza inabeba watu wengi sana na ishakuwa hospitali ya mjini, sasa ningeomba waziri aiboreshe hii hospitali kwa maoni ya kamati hospitali inavuja, hospitali ina matatizo ya maji, hospitali ina matatizo ya vitendea kazi lakini pia ina matatizo ya madereva. Mheshimiwa mji ni mji mtu yeyote anayefika pahala anafikia Mjini na sisi mheshimiwa mara nyingi hata mtu wewe ukigongewa mlango jambo la kwanza unanawa uso ndio tena baadae ukaja kukoga kwanza unakwenda kumsikiliza mtu. Kwa hiyo, Mji wa Chake-Chake kwa hadhi uliyokwishapandisha Wizara ya Afya Hospitali ya Chake-Chake ni kuitizama kwa jicho la huruma na jicho la pekee na kuangalia kwamba pale patakuwa na wageni wakifikwa na tatizo wataweza kufika pale.

Kwa hivyo, ningeshauri sana vifaa, pia ningeshauri tukaijengea vyumba ambavyo watu wanaweza wakakodi kwa sababu ni hospitali ya Mjini anaweza kuja mtu na pesa zake anataka matibabu lakini kwa kwenda ile tupate sote mheshimiwa haridhiki inabidi akodi ndege, akodi nini kwa tatizo dogo la vyumba. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba hospitali hii kwa sababu iko mjini pale ijengewe vyumba vya kuweza kukodi kwa wale wanaotaka kukodi ili mtu ajihisi kama kapata afya hasa kwa wageni. Mheshimiwa hilo nilikuwa naliomba kwa Wizara ya Afya walitizame kwa jicho kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya ina matatizo mengi ambayo yanasemekana kama kuchanganywa wagonjwa. Mheshimiwa wizara ijitahidi kwani afya ni kitu cha peke yake una mzaa mtoto akiwa salama, unamchanganya na mtu wa TB unamchanganyia TB. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana wizara ikajitahidi sana najua inafanya kazi kweli kweli lakini hii nampa pongezi Waziri wa Afya lakini nampa pole kwa sababu hili neno la ustawi wa jamii kama lilivyowekwa humu la Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ndio maisha yetu ya kila siku. Mheshimiwa Waziri wa Afya wewe una jukumu kubwa sana la wananchi wako hawa ambao kwa kweli tunakutegemea maana yake mtu analala mzima asubuhi anaamka mbovu, lakini wewe ndiye kioo chetu cha kututibu baada ya rehema za Mwenyezi Mungu tunakutegemea wewe. Mheshimiwa jikaze sana hali kama unavyoiona.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu hali halisi ya watu wetu ambao hawana uaminifu, unamsomesha ushatumia gharama, umeshamfikisha pahala aje akusaidie au aje atusaidie mtu yule anachukua maslahi yake anaondoka. Mheshimiwa ningekushauri sana sasa hivi ukifanya mambo yako ya kwenda kuwasomesha watu ufanye mchujo, uwe na watu maalum na mikataba. Lakini ningekushauri kwa sababu serikali yetu ni moja mheshimiwa nchi nyengine nyingi asilimia karibu 30 au 50 watu wengi wanapitia jeshini ndio wanafanya kazi. Mheshimiwa ningekushauri vikosi vyetu tunavyo, vikosi vyetu tunavyo kwa maana tatu. Mheshimiwa ukiona

kuna haja ya vitu maalum wale wana mikataba uchukue vikosi vyetu ukawasomeshe ili mtu yule asikukimbie mwanajeshi hakimbii, lakini hawa watu wa kawaida wanafata maslahi yao. Kwa hivyo, mimi ningekushauri ukiona kuna haja chomoa mtu kwenye kikosi naamini utapewa aje atusomeshee ili afanye kazi kwa wananchi, kazi anayoifanya jeshini na kazi atakayoifanya hapo kwa wananchi kazi ni ile ile.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nimeona tuna matatizo sana ya madaktari, sifikirii kama mheshimiwa vikosi vyetu vile havina madaktari. Kwa hivyo, tumuombe waziri achukue madaktari kidogo ni ile ile akusaidie wewe, madaktari wanao hawa na watakusaidia sana. Kwa hiyo, muombe waziri anayehusika nipe hawa watu wako kazi ni ile ile ya kuitumikia serikali hii. Mheshimiwa ningekushauri hilo ili tuweze kuziba ufa katika masuala ambayo yana majukumu makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumze kitu ambacho kinanipa faraja, kwa kweli suala la afya nimeliangalia kwa mtazamo mkubwa nikalinganisha na nchi za wenzetu. Mheshimiwa huko juu kweli kweli Zanzibar katika hali yoyote unayoiona basi bado Serikali ya Zanzibar kwa kweli inawathamini watu wake sana, maana yake nchi nyingi bure ni bure lakini Zanzibar bure yake basi ni bure ambayo ina tija kweli kweli. Kwa hiyo, mheshimiwa nakushukuru unafanya kazi kubwa sana lakini jitahidi sana na madaktari unaowaona si waaminifu wasikuvunjie hadhi kazi ni moja tu, ni kuhakikisha kwamba hatuna ulazima wa mtu huyo ukimuona hatufai wewe maliza kazi wengine wapo wanasubiri. Mhe. Mwenyekiti, kwa hapo ningeona kwamba wizara yako ina umuhimu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye Wizara ya Elimu. Mhe. Waziri wa Elimu ni kweli ni mtu mmoja makini sana na tathmini tuliyoifanya tulipompitishia bajeti yake hatukumpiga ngwara hata moja, tulimuachia aende akafanye kazi. Mheshimiwa bado una wizara ngumu na wizara yako mimi maana yake nikikwambia ni wizara nzito sana, kwa sababu mheshimiwa nataka nikwambie hapa wizara yako ni wizara yenye wapinzani wengi sana. Siasa, mambo mengi yanaanzishwa kwenye mashule, walimu na kila haja ambayo unaiona basi wewe unapigwa vita. Mheshimiwa mimi nataka nikwambie tu kwamba skuli za serikali zinauliwa makusudi na walimu wako kwa kutokusomesha watu na kufanywa kwamba zile ni skuli ambazo hazina radhi.

Kwa hivyo, mheshimiwa nataka ulijue hilo kwamba skuli zako za serikali zinahujumiwa makusudi na walimu na ndio ukaona matokeo mabovu ya wanafunzi ni kwamba zinahujumiwa. Mwalimu yule yule akitoka pale akachukuliwa katika skuli ambayo ni ya *private* utasikia mwalimu mzuri, lakini mwalimu yule yule akisomesha skuli hizi basi wanafunzi hawapasi. Hakuna mabadiliko mheshimiwa, mabadiliko ya elimu ni yale yale tatizo ni *sabotage* ambayo unafanyiwa. Kwa hivyo, mheshimiwa wewe nakuaminia nataka ufanye *research* kazi yoyote utakayoifanya, mambo yoyote utakayoyafanya kufeli kwa wanafunzi sisi hatuko kwelini, utaonekana tu kwamba wewe huna maana lakini chamsingi chukua hatua skuli zote zilizofanya vibaya basi nenda ukatizame ubaya wake umefanyika vipi. Takwimu zilizomo humu mheshimiwa mimi sizikubali sana zaidi ya maelekezo ninayokwambia kwamba tatizo walimu mheshimiwa hawataki kusomesha wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mwalimu Mkuu wa Skuli iliyofanya vibaya awajibike na walimu wengine ambao unaona kama hawana maana na hawana shida ya kazi maana yake wengine wako kwenye

siasa tu, mheshimiwa lichukulie hatua kwa sababu litakupeleka pahala ambapo watu wanakufikiria vibaya kila siku wanailalamikia Wizara ya Elimu, mara wanafunzi hawafanyi hivi lakini si kweli Wizara ya Elimu inafanya kazi vizuri lakini kuna watu wachache wanairudisha nyuma. Mheshimiwa nakuomba sana kwa hili ulichukulie hatua, na pia nakuomba hii mitihani yetu ya darasa la kumi inayofanywa jitahidi sana basi matokeo yake yaje kwa wakati, maana yake unawapa watu usumbufu wa kuwajua watoto wao kama wamepasi au hawajapasi na muda wa skuli inakuwa zimeshafunguliwa. Ningekushauri kabla ya Disemba au mwisho wa Disemba kabla skuli hazijafunguliwa matokeo haya yakatoka ili watu wakaweza kujipanga kwa mambo mengine ambayo yapo.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningemshauri Mhe. Waziri atoe motisha kwa skuli ambazo zitafanya vizuri katika wanafunzi wake, wale wanafunzi ambazo skuli zao zitafanya vizuri katika matokeo basi zitaje kuzipa viwango lakini pia uzipe motisha katika mambo ambayo yapo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine fanya mageuzi ya walimu, mwalimu akishazoea sana pahala anakuwa hafanyi kazi, fanya mageuzi ilimradi zile shule ziwe zinakwenda katika maelekezo ya upya, kitu chochote ukikipeleka pahala mheshimiwa kinafanya kazi kuliko wafanyakazi wale wameshazoea. Mwalimu ana miaka 20 pahala basi anafanya kazi nyumbani tu hata kwenda huko skuli haendi tena. Kwa hivyo, ningekushauri sana hilo suala ukalifanya kidogo kuliangalia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme mfumo wa sayansi, mheshimiwa bado mimi naona wenzetu wa Bara mfumo wa wanafunzi kuanzia darasa la kwanza mpaka la kumi na mbili mimi ninavyoona kwamba wanafunzi hawajajikita katika kufahamu nini anachokwenda kukifanya. Tunaanza kumchagua mapema darasa la kumi aanze kujua kama ni sayansi au nani. Mheshimiwa wanafunzi wengine wanakuwa na utindio wa akili bado hajazinduka, bado hajajiua mtu yule anafika mwisho kile alichokuwa akisomee ndio ambacho atafeli na kile alichokuwa anafeli ndio atapasi. Kwa hivyo, ningeshauri kama kunakuwa hakuna ulazima sana basi asizuiwe mwanafunzi asome masomo yote halafu huko mbele atatizama tusimlazimishe lazima usome kitu hiki, vitu vyengine vinafikia wakati unakuwa kidogo sijui kama mtu anaweza kujielewa.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme na skuli yetu za maandalizi iliyoko Madungu, mheshimiwa ni skuli ya kupigiwa mfano sana watu wake wameshakuwa madaktari waliosomeshwa pale, wameshakuwa walimu ile skuli inajitahidi sana. Katika skuli zako za serikali ambazo ni za maandalizi Skuli ya Madungu mheshimiwa ni ya kupigiwa mfano na mpaka sasa hivi iko hai. Kwa hiyo, ningekuomba kwa jicho la huruma uitizame sana ile skuli, wanasheria, madaktari wameshasoma sana pale. Kwa hivyo, ningekushauri sana lile eneo ukalitizama kwa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme tu kwamba kweli mfumo wa elimu wa Zanzibar kwa kweli ni mzuri na sasa hivi mashule yetu na vyuo vyetu vimehamasika sana kusoma. Lakini mheshimiwa tatizo linakuja kwenye kupasi, mheshimiwa vyuo vyetu sijui ndio tunapata ripoti mtu katika *form IV* unasikia skuli za Zanzibar ndio za mwisho. Mheshimiwa hebu fanya utafiti Mwenyezi Mungu akikujaalia ujue hili tatizo linaishia wapi, si vizuri tunavyopata aibu kama hii. Kwa hivyo, najua unajitahidi lakini usione haya, usimuonee mtu haya, msilinde na wala usichukulie hisani yoyote mtu aliyekuwa unajua kama anatuvurugia kwani sekta yako ni nzito. Kwa hivyo, ni lazima ugeuke mbogo aliyejeruhiwa usitizame mbele wewe ni kupiga tu, kwa sababu mfumo wetu wa elimu ushakuwa mkubwa sana, matokeo yake yetu ya elimu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Sarahani naomba umalizie.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mheshimiwa nishakusikia ngoja tu niunge mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapa baraka mawaziri wangu wote wawili Mwenyezi Mungu awajaalie waendelee na kazi nzuri na mimi naunga mkono hoja za kamati na mawaziri. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu juu ya ripoti hii. Kwanza kabisa niungane na wenzangu walionitangulia hapo mwanzo akiwemo mwenyekiti wa kamati hii kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi zake anazozifanya za kuimarisha sekta hizi muhimu ambazo ni Sekta ya Elimu na Sekta ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika mchango wangu ambao nimekusudia kwa hii leo na nianze na Wizara ya Afya katika changamoto zilizoelezwa kwenye ripoti hii, nianze na changamoto ya uhaba wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uhaba wa bajeti kwa kweli linakwamisha juhudi mbali mbali ambazo zinakusudiwa kutekelezwa katika wizara hii. Tukiangalia wizara hii ina vitengo vingi ambavyo tunavitegemea katika suala zima la upatikanaji wa afya kwa maisha ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia miongoni mwa vitengo vilivyomo katika sekta hii muhimu Kitengo cha *Physiotherapy***.** Kitengo hiki ni kitengo ambacho kiko katika wizara hii lakini pia hakiko kwa ajili ya watu wenye ulemavu tu, kitengo hiki kiko kwa ajili ya watu wote ambao watapatwa na matatizo mbali mbali. Tukiangalia kitengo hiki kipo kwa miaka mingi sana na mategemeo ya kila mwananchi ambaye anapatwa na tatizo la ulemavu, tatizo la ajali, tatizo la ugonjwa huwa anategemea kwenda kupata huduma zikiwemo za marekebisho, za mazoezi pamoja na matengenezo ya vifaa bandia. Lakini cha kusikitisha kwamba kutokana na uhaba wa bajeti wanaopewa wizara hii kitengo hiki kila siku inapokuja bajeti tunaposikiliza Wizara ya Afya kimetengewa bajeti lakini hadi leo kitengo hiki hakitiliwi bajeti na tatizo hatujui ni kitu gani.

Kitengo hiki kina kazi kubwa mbali ya mazoezi lakini pia ndicho tunachotegemea kitengeneze miguu bandia. Sasa hivi tukiangalia ajali ni nyingi watu wengi ambao wanapatwa na ajali pamoja na maradhi yakiwemo ya kisukari wanakuwa wanakatwa viungo ikiwemo miguu na mikono. Sasa tegemeo letu kutokana na ugumu wa upatikanaji wa visaidizi hivi kwanza ni ghali sana, kwa sasa hivi mguu mmoja wa bandia ni shilingi laki saba (700,000), tukiangalia hali zetu ni wanyonge wengi wetu na hizo shilingi 700,000 mguu huo hauwezi kutengenezwa hapa wanakwenda kutengeneza Bara na huko Bara anahitaji nauli. Lakini akifika kule siku ile ile sio kama anakwenda kununua dukani inabidi akae hoteli kwa muda wa siku ambazo atapangiwa, apimwe, atengenezewe unyayo, asubiri afanyiwe marekebisho arudi baadae mguu ule unatengenezwa arudi tena kwa kwenda kuuchukua. Kwa hivyo, utakuta ile shilingi 700,000 inaweza ikafika milioni na ukitizama watu wengi ni masikini.

Kwa hivyo, ingekuwa ni vyema wizara hii ikaongezewa bajeti ili ikaweza kukiwezesha kitengo hiki kikaweza kufanya kazi zake vizuri. Mbali ya kutengeneza miguu bandia lakini vile vile wanatengeneza visaidizi mbali mbali ambavyo wanatumia watu wenye ulemavu pamoja na watu ambao wanapata uvunjifu. Sasa kuna vifaa vingi ambavyo wanahitaji kununua.

Vile vile tukiangalia kitengo hiki kina wataalamu ambao wamesomea fani hii na hawako wengi ni wachache, kutokana na kuwa kila siku kitengo hiki hakiingiziwi bajeti wasiwasi wangu wataalamu hawa kwa vile wenzetu huwa wanawachukua wakenda kufanya kazi hasa *CCBRT* Dar es Salaam, Msasani wasi wasi wangu kitengo hiki kutokuingiziwa bajeti kwa kila siku tusije tukawavunja moyo watendaji hawa na baadae wakaona hawana faida na elimu waliyoisoma wakatafuta sehemu ambapo watapata kazi za kufanya.

Kwa hiyo, ushauri wangu serikali kupitia Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba kitengo hiki wanakiwekea bajeti yake kama inavyowekwa na wanawapatia kama ilivyopangwa kwa lengo la kusaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika changamoto ya kupungua kwa maadili ya kazi kwa baadhi ya wafanyakazi. Niungane na maoni ya kamati hii ni kweli kabisa kuna baadhi ya wafanyakazi bado maadili yao sio mazuri na tukiangalia sekta hii inatoa huduma kwa wananchi, zaidi kauli zinakuwa sio nzuri kwa baadhi ya wafanyakazi. Siku zote hapa huwa tunazungumzia wale walinzi wetu pale na wao vile vile maadili yao sio mazuri, pamoja na kuwa tunaambiwa kwamba tunakuwa tunazongea wagonjwa lakini na wao hawana maadili mazuri.

Kuna siku mimi mwenyewe imenikuta kadhia hiyo, nimekwenda mimi na mwenzangu mmoja kwa mlinzi pale chini pamoja na uheshimiwa wangu lakini nilimuomba samahani naomba unisaidie, ilikuwa kama saa sita na nusu hivi, naomba nipande juu kabisa kuna mgonjwa wangu nataka kumuona, nikamwambia samahani nakuomba mlangoni chini pale, kumuonesha kitambulisho alikichukua akakirembea na akanishuna kitendo ambacho kilinikasirisha. Kwa nini asinisikilize halafu na kwa nini anishune na nimemuomba samahani. Pana watu pale pale wakanambia mama stahamili hayo ndio mambo yetu.

Kwa hiyo, ushauri wangu mategemeo yangu ile ni kampuni ambayo tumeichukua kwa ajili ya ulinzi, kutokana na changamoto hiz na malalamiko ya kila siku ya watu lazima tukae wizara tutafakari kuna nini kutoka kwenye kampuni hii? Ikiwezekana kama hawatufai kwa nini tusitafute kampuni nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika wizara hii hii, pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na wizara hii tunakubali kwamba kuna mapungufu kwa baadhi ya dawa, lakini ningeiomba wizara kwamba kuna matatizo ya watu wenye ulemavu wa akili. Watu hawa wanatumia dawa kila siku na maisha yao yote ni dawa. Kwa hiyo, tufanye jitihada za makusudi tuweke bajeti yetu maalumu kwa kununua dawa hizi, kwa sababu walengwa wanaotumia dawa hizi wanakujazao Hospitali ya *Mental* kuchukua dawa wazazi yaani kwa lengo la kusaidia watoto wao wanapokuja pale pengine anapata dawa moja tu nyengine inabidi akanunue na dawa hizi ni ghali na maisha yetu ni magumu na pengine mtu ana watoto wanne. Kwa hivyo, wizara ingefanya jitihada ya kuhakikisha dawa hizi zinapatikana tena kwa wakati na kusaidiwa bure.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 6 hapa kuna mtaalamu mmoja tu katika Hospitali ya Makunduchi ambaye anakwenda siku moja ya Jumanne. Tukiangalia wagonjwa wanakwenda kila siku wa wilaya nzima, lakini sio kwa Wilaya ya Kusini tu hata Wilaya ya Kati pia wanategemea hospitali hii wakiwemo watu wa Unguja Ukuu, Bungi, Kikungwi na Uzi wanatemea hospitali hii ya Makunduchi. Kukosekana kwa mfanyakazi huyu kuwa mmoja mimi naona tunamtwika mzigo kwa sababu siku ya Jumanne anafanya kazi za wiki nzima na mahitaji yako mengi, hatuoni kwamba mtu huyu mmoja tunamtwika mzigo mkubwa na mtu wenyewe anajitolea. Kwa hivyo, wizara ifanye utaratibu wa kuhakikisha pale anapelekwa mtu ambaye atakuwa na dhamana na ambaye amewekwa makusudi kwa ajili ya *ultrasound* ili kupunguza hizi changamoto ambazo zinawapata wananchi.

Nikiendelea kifungu cha 8 kuna kuharibika kwa mashine ya kufulia nguo. Mimi najiuliza kama mashine ya kufulia nguo hospitali imeharibika vipi nguo hizi zinaweza kufuliwa, wanatumia njia gani kwa kufua nguo hizi? Hasa tukizingatia sasa hivi kuna maradhi mengi ya kuambukiza hatuoni kwamba tunamtafutia majanga huyo mfanyakazi. Sasa wizara ijitahidi pamoja na ukosefu wa fedha lakini ijitahidi hii mashine itengenezwe ili kunusuru maisha ya wafanyakazi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja hapo hapo ukurasa wa 6 kifungu cha 12. Katika kituo cha Kizimkazi Mkunguni na Dimbani kuna ukosefu wa maji, kwa maana hiyo maji hayapatiokani katika vituo vya afya vipi huduma hizi zitakwenda. Tukiangalia afya ni usafi na huwezi kufanya usafi kama huna maji. Kwa hiyo, suala la maji ni muhimu katika vituo hivi. Kutokana na hili sasa, ninaiomba Mamlaka ya Maji kufanya jitihada zake zote kuhakikisha maji yanapatikana katika vituo vile. Kwa sababu kituo kama hakina maji hali ya usafi haitokuwepo ndio tutasema vituo vyetu vichafu wafanyakazi hawafanyi kazi, lakini kumbe kunasababishwa na ukosefu wa maji kama huna maji huwezi kufanya usafi. Kwa hiyo, Mamlaka ya Maji ihakikishe katika sekta hizi muhimu wanafanya jitihada zao zote wahakikishe maji kule yanapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla nishauri viongozi wakuu wa wizara hii kutokana na changamoto zote ambazo zimeainishwa hapa wawe na utaratibu maalumu wa kupitia katika hivi vituo wasisubiri ripoti, wapitie wakae na wafanya kazi wao wenyewe watajionea na yale wanayosikiliza ili waweze kuja kukaa waone namna changamoto hizi zinatatuka hasa ukizingatia changamoto nyengine sio kubwa za hivyo, hazihitaji fedha nyingi lakini zinahitaji mipango. Sasa kwa kusubiri ripoti hatutofika pahala lakini wafanye utaratibu wa kwenda wakaonane na wafanyakazi wao vituoni.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Katika Wizara ya Elimu kwanza niwapongeze sana kwa juhudi zao wanazozichukua kuhakikisha sekta ya elimu inaimarika na elimu inapatikana kama ilivyoelezwa katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda ningeomba nizungumzie kwa uchache niende *specific* kwenye Kitengo cha Elimu Mjumuisho. Elimu Mjumuisho imeanzishwa lakini bado naweza kusema kwamba walemavu hawajanufaika na elimu hii. Elimi Mjumuisho inachanganya, tukiangalia ripoti imeeleza madarasa yana viwango vikubwa vya wanafunzi tukitizama mtu mwenye ulemavu anahitaji mahitaji maalum. Kwa hivyo, mwalimu sio rahisi akatoka

kumshuhulikia mtu mwenye ulemavu mwenye tatizo moja akawaacha watu mia moja, hapo ndio unapokuja ugumu wake. Kwa hiyo, kuna haja ya kufikiria upya suala zima la Elimu Mjumuisho ili kuboresha, iboreshwe. Kwa sababu wazazi wanalalamika, watoto pia wanalalamika, tumeanzisha Elimu Mjumuisho bila ya kuwa na zile zana madhubuti, ili tuwe na elimu hii tuwe na walimu ambao wana sifa. Kwa mjini *Alhamdulillah* mambo mazuri, lakini shida iko vijijini kwa watu wenye ulemavu ambao wanasoma vijijini bado wana matatizo. Hapa kuna haja viongozi wa wizara waende kule vijijini wakakae na walimu wanaofundisha wale watoto wenye ulemavu, lakini vile vile wazungumze na watoto wenyewe waseme zile shida zao na changamoto zinazowakuta, ukimkuta mwalimu atazungumza vizuri lakini ukimkuta mwanafunzi yeye ndio atakwambia changamoto gani zinamkabili na uongozi wa wizara ukaweza kuchukua hatua zinazohitajika.

Tukija katika vyoo imeelezwa ubovu wa vyoo. Ubovu wa vyoo hauathiri watu wa kawaida tu kwa mtu mwenye ulemavu una athari mara mbili zaidi. Kwa sababu watu wenye ulemavu wengine wanatumia mikono ukitizama hali za vyoo vile sio nzuri, wengine wanatembea kwa mikono wengine hawaoni choo ni hicho hicho kimoja wanatumia wote, ile ni hatari.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba wizara ikajaribu na hili suala halihitaji fedha ni kujipanga tu kwa skuli yenyewe ione kwa namna gani wanafanya usafi katika vile vyoo.

Sasa nije katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Niwapongeze kwa jitihada zao kwa sababu katika bodi moja inayozingatia masuala ya mahitaji ya watu wenye ulemavu ni Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, wanajali na wanathamini kwa mtu mwenye ulemavu, yeyote anayekwenda pale ambaye ana sifa lazima atapata mkopo kwa hiyo niwapongeze.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umekwisha naomba yaliyobaki yaandike kwa maandishi.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante yaliyobaki nitayawasilisha kwa maandishi na naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii kwa kuwapongeza wale ambao wamechangia kwa muda huu, lakini nitawatangaza wachangiaji watatu wa mwanzo watakaokuja kuchangia jioni nao ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Nadir Abdul-latif na Mhe. Zulfa Mmaka Omar.

Kabla ya kuakhirisha naomba nitoe tangazo kwamba, kesho Jumamosi tarehe 25/2/2017 kutakuwa na semina ya Wajumbe wote wa Baraza kuanzia saa tatu asubuhi, semina hiyo inahusu utekelezaji wa dhana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa itakayofayika katika ukumbi wa mikutano wa Baraza huko juu. Semina hiyo imeandaliwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Ahsanteni sana, nawatakia Ijumaa njema na swala njema. Naakhirisha kikao hadi saa kumi na moja jioni. *(Makofi)*

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea, lakini kabla ya kuendelea, wachangiaji ni wengi ambao wanataka kuchangia ripoti hii, lakini kutokana na muda naomba wachangiaji wote tuwape dakika kumi kumi badala ya dakika 15. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atowe hoja hii.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa hoja ya kutenga kando kanuni ya 58 fasili ya 6 ambayo ndio kanuni inayoongoza majadiliano ndani ya Baraza, na ndio kanuni ambayo inatoa muda wa kuchangia. Kama ambavyo umesema kwa kuwa wachangiaji ni wengi, basi tutenge kando kanuni ili tutowe fursa ya kila mjumbe kuchangia kwa dakika kumi badala ya dakika 15. Kwa msingi huo Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kutenga kando kanuni hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa naomba niwahoji waliokubali hoja hiyo wanyooshe mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na wachangiaji naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akifuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, na Mhe. Zulfa Mmaka Omar ajitayarishe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii wala sitachukua muda wa kushukuru sana. Vile vile na mimi nikuambie tu huko nyuma kumbukumbu zinavyoonesha katika wizara hii hupewa muda maalum kutokana na maneno ninayozungumza mimi ni mazima katika wizara hii. Hata alipokuwepo Mzee Kificho hapa, hukaa kidogo akasinzia ili kunipa muda kidogo kutokana na maneno mazito ninayozungumza katika wizara hii, na Dk. Ali Mohamed Shein ni shahidi wa maneno ninayozungumza katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sikumshukuru Dk. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake katika sekta hii ya afya, wajumbe sote humu ni mashahidi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa Waziri wa Fedha na Mipango hayumo humu ndani, mawaziri hawapo mpaka muda huu tunafanya utaratibu gani. Ndio yale tunayosema. Juzi nilisema humu mawaziri mnamuangusha Mhe. Rais saa ngapi sasa hivi, kuna mawaziri mmoja, wa pili, wa tatu na wanne, kweli tunalitumikia taifa, watu wanatusikiliza nje na wanatuona. Leo ni aibu kule mbele mawaziri hawapo. Umeme unakatika huo. Haya!... *(Vicheko/Makofi)*

(Hapa umeme ulikatika kwa muda kidogo)
(Baada ya muda mfupi ulirudi)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haya ni maneno ya msingi tunayozungumza hata umeme unakatika.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, Mhe. Jaku, nilisema mwanzo dakika zilikuwa 15 na tulimuomba Mhe. Mwanasheria na amekubali, na tulitoa hoja tumekubaliana una dakika 10. Lakini unakwenda nje ya ule mchango wako ambao uliokusudia. Kwa hivyo, nakuomba rudi kwenye hoja toa mchango wako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hii sekta tunayoijadili hapa sio ya mchezo Rais wetu hata katika uteuzi wake hapo mwanzo alipoingia alianza kuteuwa sekta ya afya kumchagua waziri. Sio kwa sababu imeanza na alphabet A, hapana, kwa sababu anaujua umuhimu wa afya huwezi kumdanganya. Sasa hapa tukichangia na Waziri wa Fedha na Mipango hayupo na yeye ndiye mwenye mpango wa fedha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, cha msingi Mhe. Jaku utowe mchango wako kuhusiana na Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini hoja unayoitoa hapa haihusiani na hili, kwa sababu Waziri wa Afya yupo, Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo na nina imani utakachokizungumza kama kitamgusa waziri yeyote kati ya hao ambao unawahisi hawapo, basi watamfikishia kwa sababu serikali ipo, Waziri wa Afya yupo na Mwanasheria Mkuu yupo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ndio maana nakuambia Mhe. Jaku rudi kwenye hoja yako na utowe mchango wako ambao umeukusudia. Kama huna hoja hiyo basi tukuachie ukae kitako ili waendelee wajumbe wengine. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi naona unazidi kuupoteza muda, lakini naanza tena muda wangu saa 11:04. Nasema tena sisi wawakilishi humu ndani au labda nikupe kidogo Sura Til Dhuha, *Fasabih Biniimat Rabika Fahadith*, maana yake nini. Neema za Mola wenu zihadithieni Dk. Shein keshafanyakazi kubwa katika sekta ya afya, sote humu ni shahidi kama hatukuchukua jitihada zake kumpongeza, basi tutakuwa hatujafanya haki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni katika mmoja niliyelalamika humu na nikipiga kelele katika sekta ya afya mmoja ni mimi, ikiwemo sekta ya afya, huduma za wazazi kuweka bure ni kelele zangu mimi ni mwakilishi. Vile vile suala la *ICU* kujengwa nilipiga kelele kubwa, Dk. Ali Mohammed Shein kalisikia na akalifanyia kazi, tuna *ICU* ya kimataifa sasa hivi, naweza kuthubutu kusema hata Aghakhan hana *ICU* kama ile tuliyokuwa nayo hospitali ya Mnazi Mmoja, ni jambo la kushukuru.

Lakini tuangalie pia kaondosha ada za maskuli, kanunua meli moja kubwa sana kwa ajili ya kuwajali wananchi wa Unguja na Pemba. Vile vile nimshukuru pale tulipokuwa na kilio cha wawakilishi sisi kutaka kumuona, na kakikubali. Tofauti na nje kule watani wangu wanavyofikiria. Wanafikiria hapa anakuja Dk. Ali Mohammed Shein labda kuna mengine. Niwaambie tu watani wangu kule anakuja kwa wawakilishi kumuhitaji. Tena wa CCM, anakuja kwa kuitwa na wawakilishi na ni haki yetu ya msingi. Sasa wale watani wangu wasije wakafikiria vyengine vyovyoge, kama mitandao inavyozungumza huko, anakuja kuwasikiliza

wawakilishi wake nini wanachomuitia na hii ni mara ya pili. Wasije wakafikiria huko kwenye mitandao yao hiyo waweke upande. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mwenyekiti wa kamati hii Dk. Mwinyihaji Makame, katika ukurasa wa 2. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2016/17, kufanikisha kutunga sheria ya kuanzisha wakala wa taasisi ya Mnazi Mmoja ambayo inaelekea kuwa Hospitali ya Rufaa, bado haijaelekea hii. Namshukuru sana kwa Kiswahili alichokiandika, bado haijaelekea na tuna kazi hapa, hata Mhe. Naibu Waziri wa Afya alijibu swali namna 23, nikamwambia kidogo arekebishe kauli yake. Alipojibu kwa kutamka kwamba Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Nikamwambia rekebisha hatujafika rufaa bado, na alirekebisha namshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, lakini humu ndani tushukuru kwa ujenzi wa Abdalla Mzee, ni kazi kubwa aliyoifanya Dk. Ali Mohammed Shein, sio kwamba kajenga jengo tupu tu lile, muna vitu ambavyo naamini madaktari wetu wengine hawawezi kuvitumia. Kazi kubwa keshafanya Mhe. Rais.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, niende ukurasa wa 4. Aidha, kamati ilipata takwimu za wafanayakazi 95 waliostaafu na kuelezwa kuwa hakuna wafanyakazi wengine walioajiriwa kuchukua nafasi hii, pamoja na kwamba serikali ilitoa agizo la wafanyakazi kustaafu waajiriwe. Ndio pale ninapomwambia rafiki yangu Waziri wa Afya, hapa kazi unayoifanya tunaiona Mhe. Waziri wa Afya, lakini watendaji wako hawa watakuangusha, watakupa kazi ngumu hii wizara ni nzito, na kama hukuwa makini hapa ukafuatilia mwenyewe basi watakuangusha Mhe. Waziri, kazi unayoifanya tunaiona, wala usifikirie tunakupinga haya ni masuala mazito tunakusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna waziri mmoja humu sitaki kumtaja jina lake alikuwa katuita sisi ili tumsaidie kumsukuma kwa maswali. Lakini mawaziri wengine ukimuuliza sana ana hamaki. Mimi nakushukuru uhamaki, tunasokotana dakika mbili, tatu au nne tunazungumza tena. Tunakusifu sana Mhe. Waziri kwa umakini wako.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ni katika Hospitali ya Kivunge, ambapo kamati imebaini kuwa kwa mwezi hospitali hiyo inafanya rufaa ya wagonjwa 18 mpaka 20, jambo ambalo linapelekea kutumia takriban lita 4,000 za mafuta kwa ajili ya kuwapeleka wagonjwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Hili ni kweli hata hospitali ya Makunduchi lipo. Mimi mwenyewe katika hospitali ya Makunduchi nachangia, kuna *Ambulance* pale Jimbo la Paje inatakiwa ikae pale. Nikuomba katika zile *Ambulance* ulizopokea juzi mpya, sijui kama umeshawapa Makunduchi, lakini wanahitaji na wao. Mafuta hayatoshi, inabidi wawakilishi wengine tuvute mfuko kidogo.

Lakini Jengine la kusikitisha hospitali yetu ya Kivunge hivi sasa chumba cha watu wa *research* ndio kinachotumika kwa ajili ya shughuli za maabara. Kamati wakati wa ziara yake ilielezwa kuwa inahitaji shilingi 800,000 kitu cha aibu. Jana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango jana hapa alisema katika Hansard yake, nathubutu kusema kwamba serikali hii katika kipindi cha miezi sita imekuwa ikiendeshwa kwa fedha zinazopatikana katika vyanzo vya ndani, jana waziri wa fedha kasema. Ndio mana nikasema waziri wa fedha hayupo, sio maneno yangu haya, tunahitaji bado wahisani vile vile.

Sasa hapa atowe jibu atuambie kajipanga vipi katika hoja zake na yeye anatakiwa kujibu, sekta ya afya ni muhimu, sasa yuko wapi. Naibu Waziri vile vile kateleza hapa asubuhi hatukutaka kumpiga kanuni. Anatuomba wawakilishi sisi misaada, alipokuwa akijibu swali asubuhi, huku serikali inasema vyengine anatuomba msaada. Lakini kama hapo hapatoshi Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Makunduchi ilipotembelewa ulikutwa ujenzi wa nyumba za madaktari zinaendelea. Hata hivyo, changamoto ni ukosefu wa fedha ambazo kwa kipindi cha ujenzi, mafundi wanaojenga ambao walikuwa wanajitolea walikuwa wanadai shilingi milioni 3,700,000/-, wanajitolea na hakuna milioni 3,700,000 ni kitu chakusikitisha hiki Mhe. Mwenyekiti, hasa Hospitali ya Makunduchi, ukitoa kwa *population* naweza kusema mji mkuu wa Zanzibar uko Makunduchi, nathubutu kusema hivyo kutokana na watu kuwa wengi wanaitegemea hospitali hii ya Makunduchi na hasa wananchi wa Makunduchi.

Vile vile kuna kilio cha maslahi ya wafanyakazi wa vituo vyote, hapa ndipo penye kilio kikubwa, na wafanyakazi watatukimbia kama hakuna motisha hapa. Pia kituo cha Kizimkazi Mkunguni, Mhe. Mwantatu alizungumza hapa. Umeme mimi mwenyewe nimeshachoka kununua umeme katika kituo cha Kitogani, Mwejuu vyote vinasubiri kupewa umeme, sio kazi yangu mwakilishi mimi, na tokeni mkaulize.

Mhe. Mwenyekiti, unajua wakati mwengine unatakiwa usijisifu, lakini wakati mwengine ukijisifu wengine ndio kidogo watapata mfano. Kuna hadithi za kuiga, tuigane kwa mambo mazuri sio mabaya. Jambiani kwa muda mrefu nanunua dawa hospitali. Kama sio asilimia 80 au 70 dawa nanunua mimi, nilikuwa sitaki kujisifu kwa hilo. Lakini unaambiwa ukifanya jambo jema na mwengine anaweza kuona choyo kwa mambo mema, lakini tusione choyo kwa mambo mabaya. Wagonjwa wengine wanakuja kufuata dawa pale Jambiani huwezi kuwazuwia, bado bajeti ya dawa pamoja na jitihada zinazochukuliwa bado ni ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika hospitali ya Mnazi Mmoja bado kuna changamoto nyingi, wala siwezi kusema ni hospitali ya rufaa. Waziri hawa watu wanarudia tena mara ya pili juzi tumeshuhudia *lift* kukwama, hospitali kubwa kama ile kama hapana mtu wa umeme aliyeajiriwa kukaa masaa 24 ni hatari, hawa watakuharibia kibarua chako Mhe. Waziri.

Mimi hapo kipindi cha nyuma nilikuwa nikionekana nina ugomvi na Naibu Waziri aliyepita, baadae akapata Waziri wa Kilimo, lakini watu hawakunifahamu, baadae wakanifahamu. Hoja zangu mimi ni za wananchi. Ndipo niliposema Dk. Ali Mohammed Shein katika kipindi chake cha mwanzo Wizara ya Afya aliwapa kipaumbele kamteuwa kwanza Waziri wa Afya, sio kwa sababu imeanzia na alphabet A, ni kutokana na umuhimu wa afya za watu anavyozijali. Lakini watu wakanifahamu, na sasa hivi nakushukuru Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo unanifahamu nia yangu. Hapa hapa kama hukuwachukulia hatua ukawafukuza hawa watakuharibia, utendaji wao mbovu, umeshafika wakati. Siku moja tu nilikuona uliondosha uvivu, siku uliopokea Ambulance ulitoa maneno mazito, nikusifu kwa hilo, huu ukimpya katika sekta za afya hatuwezi kwenda.

Juzi kabadilishwa Katibu Mkuu, pengine hatofika muda Mwenyezi Mungu asijekujaalia katibu mwengine aje abadilishwe. Tunafanya nini, hatuwezi kwenda katika mambo kama haya na nia ya Dk. Ali Mohammed Shein mtakuwa hamuifikishi. Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 2 mwezi wa Oktoba, katika vyombo vya habari vimetangaza kuwa kipindi chake cha miaka miwili ya mwanzo matibabu anataka yawe bure, sio maneno yangu mimi ni vyombo vya habari

vimetangaza. Yatakuwa bure kweli katika hali kama hii, anafanyakazi kubwa. Simsifu kwa sababu nataka uwaziri au naibu waziri hapana, siko huko. Lakini haki yake apewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi narudia tena

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, malizia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, nakuja. Nilikuwa sitaki kugusa maana yake hii elimu haina muhimu kuliko afya. Afya ina umuhimu wake, utampelekaje mwanafunzi skuli bila ya kupata afya, ina umuhimu wake, afya kila kiumbe hai inahitaji. Lakini waziri tunapopitisha bajeti humu mnakuwa laini kukubali. Kuna ahadi ilitolewa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhusu nyumba za walimu Jambiani. Nakuambia ingali mapema sasa hivi ile nyumba kule sasa hivi haikaliki wala haitizamiki, uliniahidi tutakwenda utaishughulikia lakini mpaka leo kimya, mimi nilikuwa sitaki kuchangia kabisa wizara ya elimu, sekta yangu hii ya afya, lakini hali iko wapi. Kanuni zetu zinatukataza za Baraza, lakini hali haipo tutafanya nini. Hali hairidhishi kabisa kwenye hiyo nyumba, inanyesha mvua mtu anaweka mabakuli kukinga maji ya mvua, tunakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kwa haraka suala la afya lina umuhimu wake na kama halikuangaliwa na bajeti yake. Mimi ningemuomba waziri wa Fedha na Mipango, kuna mambo matatu angeyapa muhimu sana, sekta ya afya, elimu na maji, tungeelekea huko kwa muda huu sasa hivi, hayo mengine yatakuja baadae. Leo vituo vya afya havina maji, hatuwezi kukulaumu Mhe. Waziri wa Afya, maana yake utasema sio kazi yangu, wenyewe ni ZAWA

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku Hashim, muda wako umemaliza. Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namuomba Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, akifuatiwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar, na Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahman Rahim*. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na leo kwa kuwa Ijumaa ni skukuu yangu mimi nimeamka vizuri na hii nitaichangia vizuri.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, mimi nitampongeza sana Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba yeye binafsi katika uongozi wake mbali ya maendeleo yote anayoyafanya mazuri, basi kuna mambo mawili kafanya mapinduzi yake mwenyewe, na mapinduzi haya ukiwacha ya mwaka 1964, basi mapinduzi ambayo mapya aliyoyafanya yeye ni suala la kujenga hospitali mpya mbili. Pemba hospitali ya Abdalla Mzee kaijenga yeye mwenyewe binafsi na hakuna kiongozi yeyote ndani ya Zanzibar aliyeweza kujenga hospitali binafsi kama ile yeye mwenyewe. Zote tumezikuta baada ya uhuru tumezikuta hospitali kubwa, lakini yeye nampongeza sana kwenye suala la afya kaweza kutengeneza mwenyewe na kusimamia na kujenga hospitali kubwa zenye mfano. *(Makofi)*

Vile vile hospitali hizi za Mnazi Mmoja mpya, pamoja na ile ya Pemba ya Abdalla Mzee, ule ni mfano kwake yeye. Mimi nitampongeza sana na hasa katika uongozi wake ambao uko safi, tofauti na viongozi wengine, sitaki kuwazungumza. Lakini ukiangalia historia Dk. Ali Mohamed Shein hana historia kama walizokuwanazo viongozi wengine duniani au ndani ya taifa letu, yuko

safi kwa upande fulani japokuwa binadamu hakuna aliyekamilika, na ndio maana tukawa tunawaambia mawaziri mara nyingi wawe saa nyengine tunapowauliza swali wasione tabu kukataa au kusema kwamba hiki kitu tumekosea au kipo. Watajaribu tu kujibu jibu ilimradi turidhike, lakini msifike wakati nyinyi ni binadamu mnapoulizwa kitu mnatakiwa mutoe ukweli hatutoweza kukulaumuni sana kwa sababu hii Serikali ni watu na watu hawajakamilika, lakini leo utamkuta Waziri unamwambia hasa hii sumu anakwambia hii soda kunywa sukari anakataa kabisa yaani ile sumu ya kumuua mtu yeye Waziri anakwambia sukari kunywa, tunaomba sana muwe wakweli.

Juzi Mheshimiwa Simai Mohammed Said alizungumza kitu akaambiwa aombe radhi lakini mimi humu asije akajaribu mtu akainuka na kanuni siombe radhi mtu yoyote, mimi ninachokizunguma ni kweli tunamuangusha sana Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein na yupo safi kwenye mambo kama haya hana matatizo kabisa na anakuwa mkweli na muwazi hata kwenye TV anapozungumza unamuona, lakini sijui vitu gani ambavyo vinasababisha mazonge kama haya ukienda suala la baadhi ya watendaji wanapewa elimu wanakuja kuletewa mafunzo Zanzibar lakini unakuja kuta mwisho wake wanakataa kwenda makwao kwenda kuwatibu ndugu zao, tunazo taarifa nimefuatiliwa kuna ndugu zetu wa Pemba wanatolewa kule kuja kusoma huku ili baadae warudi mahospitali ya Pemba kuwasaidia ndugu zao basi wanagoma wanaolewa huku, wanaoa hawataki kurudi kule sababu ni nini.

Leo hii inafika Mhe. Rais anafanya mambo yote muhimu na anatumia nguvu zake zote lakini mwisho matokezeo yake fadhila zake ndio hivyo baadhi ya watendaji wanaua watoto, kesi hazishi mahospitali, utendaji mbovu labda sijui wapewe kitu gani waweze kuridhika waweze kutenda au kama kuna siasa inatendeka kwenye masuala ya afya utakuja kujibu nini huko mbele, kwa sababu isijekuwa labda watu siasa wanaingiza kwenye afya kuna mambo si ya kuchezea unataka kucheze kachee na mapolisi ujue moja. Lakini sio sehemu ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ninachotaka kuzungumza kwamba ifike wakati Mhe. Waziri wa Afya leo nachangia kidogo dogo unifahamu vizuri, hospitali ya Mnazi Mmoja na zile nyenginezo angalau basi ifike hatua uzifanyie *renovation* utie angalau *tiles* au utie kama kapeti majumba yale yaliyobakia wacha haya mapya yanatakiwa kidogo kufanyiwa *renovation* kuna sehemu kama vyoo vya Mnazi Mmoja hakuingiliki, madokta au manesi saa nyengine tusiwalaumu wagonjwa wanaokwenda pale wengine wanatoka mikojo, wengine wamepata ajali tukiambiwa sisi tuwabebe tuwachukue tunaona haya nguo zitachafuka harufu. Lakini ifike wakati huu mzigo tusiwarushie tu ma- *nurse* sio ma-*urse* wote wanaofanya hivi wako katika hali ngumu mambo magumu, lakini kwa wale wachache wanaosababisha mazonge kama haya ya kuweza kusababisha mpaka watoto kufariki kutokezea matatizo makubwa makubwa ndani ya hospitali basi wawe c*are full* sana kwa sababu kama hawawezi kazi basi waseme waache kazi.

Tunaowatakasisi watu wanaoweza kufanya kazi wakajua nini wafanye katika hospitali, naomba sana hospitali ambazo ndogo ndogo ujitahidi sana ziwe katika hali nzuri hospitali haziko hali nzuri kabisa, na nakuomba sana vituo vyangu vya afya kwa hisani yako vya jimbo la Chaani havifanyi kazi vimekufa. Kituo ch Chaani kubwa hakifanyi kazi, kituo cha Chaani Masingini hakifanyi kazi nakuomba sana jimbo ambalo lina watu wengi, jimbo ambalo lina wagonjwa wengi na tunahitaji pale vituo vya afya.

Nikiendelea kwenye suala jengine Mhe. Waziri wa Afya ningependa kukwambia jambo jengine mabarabarani tunakuta wengi sasa hivi ambao waliokuwa hawana akili wanaitwa wakosefu wa akili ni wendawazimu, kwa nini mnashindwa kuwahifadhi mnawadhalilisha nje wanatembea wengine hawana nguo wangine wanajipiga, wengine wanakata mabarabara hawajui wanafanya nini kwa sababu si wa kuwalaumu lakini nashangaa kwamba kwa nini mnashindwa kuwadhibiti, wanapiga watu wengine wanataka kuwabaka wanawake njiani wale wendawazimu wa kiume ifike hatua muwazuie muwaweke katika hali nzuri, wawekeeni TV wazungumzishwe na watu wenye *Experience* ya kuzungumza na watu waliokuwa hawana akili. Kwa sababu tutakapowaachia itakuwa tuna wadhalilisha tuwajengee mazingira mazuri na wao kuna siku akili zitarudi na kuna siku mimi na wewe tutakwenda *mental* pengine hatuwezi kujijua dunia hii haijesha, nakuomba sana Mhe. Waziri sisi sote hatujakamilika na naomba sana utendaji uwe mzuri kama ulivyokuwa kama alivyokwambia Mhe. Jaku kwamba mtoto wa mjini hata ukipigwa pigwa kidogo huwekei rohoni ni jambo zuri tofauti na wengine wakinuna nuna mimi naona kama wanaleta sijui *design* zipi, humu tunafahamishana humu tunaelezana ukweli.

Jambo jengine ambalo la waganga Mhe. Mwenyekiti, hawa waganga wa kienyeji hawa ndio waliokuwa wakinunua viungo vya maalbino tunawachilia na tunawapa kichwa na unakuta sisi Waheshimiwa humu asilimia kubwa sana tunawaabudu waganga hatumjui Mwenyezi Mungu, ndio maana hatujawahi kuzungumza humu ndani. Mimi nina uhakika viongoi asilimia 80% kama hawajapita kwa wachawi bado hawajaingia humu ndani wanavyofikiria wao, lakini waliowaingiza ndani ya Baraza la Wawakilishi ni Mwenyezi Mungu peke yake sio mganga wala mchawi hawa wote Mheshimiwa ikiwezekana kawaike, hawa ndio wanaonunua viungo, hawa ndio wanaoharibu watu wanawapa madawa kama yule wa kule aliyewapa watu wakabadilika rangi wakaibuka rangi ya kijani kule Bara kule masuala ya dawa ya UKIMWI yule mzee sijui anaitwa mzee gani na sijui kafia wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir naomba umalizie una dakika mbili.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Allahuakbar haya ndio matatizo walahilaadhim kila siku tunasema vitu kama hivi dakika kumi.

Mhe. Mwenyekiti, masuala ya maji Wizara ya Ardhi inashughulika na mambo ya maji inawapa wanachi kunywa je upande wako wanakushirikisha vipi kuhakikisha maji yale ni masafi hayana wadudu na uchagu wa kusababisha maradhi.

Lakini jambo jengine waganga nimeshakwambia Mheshimiwa hawafai ndani ya jamii waongo.

Jambo jengine ninachotaka kusema kwenye suala la Wizara ya Elimu, nashukuru sana Serikali inajitahidi kwenye kutoa elimu bure kwenye mazingira mazuri, lakini kitu ambacho kinachochangia wanafunzi kufeli ni mazingira tatanishi maskuli yanavuja, maskuli hawana maeneo ya kukaa, hawana madeksi kuna matundu, joto kali hakuna mafeni na ndio maana mimi nikasema kwa sasa hivi tununueni busati, bora busati kuliko kukaa chini. Wale wazee hawana kitu huku *uniform* zinachanika tusione tabu wala tusione haya tunaona haya ya nini, kwani lazima tujilazimishe kitu ambacho hatuna uwezo nacho kwa sasa hivi tupekekeni majanvi Mhe. Waziri tuko tayari kushirikiana na wewe watoto wanachafuka mazingira magumu ndio maana wanafeli, kwana wanatoka huko kilomita mbili washachoka wakifika kule maudhi hata feni hakuna.

Jambo jengine kuna kituo cha walimu TC kipo Mkwajuni kwa ajili ya Wilaya kuratibu hawana gari mazingira magumu hivi shughuli za uratibu ya mambo ya elimu ndani ya Wilaya ya Kaskazini (A) Mkwajuni kituo kile watafanya vipi kazi walimu wale, posho ndogo, gari hakuna lakini mimi leo nimesema sitaku kuzungumza sana kwa sababu ijuma ni sikukuu yangu na nimeshaona dakika zimekwisha.

Mimi nashukuru sana na naunga mkono hoja na *message* wameshaipata kwamba wajitahidi tutakutana mbele mkifanya masihara mimi sina undugu sina ujamaa kwenye kazi tutakutana mbele, lakini hayo ni maombi yangu na ripoti hii nai- *support* ahante sana. *(Makofi)*

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Asante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika mchango huu, awali nianze kumshukuru Mhe. Rais kwa kutuwekea hospitali nzuri ya Mkoani nasisi Wapemba tukawa tunafarijika na huduma za afya ambayo ni nzuri ina viwango kwa hili tunampongeza na Mwenyezi Mungu atamlipa kwa imani yake juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nataka nianze na kwetu mcheza kwao hutunzwa Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza na Hospitali ya Chake Chake, kwa kweli hospitali ya Chake Chake ina matatizo mengi tukianza na tatizo la paa, Hospitali ya Chake Chake sasa hivi takriban ni miaka sita tunakuta paa lake ni bovu kwa hospitali nzima sio kwa wodi moja moja. Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya Chake Chake *sealing* zake zote ni mbovu na paa ni bovu kwa hivyo kipindi cha mvua madaktari wanapata kazi ya kusogeza vitanda pembeni ili wagonjwa wasipate kuroa wakazidi matatizo ya maradhi.

Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa kwa suala la paa tunamuomba sana atuwekee sawa kwa sababu hospitali ile ya Chake Chake inachukua watu kutoka vijiji mbali mbali tukitizama sasa hivi Mji wa Chake Chake unakua, watu wengi kutoka Wete na Chake Chake wanakimbilia pale kuliko kwenda Mkoani kwa sababu ya hali yao ya kifedha wao wanaona kwamba Mkoani ni mbali. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri suala hili katika bajeti yake aliangalie sana ni kilio ambacho tunamlilia na tunaamini kwamba Waziri huyu ni msikivu, ni mtaratibu na anawapenda

watu wa Chake Chake naamini katika bajeti yake hii Hospitali ya Chake Chake naamini mara hii itatiwa paa jipya.

Katika hospitali hiyo hiyo ya Chake Chake wodi ya watoto Mhe. Waziri naamini kwamba umeshawahi kufika mimi nakuomba tu tuende tukakague ile wodi ya watoto, ile wodi sasa hivi imekuwa mbovu manzi, mbu, madirisha yake ni mabovu, vitanda vibovu na watoto wengu wakati mwengine wanapelekwa wakiwa katika hali mbaya, vyandarua havifai, wodi ile ina harufu chafu kutoka nje kiasi kwamba wazee na watoto kwa kweli inakuwa ni mtihani kukaa katika wodi ile. Mhe. Waziri nakuomba katika mambo yako yote wodi ile uiangalie kwa sababu mtoto anapopata nafuu na yeye anatamani kucheza katika wodi zile, lakini ukitizama chini pachafu haparidhishi hata kidogo badala ya kwenda kuwatibu watoto wasi wasi wangu tusijekwenda kuwasababisha maradhi kutokana na kuokota vitu chini wakala, watoto kama unavyowajua hawaaminiki.

Nakwenda kwenye wodi ya wazazi kwa kweli ni mtihani mpevu ambao hautibiki mimi nasema, kwa sababu mule ukienda kuna kipindi unakuta hata *gloves* hamna kwa kweli ni mtihani mkubwa tunawaomba sana watusaidie na naamini kwamba Waziri huyu ni msikivu sana na ni rafiki yangu wa karibu naamini atasikia tu kilio changu na mimi nimwambie kwamba nipo pamoja na yeye tukimaliza twende tukakague pale na tumuombe Mhe. Rais tujue nini atatusaidia.

Tukitoka hapo twende katika mashine ya kuwekea sawa viungo vya watoto, pale Chake Chake kuna watoto ambao wanazaliwa katika viungo si vizuri sana, kwa hivyo pale panatakiwa mashine kwa ajili ya kunyoosha viungo vile. Lakini cha kusikitisha mashine ile ni chakavu na mbovu ndio hapo inapolazimika kwamba mzazi amchukue mtoto yule na ampeleke Mkoani au ampeleke Unguja, hali ya kifedha tunaijua kwamba ni ngumu na mtoto yule kila baada ya wiki anatakiwa kwenda kufanyiwa mazoezi na kunyooshwa viungo vile, kwa hivyo namuomba ile mashine japo asinunue mpya lakini aifanyie matengenezo ili watoto wale wapate kunufaika kwa sababu kiungo cha binaadamu chochote ni muhimu.

Tukitoka hapo Mhe. Mweyekiti, mimi nataka niende katika Daktari wa macho, katika hospitali ya Chake Chake kuna tatizo la daktari w macho na tunaangalia kwamba vijana wengi sana sasa hivi wanapata matatio ya macho kutokana na kusoma sana, watoto wale wanalazimika kwenda Wete kutafuta matibabu ya macho na wakati mwengine unakwenda kule Wete unamkuta kwamba Daktari hayupo unarudi tena. Kwa hivyo tunakuomba ututafutie daktari japo mmoja anayehusiana na matibabu ya macho ili nasi tufaidike katika huduma hii.

Sambamba na hayo tuwende katika daktari wa usingizi pale pana daktari mmoja wa usingii daktari yule kumpata kwake ni usumbufu kidogo anakaa mbali na *ambulance* iliyopo pale hospitali ya Chake Chake si nzima ni mbovu kidogo, kwa hivyo saa nyengine anatafutwa daktari yule mpaka watu wanatahayuri wafanye nini. Kwa hivyo tunakuomba utusaidie utuletee angalau

watu wawili wa usingizi katika hospitali ile ili tatizo hili liweze kuondoka na wapigaji kura wetu nao wajisikie kwamba wanafaidika na nguvu hizi za Serikali.

Nikitoka hapo niende kwenye kituo cha mkono kwa mkono tunaona kwamba kesi za udhalilishaji sasa hivi zinazidi siku hadi siku, pale katika kituo cha mkono kwa mkono wanapelekwa watoto ambao wamebakwa au wamefanyiwa kosa lolote la kijinsia, lakini tatizo ambalo liko katika kituo kile kwanza kituo kile ni kidogo kina vyumba viwili, na mtoto kama huyu akipelekwa anataka ahojiwe katika sehemu ambayo nzuri bila ya kuletewa matatizo. Pia katika kituo kile kina madaktari 25 wa kujitolea wakiwemo kama madaktari watano wa kuajiriwa, lakini tatizo wale madaktari waliopo wanaofanya kazi ni watatu tu na hao watatu wanakataa kwenda Mahakamani kutoa ushahidi, hivi tujiulize hili tatizo la udhalilishaji litamaliza vipi wakati madaktari wale wanaogopa kwenda Mahakamani kutoa ushahidi wanasema kwamba Mahakamani wanakwenda kuulizwa masuala mazito mimi nakataa kwa sababu wakienda Mahakamani naamini kwamba hawendi kuulizwa kwamba mbao inapasuliwa vipi hilo wanaweza kusema hawaliju kwa sababu si fani yao. Lakini ukifika unaulizwa mtoto huyu kafanywa nini kafanywa hivi na hivi kwa hivyo nawaomba madaktari hawa wajitolee wasiogope waende Mahakamani kwenda kutoa ushahidi ili tupate kumaliza tatizo la udhalilishaji Zanzibar.

Nikitoka hapo niende katika kituo cha afya Mwembeladu katika kituo kile Mheshimiwa kuna tatizo la msongamano wa watu ambao wanakaa pale kwa ajili ya kusubiri daladala, nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa imani yake kituo kile cha dala dala pale kiondoshwe ili upungue msongamano wa watu na magari na wagonjwa wale au wazazi wanaopelekwa pale kwa ajili ya kwenda kujifungua wasikutane na kadhia ya msongamano wa watu wapate kuwahishwa kwa wakati kwa ajili ya kupata huduma ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Chuo cha Afya Mbweni, Chuo cha Afya tunakuta kwamba kuna vijana wanasoma na vijana wale wakimaliza kusoma wanatakiwa wafanye kazi zao za vitendo, lakini la kusikitisha wanakwenda hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda kufanya *Practical* wakifika kule yale ambayo wamesomea hawayapati kuyafanyia mazoezi kutokana na uhaba wa vitendea kazi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri wanafunzi wale wanataka wafanye *practical* kwa sababu mtu anasomea fani lakini anashindwa kuifanyia *practical*, kwa hivyo unamkuta kama anasomea kung'oa jino lakini mwisho wa siku anashindwa kufanya kazi ile na badala yake wanakwenda kutuumiza vichwa. Kwa hivyo namuomba sana suala hili pia nalo aliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, najua unataka kuniambia lakini namalizia haraka haraka katika bodi ya mikopo nimshukuru Mhe. Waziri kuweka vizuri bodi ya mikopo, lakini pia naomba Mhe. Waziri wa Elimu atakapokuja mara hii ile bajeti yake katika bodi ya mikopo kidogo aichuchuze tena zaidi kwa sababu kuna vijana wengi ambao wanataka ile bodi ya mikopo lakini wanakosa fursa

hii. Pia niwaombe wale ambao walisoma kwa mikopo basi na wao warejeshe zile pesa ambazo wamekopa ili na wenzao wapate kwenda kujisomea.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ahsante *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii kuchangia wizara hizi mbili Wizara ya Elimu na Afya hasa tukizingatia kwamba bila ya elimu huwezi kusoma utatibu wa afya na ukatibu watu, kwa hivyo mambo mawili yote yanakubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote Mhe. Waziri wa Afya, Naibu wake Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na upande wa Wizara ya Elimu, Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu, Manaibu Katibu wakuu lakini natoa changamoto pekee kusema tu kwamba Wizara ya Elimu naipongeza kwa kuwa na Waziri mwanamke, katibu Mkuu Mwanamke, Naibu Katibu Mkuu Mwanamke, na wakurugenzi wengine lakini nawapongeza kwa usikivu wao na kazi zao wanakwenda vizuri ambao hawana nongwa katika kazi zao.

Lakini pia Wizara ya afya Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kuna Naibu Mkuu Mwanamke hali kadhalika na wao tuwape kweli yao wanafanya kazi vizuri ndio mafanikio haya tunayopata tukampongeza Mhe. Rais kwa kazi zao nzuri kusimamia.

Mhe. Mwenyekiti, niseme katika nafasi yangu kwamba naipongeza Wizara ya Afya tumpongeze Mhe. Rais lakini binaadamu tulivyoumbwa ufanye zuri mara elfu moja watu hawathubutu kusimama wakakusifu, lakini ikitokea bahati kosa dogo tu maelfu au malaki ya watu watakulaani lakini aliyoyafanya Rais yako wazi na yanaonekana mimi nitasema kwa ufupi sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukiacha hospitali kuu ya Mnazi mmoja kitengo cha mama wajawazito na watoto. Mheshimiwa naipongeza sana serikali kupitia wizara ya Afya na tunampongeza sana Mhe. Rais kwa kazi yake nzuri aliyoifanya. Yoyote aliyeondoka nchini kwa miaka mitano au kumi akija hapa atapotea. Hadhi ya hospitali ile sasa inaonekana. Mimi nimekwenda kwa ujanja wangu wote niliotumia ili kupata kujua baya na zuri, lakini wanafanya kazi kwa uwadilifu sana katika mama mjamzito na watoto hospitali mpya. Mhe. Waziri niseme tu kwamba hapa pahala pamefanyika kazi nzuri lakini tunataka uendelevu ule uendelee kuonekana.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika hospitali ya Mnazimmoja mimi naungana kwamba sheria tumepitisha kuwa hospitali ya Rufaa sina pingamizi na hilo. Lakini nataka niseme na nimuombe Mhe. Waziri bado kuna matatizo yaliyojitokeza katika hospitali yetu hii na nyenginezo. Leo unakwenda hospitali unataka kupima damu anaambiwa kipimo kibovu, kina matatizo ya hapa na pale. Nimwambie Mhe. Waziri tunamuomba atusikilize sana, tunasema kwamba Mapinduzi Kongwe ukenda kupima wingi wa damu unaambiwa mashine mbovu, hapa pembeni yupo mwengine kawekwa au kakaa kwa ujanja gani? Hatujui lakini anapima watu kwa sh. 3000/ na ushahidi upo.

Tumuombe Mhe. Waziri hili aliangalie na tupate jibu zuri kwa nini inakuwa hivyo. Nashangaa ukenda kupima *pressure* au unakwenda kwenye *X-ray* unaambiwa mashine mbovu, lakini unaambiwa nenda Altabibu au nenda hospitali gani. Yaani Hospitali Kuu tunayoitegemea *X-ray* mbovu hamna ni aibu, tunamuomba Mheshimiwa hili aliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema Rais kazi yake moja kukuteuwa wewe na kukupa majukumu. lakini majukumu yale unakula kiapo kwa msahafu kama mwanajeshi, kwa hivyo unatakiwa kazi yako pale uwe muwadilifu katika shughuli zile. Wasimamizi wetu bado waangaliwe wengine hawapo sawa, hilo naliomba sana Mhe. Waziri.

Jengine Mheshimiwa kuna utata wa kubakwa watoto wetu na kuwatorosha na kudhalilishwa, akina mama na akina baba na wao wamo wanajishirikisha na masuala haya. Hichi chombo cha DNA Mheshimiwa hebu naomba Wizara ya Afya utupe jibu kina uzwa bei gani na kinapatikana kwa namna gani. Kwani imekuwa ni adha kubwa anayekwenda kubakwa akenda kule anaambiwa matokeo hayapatikani kutokana na kutokuwepo kwa chombo cha DNA kama kingekuwepo basi dakika tano nyingi umeshayapata. Tuiyombe serikali kupitia Wizara ya Afya hata Mhe. Rais, Mwenyezi Mungu akitujaalia tukikutana naye tutamuomba kama Baraza DNA chombo hichi kitafutwe kwa usalama wa watoto wetu. Madaktari, mapolisi, waendesha mashtaka wanapata tabu kwa chombo hichi kuwa hakipo. Kwa hivyo niiyombe serikali hili liwepo.

Lakini jengine Mheshimiwa niseme tu kwamba jambo kubwa ambalo tunataka kulisema sasa hivi tunamuomba sana Mhe. Waziri awe mtu ambaye anavamia katika baadhi ya maeneo na kama anapata lalamiko kwa Mwakilishi au mtu yeyote asiwe anakataa moja kwa moja atafute rai za kufatilia kwa ujenja ili yagundulikane yale maovu yanayotokea. Mheshimiwa kuna siri nyingi mimi ningemuomba au ningeiyomba Kamati nitaipongeza baadaye kama imefanya kazi nzuri sana.

Tuna taasisi za binafsi au za serikali kama JWTZ, KMKM na kwengineko kana utakwenda katika JWTZ unafika kule Bububu unanyenyekewa mgonjwa, unaangaliwa, yaani unabembelezwa, sema kinachokusibu mpaka unakipata. Niombe tufate tabia hiyo njema ambayo tunataka wananchi wetu wafanye vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye elimu nakwenda opesi opesi najua muda wenyewe mdogo. Kwenye Wizara ya Elimu nimpongeze Mhe. Waziri kama nilivyowapongeza mwanzo kazi zao nzuri, zinaendelea vizuri na mimi kwa upande wangu nasema binaadamu asiye na shukurani huwa si binaadamu huyo. Nampongeza kwa kupata skuli mpya Kwarara, skuli ya kileo, kuna mambo yote ya kitaalamu ya kileo, *electronic* tupu, kuna televisheni, kuna kituo cha redio cha watoto tucheze, lakini nimpongeze zaidi kwa hivi sasa hivi tuna maangalizi ya kutengeneza msingi pale pale kwa hivyo niipongeze Wizara kwa hilo.

Kubwa ninalotaka kulisema kwamba Rais wetu kwa kauli yake njema haya yote anayoyafanya anatangaza mambo yote bure, elimu bure, kuanzia msingi mpaka sekondari, lakini tunaambiwa kuna malipo mengine wananchi wanalalamika hebu waeleze una Wizara haya malipo ya kwamba watu watoe elfu ishini, huyu atoe elfu thalathini huyu hamsini inakuwaje. Hebu labda chombo hiki kikitoa kauli tutasikia na wananchi wataelewa kwamba kuna mchango huu uwe hivi na mwengine uwe hivyo.

La mwisho Mheshimiwa kabla hujanipigia honi, nataka kusema kwamba kuna bahati mbaya baadhi ya skuli zetu na hizo zipo Wilaya ya Mjini nazisitiri jina sizitaji akitaka ushahidi Mhe. Waziri na Wizara nzima nipo tayari kuwambia pahala fulani na wenyewe watakuwa wanasikia huko, watoto wanaochelewa kufika skuli, si vyema kuchelewa mimi sipendi lakini ni binaadamu kila mmoja na uwezo wake mwengine anatoka Kwerekwe anakwenda mjini shilingi mia moja hana na usumbufu wa daladala zetu tunaujua mfano anakwenda Rahaleo akifika pale kama kachelewa anaambiwa ulipe shilingi mia tatu au huingii ndani ya darasa. Au ale bakora mpaka zimkolee ndiyo aingie kwenye darasa au akishindwa kama kakataa kupigwa bakora anaambiwa nenda kwenu.

Mhe. Mwenyekiti, hili lipo na mimi huwa napenda kusema kweli kwa sababu hii kweli kesho nitaikuta mbele ya haki, hao waliosema wapo na kama ushahidi huu anausikia nafikiri watanibeba baadaye kwa furaha. Kwa hivyo watoto tuwafikirie mengi, mimi nina uwezo wa kumpa mtoto wangu shilingi elfu mbili au mia tatu au mia mbili lakini kuna mzee mwengine anatoka nyumbani kwake shilingi mia moja uwezo huwo hana. Kwa hivyo naiyomba Wizara inapotokea kadhia kama hii tuifanyie kazi ili kuhakikisha kwamba watoto wale wawiyane sawa sawa.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa kuokoa muda niseme tu kwamba nazipongeza wizara zote mbili, nawapongeza mawaziri, manaibu mawaziri, makatibu wakuu, Naibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi, Walimu wakuu pamoja na walimu wote pamoja na wanafunzi na Wizara wa Afya, madaktari, manesi na wauguzi wote kwa kazi zao nzuri wanazozifanya na yale tunayowaeleza watusikilize ili twende sambamba kama azma ya Rais kwamba Afya bure, elimu bure. Nashukuru naunga mkono hoja.

Mhe. Ame Haji Ali: Asante Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kwa sababu dakika zenyewe ni chache sana. Nianze na Wizara ya Afya, kwanza nawapongeza sana watendaji wote wa Wizara ya Afya nianze na Waziri kwa kazi kubwa na ngumu wanayokabiliana nayo. Licha ya kuwapongeza pia niwape pole. Kwa kweli mzigo wao ni mkubwa mno na kwa bahati ukifanya ziara ya kutembea katika vituo ndipo utakapojionea hiyo hali na uzito wa ukubwa wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na hospitali ya Kivunge nianze hapo. Hospitali ya Kivunge awali ilitegemewa kwamba ihudumie watu katika shehia saba baadae ikawa hospitali ya Wilaya. Lakini nataka niwambie wizara kwa sasa hospitali ya kivunje ni hospitali ya Mkoa, kwa hiyo Mkoa mzima wa Kaskazini unaitegemea hospitali ya Kivunge. Naiyomba sana Wizara ilitizame jambo hilo iwapatie huduma na vifaa vinavyostahiki ili kwa ajili ya kuhudumia Mkoa mzima wa Kaskazini.

Nitoke hapo kwa haraka haraka niende katika hospitali zangu mbili niziguse katika jimbo la Nungwi. Kwanza ninze na hospitali yaani kitua cha Afya cha pale Tazari. Mhe. Naibu Waziri wewe ni shahidi nimekwenda na wewe kile kituo kinavuja sana. Katika masika haya yajayo nazani huduma pale zitashinda kutolewa. Naiyomba sana Wizara ilitizame jambo hili. Sambamba na hilo kuna kituo chengine pale kidogo nacho sasa hivi milango yake imeshamaliza kubugujwa na mchwa havitafungika vile vituo watu wataendelea kupita ndani. Wizara iliangalie hilo na tuone kwamba tunaweza kuwasaidia vipi.

Niruke kidogo niende katika hospitali ya Chakechake Pemba wenzangu wengi wamesema ubovu wake unakithiri, unatia aibu, haufai kuonekana katika hospitali iliyokuwa katika mji kama ule. Tujitahidini tutafute namna angalau basi tujaribu kulikarabati lile jengo. Lakini sambamba na hayo katika hospitali ile tulikutana na kadhia moja kubwa pale Chakechake pamoja na konda sijui kama hizi taarifa Wizara wanazo ama laa. Pale katika kituo cha Chakechake tumewakuta wahudumu wa kituo kile pale katika eneo la TB wameambukizwa wao wahudumu ndio wameambukizwa. Kwa hiyo tukapewa taarifa pale kuna watu watatu kituo cha Konde pana watu kama saba wao wenyewe wahudumu wamepata maambukizo. Sasa katika hali ya kawaida kama wahudumu wapo katika hivyo, tunaiomba wizara sijui wale wametizamwa katika misingi gani na wakarudishwa katika hali ili sasa wasijewakavunjika moyo katika kuwahudumia wananchi wetu. Hilo nalo tumelipata katika ziara yetu, naomba sana Wizara nayo ilifanyie kazi ili ilitizame kwa upana wake.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nataka niende nalo kwa haraka haraka najitahidi nao ni uhaba mkubwa wa madaktari katika vituo vyetu vyote. Ni ukweli usiofichika Wizara inajitahidi lakini bado tunaupungufu mkubwa wa madaktari. Katika hili mimi labda nichukue nafasi ya makusudi kabisa kuiomba serikali tuwaoneeni huruma watu wa Wizara ya Afya, Kweli vituo tumejitahidi kufungua lakini madaktari hakuna. Wakati mwengine unaweza ukafika mahali ukawalaumu wauguzi, wakati mwengine wauguzi hawa wanafanya kazi mpaka mtu anachoka. Kahudumia watu mpaka kachoka, wanaokuja sasa huku usitegemee kwamba atawahudumia vizuri zaidi ya kuwapa lugha mbaya. Tusaidieni sana Wizara tupate madaktari wa kutosha ili sasa Wauguzi hawa wakifanya vibaya tuwalaumu, lakini mimi nahisi kwamba miongoni mwa tatizo ni ule uhaba wao. Sasa mtu kafanya kazi mpaka kachoka anaweza sasa akakujibu lugha yoyote kutokana na ile kuchoka yake. Mimi naiyomba sana serikali tulitizame katika jambo hili ili na wao tuweze kuwapa msaada unaostahiki.

Lakini la tano niende haraka sana na nazipongeza sana hospitali binafsi. Hospitali binafsi zimekuwa zikitoa mchango mkubwa kuwahudumia watu wetu nao nawapongeza. Muhimu katika hili ni lazima watambue kwamba wao ni sekta ya huduma sio ya biashara. Wajitahidi na watambue kwamba watu wanaokwenda pale hawaendi kwa ajili ya biashara wanakwenda kwa ajili ya huduma basi vituo vyetu hivi tuvisaidie kila hali ili waweze kuwasaidia wananchi wetu katika kuwapatia huduma na isiwe ni katika maeneo ya biashara.

Niruke niende hara hara katika Wizara ya Elimu kwa sababu ya muda kabla Mwenyekiti hujanigongea. Kwanza niwashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Elimu nianze Mawaziri, Manaibu Waziri na watendaji wote, wametupa ushirikiano wa kutosha katika kazi zetu za Kamati. Shukurani zangu na pongezi za zaidi ni kwa Wizara hii pale niliposimama kwenye Bajeti na nikawaomba katika bajeti yao ya mwaka huu wanimalizie madarasa yangu manne pale Bwereu, nawashukuru sana kwa juhudi zao na kukubali ombi langu lile. Mhe. Waziri kwa taarifa yako ile skuli sasa imeshatiwa rangi nzuri, bado kuna ahadi hujazikamilisha pale naomba nazo zikamilishwe ili iweze kuwa vizuri zaidi. Nawashukuru sana na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Nungwi hizi pongezi nawapeni kwa kazi kubwa ambayo imefanyika pale.

Mchango wangu mwengine haelekeza huku katika Elimu, katika matembezi haya ya kuvitembelea vituo hivi, tumegundua jambo ambalo hili sasa Weheshimiwa naomba sasa sote

kwa pamoja tulichukueni. Miongoni mwa matatizo tuliyoyagundua ya wanafunzi kufanya vibaya ni ufinyu wa nafasi za kukaa madarasani. Madarasa yetu hasa ya *nursery* na msingi watoto wengi mno. Darasa moja lina watoto mia moja na kuendelea lina mwalimu mmoja, hawezi kusomesha hata angekuwa na ujuzi wa aina gani.

Mimi natoa wito kwetu sisi Wawakilishi tuanze toke leo twende tukazungumze na Kamati zetu za kule ambazo zinahudumiwa na wazazi wenyewe, kama tunataka matokeo mazuri ya watoto wetu ni lazima tujenge mabanda ya kutosha ili wanafunzi hawa waingie kwa nafasi, wawe na nafasi za kutosha halafu tuiombe serikali itupatie walimu wa kutosha. Lakini vyenginevyo katika sura ya watu mia moja katika darasa linalosomeshwa na mtu mmoja msitegemee miujiza, walimu huwa hawawafikii wanafunzi hawa. Na bahati mbaya sana haya yanaanza kule kwenye msingi tokea *nursery* tusiwategemee wanafunzi katika misingi hii kuja kurudi wakaingia katika sekondari katika matokeo mazuri.

Sambamba na hilo niende katika vyuo vituo vya uwalimu TC tunaishukuru serikali lakini naiyomba sana wizara iwaongezee nguvu hawana usafiri, hawana watendaji wa kutosha, mambo mengi katika hivi vituo tuvisaidieni, vitatusaidia sana katika kuwaweka sawa wanafunzi wetu.

Suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala zima kama nilivyotangulia kusema mimi niiyombe serikali kwa dhati kabisa ya moyo wangu kwamba tuziangalie Wizara mbili hizi kwa jicho la huruma sana, Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya. Jamani hawa wana majukumu makubwa na wanakabiliwa na kazi kubwa sana kwa makusudi kabisa. Naiyomba serikali tuwaongezeeni bajeti yao katika mwaka ujao, ili sasa waende kule chini wakatatue changamoto, jamani kuna changamoto nyingi kule chini. Lakini tutakaa hapa tutawalaumu wakati kumbe mfuko wao hautoshi. Mimi nitoe mfano mmoja katika hapo, Mhe. Rais alitangaza kwamba akina mama wote watibiwe bure hasa katika maeneo ya uzazi lakini unafika mahali mipira ile ya elfu tatu hayapo hospitali, sasa anafanyaje daktari, inabidi amwambie mgojwa mwenyewe aende akatafute. Nia safi na madhumuni makubwa ilikuwa ni kuhudumia watu wetu lakini jamani uwezo wa serikali tujitahidini bajeti za Wizara mbili hizi tuziongezeni ili tuweze kuwahudumia watoto wetu vizuri kule chini.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kwa sababu nilishiriki katika kuiandaa. Kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Nungwi ninaowaongoza tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Asante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Asante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa, lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru hii kwa kunipatia na mimi nafasi hii nikaweza kusema machache katika Wizara zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kama walivyotangulia wenzangu kusema kumpongeza sana Mhe. Rais Dkt Ali Muhammed Shein kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameweza kuzipa Wizara hizi mbili kipaumbe na ndio Wizara kweli kubwa, Wizara zenye majukumu mengi. Tunamshukuru Rais kwa uwoni wake, kwa sababu Wizara ya Elimu ni muhimu sana na Wizara ya Afya ni muhimu sana. Huwezi wewe kwenda kusoma kama huna

afya njema, na huwezi kuwa na afya njema kama hakuna daktari aliyesomeshwa na mwalimu. Kwa hitu viwili hivi vinategemeana kwa hivyo Wizara hizi ni muhimu sana na niombe tu Waheshimiwa wenzangu tuchukue juhudi za makusudi kumuunga mkono Mhe. Rais wetu kwa juhudi hizi kubwa ambazo anazichukuwa kuendeleza suala zima la elimu na afya. Tukiweza katika mambo mawili haya basi nadhani mengine yatakuwa ni mtiririko kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika sekta ya Afya ambapo katika ripoti ya Kamati imeonyesha kuna wafanyakazi 95 ambao wamestaafu kazi lakini hakuna wengine walioajiriwa katika nafazi hizo. Ripoti hii imeonyesha mapungufu mengi ya wafanyakazi katika sekta hii ya afya. Lakini nilipoona hizi nafasi zipo na tayari hapa uwajiri umeshafanyika labda nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja atwambie ni kwa nini nafasi hizi hazikuweza kujazwa na zipo tayari uajiri wake ili kuweza kupunguza yale makali ya wafanyakazi ambao wamekosekana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende katika hospitali ya Wete ambayo ina kilio kikubwa cha upungufu wa wafanyakazi ambapo kunaonekana hapa vifaa vipo vya kufanyia kazi jambo ambalo linakosekana katika hospitali nyengine, lakini wao vifaa wanavyo lakini wafanyakazi wa kuhudumia vifaa hivyo hakuna. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana Mhe. Waziri atakapokuja atupe ufumbuzi juu ya tatizo hili kwa sababu hapa pia ripoti imetuonesha kama Wizara inafanya juhudi ya kupeleka wafanyakazi katika kituo hiki. Lakini kuna watu ambao kwa makusudi wanapiga juhudi za Wizara kuona wafanyakazi wakipelekwa basi wao wanawapa uhamisho kuwarudisha huku Unguja. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hapa inaonekana kuna mchezo fulani unafanyika, kwa hivyo Mhe. Waziri utakapokuja hebu tupatie mafahamisho mazuri kuhusu suala hili la kwa nini au kuna mtu mwengine zaidi yako wewe, kwa sababu mimi ninajua Wizara ya Afya kiongozi wao mkuu atakuwa ni Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu.

Sasa tunapoambiwa kuna viongozi wengine ambao wanaweza kutoa maamuzi hayo basi lazima tunataka ufumbuzi huu tuujue, au hayo ndio majibu yanayotajwa basi pia vile vile tuelewe. Kwa sababu Kituo cha Afya kama hiki maisha ya watu yanaweza kupotea kwa kukosa wafanyakazi ambao wamekosekana pale na pia inaonekana kuna upungufu katika kituo ambacho wauguzi wale katika sehemu ya upasuaji, kuna muuguzi mmoja, Mheshimiwa hii ni hatari kwa kweli lazima suala hili tulipiganie kwa juhudi zetu zote kuunga mkono yale mawazo ya Mhe. Rais wetu anayotaka kwamba wananchi wake waweze kuwa na afya njema katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika sekta hii ya afya katika hospitali ya Kivunge ambapo kunaonekana kuna wafanyakazi 80 lakini wapo katika nyumba 12, hili ni tatizo na tunajiuliza maswali hapa watu hawa wanaishi ishi vipi. Lakini niiombe tu Serikali iweze kuchukua juhudi ya kujenga vituo hivi ili madaktari wetu hawa waweze kufanya kazi zao kwa utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, pia ripoti katika hospitali nyingi ambazo wenzetu wamefanikiwa kuzitembelea wana kamati wameonesha kuna malalamiko ya kukosekan fedha za likizo kwa wafanyakazi na imeonesha pia kama kuna baadhi ya wafanyakazi hawajawahi kupata hata mara moja hizo fedha za likizo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akija pia hili tupatie ufumbuzi wake.

Nije katika kituo cha Hospitali ya Muembeladu ambapo kuna wajumbe wenzangu pia wameshalichangia suala hili na mimi kwa umuhimu wake naomba niongeze kulichangia. Mhe.

Mwenyekiti, kituo cha daladala kiliopo pale kwa kweli kile kituo kinasumbua san asana. Mhe. Mwenyekiti, hakuna asielewa katika suala la uzazi mjamzito anapoletwa katika kituo pale anakimbizwa kuahishwa na inategemea hali ya mzazi inavyokuwa kunakuwa mtu anaumwa tu uzazi lakini kuna wengine wanakuja wana hali mbaya kabisa. Kwa hivyo wanawahishwa katika hospitali sasa kuja akakumbana na msongamano wa magari si jambo la busara, tunaiomba sana Serikali ifikirie juu ya kukiondoa kituo hiki ikizingatia uwepo wetu sisi hapa umetokana na mama ambaye alibeba ujauzito na akaweza kutuzaa sisi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kituo cha Makunduchi, hapa pia Kamati ilipotembelea ilikuta kuna ujenzi wa nyumba ya madaktari lakini pia mafundi hayo wanadai fedha milioni tatu na laki saba. Mhe. Mwenyekiti niombe tu Wizara au niiombe Serikali iwafikirie watu wetu hawa huwa wana wafanyakazi kwa kujitolea sana. Kwa hivyo sasa pale wanapochukua juhudi ya kuja kupoteza muda pale kwa kufanya juhudi ya kusaidia Serikali yao, basi kile ambacho tumewapangia kuwapa tuwape ili kiweze na wao kuwasaidia na familia zao.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika sekta ya elimu kwenye program ya Skuli za Maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, niishukuru na niipongeze Wizara kwa juhudi zake lakini pia niseme yale mapungufu ambayo yalikutikana katika vituo vyetu hivi. Kwanza kabisa katika Skuli za Maandalizi kumeonekana changamoto ya uchakavu mkubwa wa majengo na skuli hizi tuelewe wanaosoma pale ni watoto wetu wadogo sana. Kwa hivyo walihitaji kupata miundombinu mizuri wakaweza kusoma katika mahala pazuri, mengine majengo yapo katika hali ya hatari, kwa hivyo ni suala Serikali iweze kuzingatia.

Pia kuna ruzuku ambayo mlikuwa mkiitoa nipongeze kwa juhudi hizo lakini ruzuku hii inaonekana bado ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji. Nimuombe Mhe. Waziri hali ikiruhusu basi waongezee kidogo ili na wao waweze kusoma katika njia nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna *program* ya ubora wa elimu. Mhe. Mwenyekiti, ubora wa elimu huwa unatokana na vituo vya walimu wetu ambavyo wanapata mafunzo mbali ili kuweza kuendeleza kazi zao. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ndani ya vituo hivi huwa vinakosekana fedha za kuendeshea shughuli zao na hao hawa ndio walimu tunaowategemea waweze kupata mafunzo ili waweze wakafanye kazi zao katika kiwango kizuri.

Mhe. Mwenyekiti, fedha zilikuwa zikipatikana kupitia michango lakini pia tunamshukuru Mhe. Mwenyewe Dr. Shein kwa kuzuia michango hii kuna aweze kuwasaidia wanyonge ili watoto wa kinyonge waweze kusoma. Sasa niiombe Serikali iweze kufikiria mikakati mbali mbali itakayosaidia vituo hivi kupatiwa fedha kwa lengo la kuviendesha vituo hivi viweze kufanya kazi zake kama inavyohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa lakini ningependa haya ambayo nimechangia basi Mhe.Waziri aweze kutupatia majibu yaliyokuwa sahihi kwa manufaa ya afya na elimu za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nichukuwe fursa hii basi kumpongeza sana Mwenyekiti, wa Kamati hii na wajumbe wake wote. Kwa kweli kazi walioifanya kubwa nzuri inapendeza na Mwenyezi Mungu inshaallah sote kwa kuwa nia yetu ni moja basi Mwenyezi

Mungu aweze kutusaidia juu ya kuzifanyia kazi changamoto hizi ambazo tunazipata ili nchi yetu iweze kuendelea katika hali nzuri pamoja na wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja ripoti hii ya ustawi wa jamii. (*Makofi*)

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kuniwezesha jioni hii kuhudhuria katika kikao hiki, pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kwa kuchangia ripoti ya Ustawi wa Jamii. Kwa kuwa kama hivyo nitakwenda chap chap.

Lakini kwanza nataka nianze na wakala wa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Katika ripoti nimeona taarifa kwamba stahiki za Mkemia Mkuu hazilingani na hadhi yake. Kwanza tumshukuru Mungu sana kwa kutubarikia wataalam wa fani mbali mbali hapa Zanzibar. Hapa Zanzibar tumebarikiwa na wataalam wa kila fani. Kama hivyo ndivyo tuna wajibu sisi kuwaenzi vizuri kama inavyostahiki, kwamba tunapowaenzi wataalam wetu tutamia gharama ndogo kwa kutufanyia kazi kubwa. Lakini endapo hatutowaangalia kwa jicho la huruma tutashtukia kwamba tutapata gharama kubwa kwa kutafuta wataalam ambao kazi yao itakuwa ni ndogo mno kulingana na gharama tutakayoitoa kwa wao.

Vile vile tunaweza kupata *damage* ya hata kukimbia wataalam wetu wakenda kufaidisha nchi nyengine. Nchi yetu inawagharamia wataalam kwa kwenda masomoni nchi za nje kwa gharama kubwa, lakini za kusikitisha kwamba kuna taarifa huku kuna wafanyakazi wawili walipokwenda masomoni mpaka leo hawajarudi na wameshamaliza muda wao wa masomo, ambapo hao walisomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa gharama zote wakalipiwa kila kitu. Sasa hii inafahamisha kwamba baadhi ya wafanyakazi hawafanyi kazi kwa ajili ya moyo safi wa nchi yao. Mfanyakazi hawezi akatoroka akenda masomoni halafu akabakia huko huko ikiwa yeye anaipenda nchi yake. Kwa maana hiyo hapo tunapata picha kwamba wafanyakazi watakaopelekwa masomoni Ng'ambo wende kwa masharti maalum na yakikosekana masharti hayo wafuatwe huko huko waliko waje hapa. Kwa sababu wapewa nafasi hiyo wamekoseshwa nafasi watu wengine ambao ni waaminifu wapenzi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tunapowapeleka wafanyakazi wetu nchi za nje kwenda masomoni tuwalipie kwa sababu unapokwenda kuhoji katika Taasisi fulani utaambiwa hapa kuna wafanyakazi 10 wapo masomoni nje lakini wanajilipia wenyewe. Sasa wewe unampeleka mfanyakazi anajilipia mwenyewe unategemeaje, wewe hujamdhibiti, ili tuwadhibiti tuwapeleke kule kwa kusomeshwa na Serikali yao hapo bila shaka itakuwa tumewadhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Elimu, Programu ya Elimu ya Sekondari. Kwanza hapa nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, nimpongeze Naibu Waziri wa Elimu, nimpongeze Katibu Mkuu, nimpongeze Naibu Katibu Mkuu, niwapongeze Makamishna pamoja na Afisa Mdhamini ambao wote wanafanya kazi kwa umoja na wanafanya kazi kwa kujituma na wanafanya kazi bila ya woga tunawashuhudia hawalali hao ili kuiboresha elimu Zanzibar na kuwaboresha wanafunzi wetu. Pamoja na kwamba wakati mwengine hupapurana papurana humu na Waziri au Naibu Waziri tukaona kama hatendi haki lakini hawalali hao kwa ajili ya kuboresha mafanikio ya elimu Zanzibar.

Lakini tukumbuke kwamba siku moja kasa anaambiwa kasa mbona huchezi wote wenzangu wanacheza wewe umekaa tu na wewe ndio mkubwa, wenzako wanatoka kijasho wewe mbona huchezi anasema nacheza lakini gamba ni gumu. Mhe.Waziri pamoja na Naibu wake wanacheza lakini gamba ni gumu. Kwa maana hiyo…..

(Hapa hapakuwa na rekodi kwa muda mfupi)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa sio uanze umalizie. Mhe. Said Omar Said Karatu kama ulivyonitaka kuwa uanze mwanzo kumbe uanze mwanzo kweli kwasababu yale uliyoyazungumza yote hayapo kwenye *hansard* kwa hio kama uanze, uanze mwanzo kweli na nitakulinda na dakika zako hapo utakapoanzia na vizuri umeenda kwenye nafasi nyengine ambayo mchango wako utaingia kwenye *hansard* kwa hiyo nimekuruhusu uanze mwanzo. *(Makofi)*

Mhe. Said Omar Said Karatu: Ahsante sana Mwenyekiti kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu Jallah Subhana Wataallah kwa kuniwezesha kufika katika kikao hiki jioni hii pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya ustawi wa jamii kwa kunusuru muda naomba nianze na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ndani ya ripoti imetwambia kwamba stahiki za Mkemia Mkuu haziendani na hadhi yake, naye ni mtalamu na mtalamu lazima mambo yote yawe ya kitalamu mpaka maslahi yake yende kitalamu yeye yuko peke yake hafanani na wengine kwa hiyo kwa mambo yote lazima yeye awe ni bora kwa ufanisi na kwa maslahi kutoka Serikalini.

Katika taarifa vile vile inasema kwamba kuna wafanyakazi wawili ambao walipelekwa Ng'ambo huku kusoma lakini kwa bahati mbaya hadi leo hawajarudi na wameshamaliza masomo yao ina maana wameshatoroka Zanzibar na wale walipelekwa kule kwa fedha za Wazanzibari ili warejee huku wawasaidie Wazanzibari waliowapeleka kule, hasa hawa Serikali ikawatafute popote waje huku.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti ningeishauri Serikali kwamba inapopeleka wafanyakazi kusoma iwagharamie kwasababu kama haitawagharimia itakuwa haijawadhibiti kama wafanyakazi wanakwenda kusoma kujisomea wenyewe tu waweza hata kuamua wasije tena huku, wala huna utawafanyaje lakini jee umekwenda kuwasomesha kwa mali ya umma lazima wailipe wanaweza wakenda wakachukuliwa walipo wakaja hapa kwa niaba ya Wazanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, chapuchapu nende katika Wizara ya Elimu *program* ya elimu ya sekondari hapa kwenye ripoti tumeambiwa kwamba walimu ni haba mno na ni kwenli kabisa walimu ni haba walimu ni haba kuanzia *primary*, *secondary* na kuendelea pamoja na kwamba ukiwaona walimu kwenye kiwanja utaona kama walimu ni wengi lakini walimu si wengi, kutokana na ule muundo wa kielimu walimu utakuta ni wengi lakini si wengi kila siku wanahitaji kuongezwa nimshukuru hapa Mhe. Waziri wa Elimu, Mhe. Naibu Waziri walimu, Katibu Mkuu, Mkurugenzi, Kamishna pamoja na Afisa Mdhamini ambao wanaofanya kazi kwa kujituma wanafanya kazi kwa umoja na wanafanya kazi kizalendo hao tunaowaona kila pembe pamoja na kwamba sisi wakati mwengine hushambulia shambulia sana lakini kama nilivyosema kwamba aliambiwa *kasa huchezii, cheza wenzako wanacheza wewe unakaa tu na wewe ndio mkubwa;*

akasema kwamba nacheza lakini bamba ni ngumu. Kwa hivyo tuiombe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwaajiri walimu tuwache wacheze sasa.

Na katika kuajiri tuzangalie walio waadilifu, walio waaminifu, walio wakweli tusiajiri watu wanao omba ajira tuwaajiri watu watakao ifanyia kazi ajira, wako watu wa aina mbili tukishawapata watu hao hapo Waziri itakuwa haingiwi tena kwasababu ni mfanyakazi kikawaida na Naibu wake wanafanya kazi tutaiona sasa hiyo kazi yao.

Mhe. Mwenyekiti, hapo ndani ya uajiri hapa mara nyingi unapokuja uajiri husikia wanaotakiwa ni watu fani ya sayansi tu sasa tunaomba waajiriwe wa sayansi waajiriwe na *art*, hasi tukisema sis tunawajiri wa sayansi hawa wa *art* wataajiriwa na nani *(Makofi)*

Hatuwezi tukavunja moyo sasa hivi wengi sasa hivi washakata tamaa wenye ma *degree* washakata tamaa kwasababu ikitokea taarifa ni nani ah, watu wa sayansi sisi je, si tumesomeshwa au tumeshomeshwa kwa ajili ya nini na kwanini tukaendelea kusomeshwa kama hatuajiriwi. Mimi ningeomba sana hiyo ajira iangalie pande zote, tujue kwamba kila mmoja ana kiu yake huyu ni mtu wa sayansi huyu ni mtu wa art na kila mmoja anafanya kazi kwa maendeleo ya Taifa kwa ufanisi.

Nikitoka hapo nende katika matokeo ya mtihani tumearifiwa kwenye ripoti kwamba matokeo ya mitihani ya sekondari si mazuri sana kwa sababu gani moja ni sisi wazee kutokuwa na mawasiliano na walimu pamoja na wale wanafunzi endapo mwalimu mzee atakuwa pamoja na mwalimu, atakuwa pamoja na mwanafunzi wanawasiliana kila wakati mwanafunzi atakuwa mzuri mbona. Lakini la pili ni baadhi ya walimu wa sekondari uwezo wao ni mdogo wa kufupisha, uwezo wao ni mdogo utamkuta mtu ana *degree* lakini mimi hapa ningeomba hapa Serikali wakati wa ajira tusiangalie karatasi *degree* hii karatasi si *degree, degree* kichwani *(Makofi).*

Tumfanyie kwanza yule *interview* akifanikiwa tumwambie alete cheti chake tusikubali cheti tu kwani ni wangapi wenye *degree* hawako watu ambao wana *degree* za Muslim lakini hana uwezo wa kusomesha kiarabu darasa la nne hivi itakuwaje. Kuna watu wana *degree* ya sayansi hajui *symbol* ya *water* haijui sasa lazima twende kwa uchunguzi ndio tufanikiwe. *(Makofi)*

Siku moja nilipita sehemu nikasikia mama mmoja aha mtoto wangu keshaliza juzuu thalathini huyu sasa mimi nikashangaa mtoto mdogo kwanza nikenda na safari zangu baadae nikarudi ah nikaja kwa yule mama nasikia nilipopita hapa wasema kuwa huyu keshamaliza juzuu thelathini kumbe keshamaliza juzuu thelathini kwa kuzichana. *(Makofi)*

Hasa ukiambiwa keshamaliza juzuu thelathini wampa hadhi ala kammaliza thelathini kwa kuzichana hasa na sisi huyu ni *degree* ana *degree* gani pengine ana *degree* ya ukaidi tu lazima twende kama wanavyokwenda nchi za wengine anajajiwa yule mtu mwenyewe watu hawatosheki na karatasi anaweza mtu kupata kukuonesha wewe cheti ya *form iv* na yeye alimaliza darasa la nne lazima hapa tuwe makini sana.

Mheshimiwa kwa kuokoa muda na kule katika program ya ubora wa elimu mheshimiwa kwanza ni wapongeze sana walimu washauri wanaofanya kazi *Cheeses* Unguja na Pemba wanafanya

kazi vizuri sana, wanafanyakazi kwa kujituma sana, wanafanyakazi kizalendo. Mheshimiwa pale pamoja na kamba wanafanya kazi kwa wiki moja siku yaani wanafundisha walimu pale kwa wiki moja kwa kila wiki siku mbili siku moja ya kazi na siku moja ya wenyewe wale ya binafsi siku moja ya jumamosi, lakini nataka nikuhakikishe Mhe. Mwenyekiti kwamba watakapo maliza miaka yao kama miwili au mitatu watakuwa na cheti kizuri, wanatakuwa ni watu wanao aminika kabisa pale kutokana na wao wenyewe wanapenda na juhudi za walimu wao waliopo pale TC hiyo mcheza kwao hutunzwa au huangaliwa kwa hivyo naiomba Serikali iwaangalie walimu wale wa TCs pamoja na walimu wanaofundisha walimu vyuo vikuu. Mchezaji taarabu anatunzwa kwa sababu gani, kwa kufurahisha. Je, wale hawafurahishi kama wafurahisha kwanini tusiwatunze, naomba sana tuwatunze walimu wetu walimu washauri walipo pale na walimu wengine wanaofindisha walimu katika vituo vya walimu.

Namalizia programu ya Elimu Mbadala nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuamua kuijenga shule ya Elimu Mbadala katika eneo la Wingwi Pemba. Pale hasa ndipo pahala hasa inapohusika na skuli kama ile Skuli ya Elimu Mbadala kituo kile kitafanya kazi vizuri kwasababu kimewekwa pahala ndipo, kwasababu gani nataka nikuhakikishe Mhe. Mwenyekiti kwamba kwa Pemba hakuna mji ambao una skuli nyingi kuliko Wingwi kwa Pemba nzima kwa hivyo pale kiliwekwa pahala ndipo pale na chuo hiki kitakuwa kinafundisha fani mbali za kiamali kama ushoni, upishi, fundi bomba, umeme na mambo mengine kwa hivyo, naiomba Serikali ipeleke mkono wake wa rehema pale ili tupate vifaa hivyo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti naiunga mkono hoja nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Omar Said Karatu kwa mchango wako sasa nimuite Mhe. Miraji Khamis wa Jimbo la Chumbuni na Mhe. Makame Ali Ussi na Mhe. Bi Hindi ajitayarishe.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii na kamati yake kwa ujumla kwa kazi kubwa sana waloifanya na tumepata ripoti nzuri sana na alitushauri sana tupite zaidi kuiangalia ripoti kwa sababu vitu vyote vimesheheni, lakini niseme tu Mhe. Mwenyekiti yapo baadhi ya mambo mawili matatu na sisi tutayaengeneze ili kusaidiza kamati kwenda kufanya kazi vizuri lakini kwa ujumla pia nimshukuru mchangiaji aliyepita alitoa nasaha nzuri sana pamoja na vionja vingi vya mifano lakini alituasa sana hasa katika sekta ya elimu na kama Waziri wa Elimu na Mwenyekiti wa Kamati mlikuwa mnasikiliza kwa makini moja ya mambo ambayo ametuasa tujitahidi sana kuwandaa walimu bora ambao tutapata ile *delivery* nzuri ya *quality* ambayo tunaihitaji kwa wanafunzi wetu wanaomaliza shule zetu na nasaha zile kinyume chake kama hatujafanya vile tutakuwa tunaandaa *quantity* kila mwaka na namba kubwa ya watu ambao wanatoka shule lakini kichwani hamna kitu na hayo hatuwezi kufikia kama hatujajipanga vizuri kwenye maeneo mengi.

Mojawapo ni eneo pia la ukaguzi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati katika ripoti yake nikiisoma kuna ukaguzi wa walimu inaonekana hakuna ufanisi kwa vile wanakosa usafiri wa kwenda kuwakagua

walimu, mie nafatilia kwa karibu Wizara ya Elimu hii sababu moja hapo pia tunaishi na walimu lakini mfumo wa sasa kwa *inspection* ya walimu hawa ile *basic inspection* si mfumo rafiki sana. Ni mfumo ambao hautufikishi maana wakikwama huku mjini basi ule ufanisi wa kumkagua walimu kiufanisi, kinidhamu za walimu haupatikani sababu muda unakuwa mkubwa walimu hawakaguliwi lakini tukiwa na ukaguzi ambao tuna wakaguzi kiulaya wanafanya kazi kila mwezi walimu wanafikiwa kukaguliwa hakukuwa na shida sasa leo tukirudi katika mfumo tulio nao sasa hatuwezi kutengeneza mazingira mazuri ya kuwakaguza walimu ambao nao kwa kiwango kikubwa tunatakiwa hii kazi ifanyike uhalisiya upatikane lakini pia ufanisi uwepo. Kwa hiyo miye niombe sana katika mazingara hasa na hasa ushauri ulivyotoka kwa mchangiaji wa mwisho amesema kama tumeuzingatia vizuri, eneo hili nalo lina *support* kwa kiasi kikubwa kwa kuonekana ili twende katika hatua nzuri yakusaidia Wizara ya Elimun Mafunzo ya Amali ifike pahala pazuri basi eneo hili tuliboreshe turejeshe utaratibu ambao kwa sasa haupo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa katika eneo hilo hilo katika *program* ya ubora wa elimu. Ukiangalia na ukifuatilia kwa karibu skuli binafsi wanaanza kufundisha *standard one* mpaka *six* kwa Kiingereza, wana mikakati mizuri ya kuwajenga kupitia lugha ya Kiingereza. Lakini skuli zetu zinaanza *standard four* mpaka *six* pale ndio wanapata, sasa ukiwakuta wanafunzi wa *standard six* wanaotoka *private* na wanaotoka katika shule zetu hizi ambazo tunazitegemea za walala hoi kama sisi kina Miraji, unafika pahala ule ubora huukuti, nakwenda kumsomesha katika Skuli ya Fedha uwezo haupo, maana hizi shule ndio za wakwezi na wakulima ambao wamefanya Mapinduzi ya nchi hii.

Sasa mimi nimuombe Mwenyekiti wa Kamati katika moja ambalo la kulizingatia basi wizara ichukue jitihada ya kubadilisha mfumo mzima wa ufundishaji katika eneo hili na ile mitaala yetu basi ianze toka huko chini kwa lugha hii. Kwa sababu wakianza darasa la nne, wakiingia darasa la tano au la sita hawamudu vizuri masomo yao, na masomo yanakuwa mengi na yote yanabadilika isipokuwa Dini na Kiarabu mengine yote yanakuja kwa lugha ngeni. Kwa hivyo, kwa kuwafundisha lugha pale mpaka wakafika darasa la sita wanafanya mitihani ukija ukilinganisha viwango vya hawa ufaulu wao unakuwa mdogo sana. Kwa hivyo, naomba sana shule hizi kama dhamira ya serikali ilivyo, basi na dhamira hiyo hiyo ibadilike katika kuongeza ufanisi na kiwango kizuri cha elimu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini eneo jengine alilizungumzia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati la fedha zile ambazo zinakusanywa za *Skilled Development Levy* alilitolewa ufafanuzi mkubwa fedha hizi zinakusanywa kwa nia safi kabisa yakwenda kuwasaidia wajasiriamali. Leo hii tunatengeneza wajasiriamali, tunatengeneza vyuo wamehamasika lakini hawakutani na msaada wa fedha hizi. Sasa tukifika pahala Serikali hii ya Mapinduzi ikiwa ina nia ya kuwaendeleza hawa fedha ambayo hii sehemu kubwa inatokana na hawa walipa kodi lakini tumeiundia utaratibu au tumeunda mfuko huu kwa malengo maalum, sasa kwa nini yakwame kati, si kila kitu kina utaratibu wake. Sasa hili ikifika pahala nalo kama tunalisubiri mwezi wa Septemba ndio mpaka lije lianze na lipate majibu, lakini uhalisia vijana wetu ndio tutawaweka katika mazingira sio rafiki. Sasa kama nia njema ya serikali ipo katika eneo hili basi tuboreshe na tuone dhamira kamili inafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niungane pia na Mwenyekiti katika eneo la elimu ya maandalizi na msingi alilielezea katika muhtasari wa ripoti yake. Lakini ukiangalia na changamoto ya ripoti

hizi tulizopewa kuna maeneo yanaeleza kuwa ukosefu wa nyumba zile za walimu lakini na miundombinu ya mashule. Mimi nilipita shule moja ya maandalizi hii iliyokuwepo Magomeni, kuna shule pale ya Maandalizi ukienda siku ya mvua inavuja na *hardboard* zake zinataka kuwaangukia walimu. Shule inabeba watoto wachanga kwa maana wadogo maana maandalizi hawaingii watu wa sekondari wakiingia ndio wamesha-*graduate* ndio walimu hao. Leo hii shule ile inayobeba vijana wetu ikija mvua maana yake ukakinge kwa mabeseni hivi haileti picha, haileti heshima. Vijana hawa wanatakiwa waekewe misingi mizuri tokea huku chini, leo wanaanza kusoma kwa tabu katika shule ya maandalizi kama ile, kila pahala unaona shida kweli.

Sasa eneo hilo katika shule ya maandalizi, lakini kuna shule nyengine zina mitihani pia, uko mtihani katika nyumba wanayokaa walimu Jambiani, naamini hili Mhe. Mwenyekiti umeweza kulifikia lakini Mhe. Waziri naamini katika ziara zako umeweza kulifikia, walimu wale wanakaa katika mazingira ya shida sana. Nyumba haziendani na hadhi ya wale walimu, Mhe. Waziri mimi nishukuru sana unatokea uwalimu na mpaka sasa hivi ni mwalimu, na mimi nawatetea sana kwa sababu na huko nyumbani ninae mwalimu. Ninalotaka mazingira haya ya walimu yawe mazingira rafiki, wakitoka mle wawe hawana *assignment* nyengine wanayoifikiria wabakie tu ile kwenda kuwafundisha vijana wetu ili waelewe vizuri. Sasa maeneo haya tujitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine lile la namba ya wanafunzi imezungumzwa hapa na Mwenyekiti wa Kamati yeye kakuta mia, lakini mimi Mhe. Mwenyekiti nakwambia ukirudi tena katika kamati tenda na Kinuni, ukishuka chini ya 250 Kinuni Mwenyekiti njoo unipe unasema sasa hivi mikakati imeendelea labda imekuwa 170, lakini *role* hiyo ndio skuli hizi za Kinuni. Sasa leo mwalimu unamkuta ana watu 200 au 250 mwalimu mmoja kakaa mbele huku na mwalimu mwengine amekaa nyuma, yale maadili hasa ya uchungaji wa wale wanafunzi pia hayapo. Maadili haya kwa namba hii wanachungwa kondoo sio watu, unawafundishaje watu 250 unakwenda mwalimu huyo mmoja kakaa mbele na mwengine yuko nyuma humjui anayesema, wala humjui anayenyamazisha watoto. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba na hili tujaribu sana kufikia pahala kutafuta utaratibu hata kama tena hauwezekani kwa sasa basi washaurini hao wazee waende kwenye *family plan* wasizae sana maana serikali haina uwezo wa kuwasomesha.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niende katika eneo la majengo ya skuli pawe na ukarabati na kuwekwa uzio. Hili naomba nilisemee kwa skuli ya jamaa zangu na ndugu zangu wa Kiwengwa. Tulizungumza juzi katika suala la nyongeza, jitihada Wizara ya Elimu wakasema wanakwenda nayo. Lakini niseme ardhi ile mpaka inajengwa skuli ya Kiwengwa Kairo imeombwa serikalini, fanya maendeleo ya uwepo wa shule pale wananchi wameaza jitihada ya kujenga ile shule anatokea mtu kapewa hati ndani ya hati ya skuli ya Kiwengwa Kairo. Jambo la kusikitisha sana lakini yote kwa yote hapa tulipo hata kama zimetoka hati mbili, hii hati moja kwa ajili ya maendeleo ya jamii, na serikali imeweka wazi kuwa ardhi ni mali ya serikali panapo jambo la kijamii ardhi hizi huelekezwa kwenye jambo la kijamii. Leo mtu serikali sisi tumeifatilia imemwita inamwambia impe eneo jengine la Kipandoni amekataa, futeni tu ile twendeni kwenye maendeleo kama hataki yeye basi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali hii ardhi ni mali yake sasa inakwenda kumbeleleza mtu wakati utaratibu upo sisi tunataka kufanya maendeleo, Skuli ya Kiwengwa tunataka tuchangie ili watu wapate kusoma vizuri anatuzuia yeye mtu mmoja eti kama kaimiliki serikali. Mhe. Waziri na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati naomba eneo hili lishughulikieni ipasavyo ardhi ni mali ya serikali

kwenye mambo ya jamii, futa yale mambo ya kawaida elekeza katika jamii. Mimi nyumba yangu hata ikataka kubomolewa kunataka kujengwa kituo cha afya kabomoweni ndio mambo ya jamii, mimi nitaenda kodi.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke katika eneo hilo sasa niende kwa rafiki yangu Waziri wa Afya.

Mhe. Mwenyekiti, hapa sina mengi hata huna haja ya kunipigia kengele namalizia tu maana pale napita njia huko kote kushakwenda vizuri. Mhe. Waziri wa Afya katika eneo lako kwenye ripoti hii kuna maeneo yametajwa baadhi ya hospitali zako ikiwemo hospitali ya Wete inaonekana hapa kuna watu wanahamishwa hamishwa. Lakini mimi nina jambo moja ambalo katika sura ya kawaida hivi unaweza ukasikia kitu ambacho baadae kufanya kazi kwake ukaja ukawauliza wenzako.

Kuna wizi ulitokea mwaka jana 2016 vifaa tiba na mablanketi yaliibiwa, lakini dhamana wa stoo akahamishwa akapelekwa eneo jengine ndio *penalty* yake, kahamishwa wizara nyengine lakini wapo wafanyakazi wakaambiwa wachangie huduma hizo za upotevu wa vile vifaa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri hili nalo halisubiri Septemba tunataka zile hatua za utekelezaji alau kwa wale watu tumefanyaje katika eneo hili, tupate tu basi ile *highlight* kweli hili tendo lilitokea na huyu aliyehamishwa kwa nini ahamishwe kwanza kabla ya zile adhabu nyengine hazijamkutia na kama kapewa ni ipi? Lakini unapotokea wizi pahala kuna vitu vingi, kitu kimoja kuvunjwa katika lile eneo lakini ripoti zilivyo yule mtu kama kenda kufungua lile eneo kafungua mlango kachukua vitu katoka tu hakujavunjwa. Hebu Mhe. Waziri hili na Mwenyekiti tuone tunaishughulikia ripoti hii tunakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie na huko huko katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Kipindi kirefu tulikuwa tunalisemea lile eneo la matatizo ya hisia. Si kauli nzuri kusema vile vichwa maji lakini Mhe. Waziri ameshanifahamu sasa nataka kutumia neno ambalo ni rafiki lile la kitiba tiba lile sijalipata. Lakini eneo hili mara nyingi tunapata madaktari kutoka nje wanakuja wiki au tatu wanaondoka, lakini wakifanya ule upasuaji ile dhima ya yule mgonjwa ambaye amefanyiwa upasuaji wakiondoka wao likitokea tatizo tunawapelewa wapi. Mpaka sasa Mhe. Waziri hebu ukija utwambie kama jitihada za serikali ku-*cover* eneo lile kutafuta mtaalamu imefikia hatua gani?

Sasa baada ya hayo mimi naomba sana nimalizie kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa wizara zote mbili hizi, watendaji wa wizara hizi lakini shukurani za pekee zije kwako Mhe. Mwenyekiti, kazi umefanya nzuri na wajumbe wako nawapongeza sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji ni wengi waliobaki na muda hatuna kwa hiyo nilikuwa nawaomba sana waheshimiwa ambao sikuwataja basi wapeleke michango yao kwa maandishi. Nawaomba sana.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii pengine ya mwisho yakuwa mmoja kati ya wachangiaji wa ripoti yetu hii inayowasilishwa sasa hivi.

Kwanza kabisa napenda niwapongeze sana, sana wana kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya na hususan Mwenyekiti ambapo amewasilisha ripoti yake kwa mbwembwe sana akiwa na uhakika kwamba aliyoyaandika ni sahihi na sisi tunamuunga mkono kwamba ni sahihi. Pia napenda niwapongeze sana wizara hizi mbili husika zilizokaguliwa kwa kutoa au kujibu masuali yaliyokuwa yameulizwa na kuwezesha kuandika ripoti hii ambayo ni nzuri.

Kwanza kabisa niende kwenye jambo la *hansard*. Leo tarehe 24/02/2017 katika ratiba ya mkutano wa tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi inaonesha kwamba itawasilishwaRipoti ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Lakini tukienda huku kwenye utangulizi wa ripoti hii imesema imekaguwa wizara mbili, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa nimejaribu sana kuitafuta wizara hii inayohusiana na wanawake haipo, sasa inawezekana itakaguliwa baadae hili nimelileta kutanabahisha tu kwamba hii ratiba inasema kuna wanawake na huku kwenye kitabu hiki hakuna ripoti ya wanawake. Ni hilo tu ambalo nilitaka kulizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza baada ya kutoa pongezi naanza na Wizara ya Afya.

Wizara hii ni wizara mlezi, ni wizara mama, miongoni mwa shughuli nyingi sana za Wizara hii ya Afya ni kukinga, kutibu na ikiwezekana kuondosha kabisa matatizo ya maradhi na magonjwa ya aina zote ili kuwa na jamii yenye afya na nguvu ya kuleta maendeleo. Sasa wizara hii pamoja na kazi zake kubwa hizo inakabiliwa na changamoto. Nasema haya niliyoyachukua ni mawazo ambayo nimeyapata kwenye kitabu na pengine yamo, pengine mengine yatakuwa hayamo lakini yote yanalenga kwenye lengo moja la kuweka sawa mambo yetu ili safari yetu ya kwenda kwenye maendeleo tuweze kufika kwa haraka na kwa usahihi.

Mhe. Mwenyekiti, hii wizara inakabiliwa na changamoto za kuibuka kwa kiwango kikubwa cha magonjwa ya sukari, *pressure*, ukimwi na kadhalika. Na hivi sasa basi duniani huko kuna maradhi yaliyojitokeza kwa mfano kuna *ZICA* ni tishio, kuna *Ebola* ambayo inatoweka toweka lakini nayo ni tishio… na mengine mengine mengi sana yote haya yatakapotokea tunaomba Mwenyezi Mungu yasitokee lakini yatakapotokea ni Wizara ya Afya ndio itatakiwa iyashughulikiwe. Kwa hiyo, nasema wizara ina jukumu kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ni kuibuka kwa vituo vya afya na hospitali nyingi zikiwemo za binafsi ambazo kwa kiasi fulani zinahusika na uchafuzi wa mazingira kwa kutupa taka taka ovyo mitaani au kuchoma moto ovyo ambao moto wenyewe kuchoma mabaki ya madawa pamoja na mabaki ya binadamu ukiyachoma yale hewa ya sumu ambayo inaweza ikasababisha madhara makubwa kwa wananchi. Sasa basi kutokana na haya mimi naona nishauri tu hapa kwamba tunahitaji kuwa na usimamizi wa kiafya sote sisemi Wizara ya Afya tu kwa sababu Wizara ya Afya na sisi pia ni wenzetu tuwasaidie katika kusimamia kiafya na kuimarishwa utekelezaji wa kanuni za afya katika maeneo yote.

Mhe. Mwenyekiti, halafu mpango wa kuwapata wataalamu kwa magonjwa mbali mbali hata hayo ambayo hayajafika hapa, lakini tukiwa nao tayari hapa yakitokea wapo basi pia ingetusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jengine ni maadili ya afya hizi health ethic ni lazima zifatwe kwa utaratibu ule ambao unataka ufatwe. Sasa wizara pia sasa jambo jengine ambalo kwa sababu inatibu maisha ya watu wizara ipatiwe fedha za kutosha katika bajeti zake ili iweze kutibu, kukinga, na kuondosha maradhi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara ya Afya. Utafiti ni muhimu sana kwa maendeleo ya afya, utafiti wowote ule lazima ulenge kwenye kuleta ufumbuzi kwenye tatizo fulani, kuongeza ujuzi kwenye taaluma iliyopo au kuondosha utaratibu uliopo na kuweka ule unaofaa ndio maana ya utafiti na utafiti ni wa kimataifa. Hata ufanywe hapa na huko kwengine njia zitakazofuatwa zitakuwa ndio zile zile. Kwa hiyo, naiomba hii Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ifanye utafiti sana wa magonjwa, kuna magonjwa mengi, mengine pengine hayatambulikani kama yanaathiri sana lakini yapo. Kwa hiyo, tukianza kuyajua hayo tukaanza kuyashughulikia basi tutaweza kupambana na magonjwa ya aina mbali mbali kwa usahihi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri serikali yetu tukufu iwapatie bajeti ya kutosha hawa ili wafanye tafiti zao kwa makini zaidi, wapatiwe usafiri kwa ajili ya kwenda kufanya utafiti huko vijijini na kwengineko.

Sasa niende kwenye Hospitlai za Kivunge na kwengineko, nitakwenda kwa jumla tu sitoenda hospitali moja moja. Sheikh Ame Haji Ali hapa kaeleza kwa sababu yeye ni mwana kamati kaeleza vizuri sana hospitali moja moja, lakini mimi nitakwenda kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nasema yapo mafanikio makubwa sana katika hospitali na vituo hivi vya afya, vinatoa huduma vizuri vingine bado vinakarabatiwa lakini lengo ni kuja kutoa huduma. Sasa lakini wana changamoto na hawa, wana uhaba wa madaktari. Kwa mfao hiyo Hospitali ya Kivunge hapo kuna daktari mmoja tu, kwa sababu pale ni nyumbani nakwenda sana najua kuna daktari mmoja wa ganzi anakaa mjini hakuna nyumba ya kukaa yeye pale. Sasa muda wote anatakiwa awepo pale lakini na nyumbani kwake huko anatakiwa. Kwa hivyo, imekuwa ni matatizo sana yuko peke yake ni vizuri wakawa angalau wawili wakawa wanakwenda kwa zamu ili na huyu mwengine apate kupumzika. Hivyo hivyo wafanyakazi wengine wapatikane ili kuondosha tatizo la ufanyaji kazi, vitendea kazi navyo vipatikane kwa wingi.

Jengine tena niingie kwenye Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi. Bodi hii nayo ina kazi kubwa ya kulinda maisha ya watu kwa kusimamia upatikanaji wa chakula, dawa na vipodozi salama. Kwa sababu kuna baadhi ya hospitali leo utakwenda kununua dawa ya aina fulani nzuri imekutibu dawa ile ile siku utakayokwenda kununua tena inakuwa haifai kabisa inaonekana kama wamechakachua kidogo. Kwa sababu haiwezekani dawa ile ikusaidie ukija kununua tena dawa kama ile usiipate tena ukienda utaipata kwa rahisi zaidi lakini kumbe sio wameshaichakachua.

Sasa kitengo hiki cha madawa niende kwenye madawa ya kulevya. Vijana wengi wameingia kwenye madawa. Pale kwangu Mtopepo wameshanijia vijana wengi wanataka waende *sober house* niwasaidie, nawasaidia wale ambao nina uwezo nao na kuna mmoja akasema hasa mimi nataka kurudi kwetu Uganda kuna wazee wake kule, akasema nisaidie nauli nirudi nyumbani kwa sababu hapa naharibikiwa na mimi yakanijia mawazo kwamba huyu ataharibika zaidi,

nikamsaidia nauli sasa hivi yuko Uganda. Kanitumia salamu huku naishi maisha mazuri na sitaki kurudi tena kwa sababu nikirudi huko nakula unga.

Hapa Kidongochekundu kuna vijana ambao wanapewa dawa za kukata makali ya madawa ya kulevya, pale saa nne ya usiku ukienda washafika wanasubiri dawa ili wapate kunywa waepukane na haya madawa ya kulevya. Lakini sasa nasikia ile dawa inawalevya zaidi wengine wanafuata kwa sababu imeshakuwa ulevi wa bure. Sasa nasema kitengo hiki hakina budi kiichunguze hii dawa, mana wengine nimewasikia wamesema kuna mwenzao mmoja alikunywa dawa ile akenda akalala akafa, sasa wana wasiwasi dawa inaweza kuwa na matatizo. Kwa hivyo, kitengo hiki kifanye utafiti wa kutosha na wa kina hii dawa ni nzuri na lazima wapewe hawa hakuna njia nyengine zozote za salama za kuwafanya wasile madawa zaidi ya kuwapa dawa nyengine wakanywa wakazidi kuathirika? Naomba sana kitengo kinachohusika kishughulikie hili.

Jengine niende kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naipongeza sana Wizara ya Elimu wanajitahidi sana, kuna rafiki yangu hapa Maalim Mmanga Mjengo Mjawiri (Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) unavyomwambia maalim twende ukakague skuli saa yoyote yuko tayari, namshukuru sana nampongeza na Waziri wa Elimu pia nampongeza na yeye yuko tayari kusikiliza matatizo. Kusema kweli hasa wizara hii inajitahidi kutekeleza programu kubwa na ndogo zote kwa pamoja, wanazingatia sana hii *Program Basic Budget,* nimeangalia hapa kwenye kitabu hiki wanaitekeleza vizuri. Lakini sasa kuna matatizo madogo madogo ya changamoto ambazo zinahitaji kutatuliwa kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sina haja ya kuzitaja hizi programu ziliopo lakini nashauri kwa sababu changamoto ni nyingi sana vikalio na mengine wametaja hapa watu wengine, wamediriki kusema yanunuliwe majamvi yawekwe. Mimi siungi mkono kuwanunulia majamvi wapewe madeski wakae juu ya madeski ili waweze kuandika vizuri.

Sasa nashauri huduma za lazima za miundambinu ziimarishwe. Kwa mfano, majengo ya skuli yaimarishwe yale mabovu yatengenezwe, zitanuliwe nyengine kwa sababu wenzangu wamesema hapa darasa moja lina wanafunzi zaidi ya 200 au mia na zaidi. Sasa si rahisi kusomesha watoto mia na zaidi kwa mwalimu mmoja wakati mmoja. Kwanza watakuwa hakuna kwa kupita, huyu akinong'ona tu keshakera wenzake wote. Kwa hiyo, ni vizuri labda wasizidi 40 au 50 wanaweza kutosha. Hivyo, tutanue skuli zetu ili madarasa yawe mengi tuweze kufundisha wanafuzni wetu kwa wingi zaidi.

Baraza la Mitihani nalo lina jukumu kamilifu la kusimamia mitihani ya Moko isiwe wao wawe na madaraka kamili ya kusimamia hii mitihani ya Moko, wasitegemee usimamizi utoke mahala pengine. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu naishauri sana Moko waisimamie wenyewe badala ya kusubiri wasimamie wenzetu ama kutoka Bara ama kutoka kwengine kwani elimu yetu hapa mradi *syllabus* zetu ziko sawa nadhani hakuna sababu kwa nini tusiweze kusimamia wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naona unanitizama sana kwamba muda wangu umekwisha, nakushukuru kwa kunipa muda na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii nikaweza kusimama hapa na kuweza kuchangia ripoti hii ya kamati. Nianze kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya na naibu wake na Afisa Mdhamini Pemba. Pia nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na naibu waziri na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na Wizara ya Afya. Hospitali ya Wete. Hospitali hii ni hospitali kubwa kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba niende kwenye Wodi ya Wazazi. Wodi ya Wazazi ya Hospitali ya Wete tunajua kuwa kuna wataalamu wengi ambao wanaweza kutusaidia sisi wanawake tukienda kujifungua, lakini tunajua kwamba kuna wakunga ambao wanatokana na hospitali na wakunga wa vijijini. Hospitali ya Micheweni huwa wanatoka wazazi kwenda kujifungua Hospitali ya Wete wanapopata rufaa, lakini wanapokwenda kule na wakunga wao huwa wanadharauliwa sana. Kwa sababu sekta hii imetugusa sana sisi wanawake Mhe. Waziri tunajua tuna wataalamu wengi wa afya, tuna wakunga, tuna na wakunga wa kienyeji, Mhe. Waziri kwa kweli tunamuomba sana aweze kuzungumza na wakunga hawa ili wanapokwenda wazazi Hospitali ya Wete wasiwanyanyase kwa sababu kuna matokeo mbali mbali ambayo yanajitokeza.

Hivi juzi kulitokea tukio kulikuwa na mzazi amejifungua mtoto wake salama usalimini lakini likatokea tatizo kwenye kitovu, tunajua sasa hivi kuna utaalamu mwengine wa kufunga kibanio. Zamani ilikuwa tunafunga uzi halafu tunaweka plasta, ikisha tunafunga na vibanio vyengine ambavyo ni vya mipira, lakini vibanio hivi kwa kweli vimetoa athari kubwa kwa watoto wetu. Mhe. Waziri tunajua ni wataalamu sana wakunga wale lakini wahudumu wale waweze kupewa taaluma sahihi ili kuokoa maisha ya mtoto pamoja na maisha ya mama.

Mhe. Mwenyekiti, niende Hospitali ya Micheweni. Hospitali hii ni hospitali ya wilaya takriban wilaya nzima huwa wanatumia hospitali ile. Lakini hospitali ile ni ya zamani sana eneo la hospitali lina uzio lakini uzio ule ulijengwa tangu hospitali ile ilipofunguliwa. Kama tunavyojua tuna Wodi ya Wazazi ambayo alisimamia Mama Shadya na Mwenyezi Mungu akamjaalia wodi ile ikajengwa mpaka tukahamia na vitanda vimo *Alhamdulillah*, lakini magodoro yake yamechanika kwa kweli ile sio hatua nzuri kwa hospitali ile kuhudumia wazazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa kweli hospitali hii tuna daktari mmoja tu anayehudumia watu wanaopata ajali na wanaofariki. Daktari yule mmoja hata akipigiwa simu akija kwenye maiti kumkagua ni hatua kubwa sana kwa kweli. Tunamuomba Mhe. Waziri aweze kuweka daktari wa pili ili kuweza kufanya ufanisi wa kazi hii, kama tunavyojua wananchi tunapotokewa na ajali tunatakiwa na maiti wetu tukienda kumtaka maiti yule tuweze kumchukua ili kwenda kumzika. Sasa hatua zile ziwe ni za wepesi na za ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, niende Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa kweli tunamshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na kutujengea majengo ya skuli ili watoto wetu waweze kusoma na wawe wataalamu na waweze kuja kutusaidia.

Sasa niende hapa kwenye Chuo cha Kiislamu Micheweni. Chuo cha Kiislamu Micheweni kilifunguliwa tangu mwaka 2001, chuo kile kina mazingira ambayo ni ya utatanishi kwa sababu

kuna wananchi ambao wanasema maeneo yale ni yao sasa hivi, kwenye ripoti hii ya kamati ni changamoto mojawapo eneo lile linavamiwa, ingawa ukuta ule ulijngwa tangu kipindi cha miaka mitano iliyopita. Tunamuomba Mhe. Waziri aweze kulisimamia hili ili uzio ule uweze kumaliza wananchi wasiweze kuyavamia maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye skuli zenye dakhalia Wilaya ya Wete kuna matatizo, kwenye changamoto wameeleza kuna matatizo ya gani kwa sababu wale ni wanafunzi na ni watoto ambao wanaishi pale linapotokea tatizo wanashindwa kupelekwa hospitali kwa sababu hapana gari. Mhe. Waziri tunamuomba sana aweze kufanya juhudi zake pamoja na kushirikaina na wizara na serikali ili ipatikane gari watoto wale wanapopata maradhi waweze kupelekwa hospitali.

Nikiendelea mbele nirudi nyuma, Chuo cha Kiislamu napo pia pana changamoto ya garim, gari lile ni la mwanzo tangu chuo kile kilipofunguliwa gari lile ni kubwa kwa kweli ni tatizo kwa wanafunzi. Kwa sababu gari lile ni la kuchulia kuni na vifaa vya chuo pamoja na chakula. Mhe. Waziri tunamuomba aweze kufuatilia ili kufanye uwezekano na kuweza kupatikana gari kwa sababu chuo kile ni kikubwa na kwa kweli wanafunzi ni wengi zinapotokea kesi kama hizo inakuwa ni mtihani. Wanafunzi wenyewe wawe na mashirikiano ya pamoja waweze kupiga simu kwenye maeneo mbali mbali ya Jimbo la Micheweni ili kuweza kupata gari akachukuliwe mwanafunzi kupelekwa Hospitali ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea mbele nije hapo hapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Naibu Waziri na watendaji wake wote na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na hatua ambayo ni ya utekelezaji wa juu kwenye huduma hizi za elimu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru aunga mkono ripoti hii ya kamati kwa asilimia mia moja ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kunipa fursa hii niweze kuchangia machache kuhusu Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Wajamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependa niseme machache kuhusu Wizara ya Afya hapo labda naweza nikasaidia kwa kiasi fulani. Kwanza nianze kuzungumzia suala la afya kwa upande wa kupongeza wizara hiyo kwa jitihada wanazozifanya, ingawa mapungufu yapo hatukatai lakini kwa kiasi fulani wanajitahidi isipokuwa changamoto pahala popote hazikosekani madhali panaishi watu na mahitaji ni makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, watu walikuwa wanazungumzia kuhusu rufaa hasa kwa upande wa Kaskazini ya Unguja. Wanasema kwamba hospitali ile ni kwa ajili ya watu labda vijiji kama sabaa pamoja na eneo zima. Mimi nataka watu wafahamu tunapozungumza hospitali za wilaya ina maana kwamba wilaya nzima hospitali zote ndogo ndogo zinazozunguka katika wilaya ile rufaa yao inakuwa ni pale kwenye hospitali kubwa iliyoko katika sehemu ile. Kwa hiyo, ndio maana kuna Kaskazini hospitali yao ya rufaa ni Kivunge, Makunduchi Hospitali ya Wilaya kwa Wilaya ya Kusini, Mnazi Mmoja kwa Mjini na Pemba halikadhalika utaratibu ni huo huo. Kwa hiyo,

nafikiri si kosa kama watu watatolewa kwenye vituo wakapelekwa kwenye Hospitali ya Kivunge kwa ajili ya kwamba wanakwenda kupata mahitaji zaidi. Vituo vya afya vidogo vinafanya kazi ndogo lakini Kivunge ndio Hospitali ya Rufaa kwa kule.

Tunapozungumza rufaa watu wanafikiri rufaa sijui ndio mpaka hospitali iwe kubwa inafanya kazi kama Muhimbili, rufaa maana yake ni kutoka katika hospitali ndogo ukaenda hospitali kubwa. Ukitoka hospitali ya Kidoti ukienda Kivunge tayari umekwenda kwa rufaa, ukitoka Kivunge ukienda Hospitali ya Mnazi Mmoja tayari umekwenda kwa rufaa na hospitali za rufa azilizo kubwa ni mbili kwa Unguja ni Mnazo Mmoja na kwa Pemba ni Abdalla Mzee. Kwa hiyo, naomba watu wafahamu hivyo na hivyo kusiwe na malalamiko kwa nini watu wengine wanakwenda pale.

La pili, pamezungumziwa ukosefu wa majumba katika mahospitali. Ni kweli hilo, lakini wakati tunajenga vituo vya afya wananchi walikuwa wana moyo walikuwa karibu kila kijiji kinatakiwa kiwe na kituo cha afya na walijitahidi mpaka ikafika wakati tukasema jamani hata kigezo cha Umoja wa Mataifa ni kilomita tano, sasa hivi vituo vya afya vimekuwa chini ya kilomita tano. Mimi nafikiri sasa hivi ifike wakati tusimamishe na kweli Rais akatoa tamko. Lakini nyumba haziko katika utaatibu kama huo karibu ukiona nyumba zote zimejengwa na Wizara ya Afya kwa nini wananchi tusiwe na moyo ule ule pamoja na Wawakilishi na Wabunge wetu tukajaribu kusaidiana na serikali tukajenga nyumba kwa ajili ya wafanyakazi katika sehemu zetu za vituo vya afya. Mimi nafikiri tukifanya hivyo itakuwa tunajisaidia sisi na serikali bila shaka itachukua juhudi kusaidia juhudi hiyo inayofanyika.

Pia kumezungumzwa kuhusu lugha ya wafanyakazi. Wafanyakazi wa afya wana lugha mbaya. Mimi sisemi kwamba tuna lugha nzuri au tuna mbaya, lakini nafikiri inategemea na mazingira. Kama tunavyoambiwa kwamba wafanyakazi wa afya wako kidogo. Wizara ya Afya ilipokuwa inachukua makundi fulani kwa miaka ya nyuma, ilikuwa inachukua wafanyakazi wengi, na wafanyakazi wale imefika kipindi sasa hivi wanatoka kwa wingi vile vile. Kwa hivyo, wafanyakazi wa afya wamekuwa kidogo sana. Serikali imekubali na itaajiri watu.

Lakini pia mimi nafikiri na wananchi tunaokwenda mahospitali tukienda twende na nia njema. Kwa sababu kuna wengine mtu anajifunga tangu anakotoka, mimi nikifika pale ukinigusa tu, maana ndio tabia yetu kwamba kwa nini kwa sababu tunafanyakazi hivyo, lakini sio hivyo. Tukienda kwa lugha nzuri na wale ni binadamu, binadamu akiwa kachoka watu wamemzunguka atakuwa ana- *panic* na ikiwa utamkorofisha kidogo tu atamaliza aliyonayo moyoni.

Kwa hivyo, mimi nafikiri tuwe na lugha nzuri baina yetu sisi wafanyakazi wa afya na wagonjwa wanaokuja pale. Au wanaokuja kuangalia jamaa zao, vyenginevyo watakuwa wanakosana kila siku. Ukiambiwa kwamba sasa hivi huwezi kuingia basi ukubali, kwa sababu anayehudumiwa kule ndani ni mgonjwa wako na kuna saa za kutizama wagonjwa fika kwa wakati. Lakini saa nyengine kunatokea dharura hatukatai, basi jaribu kujieleza ili na wenzetu wafahamu kwamba huyu mtu ana dharura na dharura hii kwa kweli nimsaidie, sio kwa kuingia ndani basi hata wewe ukichukua ukenda ukamsaidia. Vile vile kuhusu wale walinzi wa maeneo yale, nao pia wako pale kwa ajili ya kutekeleza taratibu zao. Kwa hivyo, mimi nafikiri ifike pahala tuelewane kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *ZSJ*. Mimi kwa upande wangu naona kwamba kwa vile sheria ya wakala imeshapitishwa na vile vitengo vikiwa vitasaidiana, nafikiri mambo yatabadilika kwa kiasi fulani. Mimi nafikiri na wananchi nao wajitahidi kusoma vifuko au vifungashio, vyakula pamoja na madawa, vina umri wake vinatakiwa vianze leo na vimalizike kesho. Kwa hivyo, ukikiona uchukuwe jitihada ujuwe kwamba hiki kweli kinafaa au hakifai. Mimi nafikiri kwa sasa hivi taifa letu limeelimika, wengi wetu tunajua kusoma, kama hujui kusoma muulize mwenzio. Hivi kweli hiki kingali bado kwenye matumizi, kwa sababu usipofanya hivyo ukitumia kitu ambacho kimepitwa na muda wake, bila shaka utapata madhara.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu wodi ya wazizi. Leo nimekwenda wodi ya wazazi nilikuwa nina mgonjwa jana. Napenda niipongeze serikali pamoja na Wizara ya Afya kwa wazazi wote wanaozaa kwa kawaida au kwa operesheni hakuna anayenunua vitu, vitu vyote viko kamili, kwa hilo napenda niwapongeze.

Vile vile kulizungumzwa kuhusu Chuo cha Afya na kutaka hospitali ya afya. Mimi nafikiri sasa hivi kwa vile Chuo cha Afya kimeshakwenda *SUZA. SUZA* kinajiandaa kwa hayo, lakini sasa hivi itabidi zitumike hospitali hizo hizo zilizopo ambazo ni za rufaa na vituo mpaka hapo mambo yatakapokaa sawa. Kwa hivyo, hicho sio kitu cha siku moja kwa sababu wanahitaji madaktari wale wale wa kuwafundisha na ma-*nurse* wale. Kwa hivyo, tuendelee kutumia wakati serikali inajiandaa la kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, napo nitowe pongezi sana kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mwaka jana wametufunua macho, skuli zetu zile kubwa kubwa zilifanya vizuri na matokeo sote tumeyaona ni tofauti na mwaka juzi. Kwa hivyo, jitihada imeonekana kwamba tulipotoka na sasa hivi tulipo ni tofauti na nawaomba wazazi na walimu tuzidi kushirikiana ili tupate matokeo mazuri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, serikali ilifanya elimu bure, serikali bado ina nia ya kufanya elimu yote kuwa bure, kwa hivyo tusomeshe watoto wetu Mwenyezi Mungu akipenda *In Shaa Allah* hivi karibuni Mwenyezi Mungu akitupa nguvu elimu ya sekondari na ya *primary* itakuwa bure. Ahsante sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dk. Sira. Lakini kabla sijawaita Waheshimiwa Mawaziri, muda wetu uliobakia ni mdogo sana, kwa hivyo nilikuwa namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atowe hoja ya kuweka kando kanuni ya muda, ili tuendelee na yaliyobaki. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa hoja ya kuliomba Baraza ili tutenge kando kanuni ya 23, ambayo ndio kanuni ambayo inaongoza muda wa vikao. Kwa kuwa leo siku ya Ijumaa kanuni zinatueleza vikao vya Baraza vitamalizika saa 1:45 na kwa kuwa hoja iliyokuwepo mezani, bado haijamalizika. Kwa hivyo, naomba kuliomba Baraza na kutoa hoja ya kutenga kando kanuni hiyo ili tuendelee na mjadala mpaka hapo utakapomalizika. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa wale wanaokubali wanyooshe mkono, na wanaokataa. Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa hii kuweza kuchangia na kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo wajumbe wanazichangia.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu ambaye ametujaalia uzima na afya njema tukaweza kuwa hapa katika Baraza letu tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii vile vile kumpongeza kwa dhati kabisa na kumshukuru Mhe. Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein, kwa jitihada yake kubwa kwa serikali yetu, lakini jitihada kubwa kwa Wizara yangu ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Napenda sana kumshukuru mheshimiwa kwa mchango wake wa hali na mali ambao jicho lake lote analitupa katika sekta ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na kamati yake yote, kwa ushirikiano mkubwa ambao wanaipatia wizara yangu. Kwa kweli tunamshukuru sana Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame pamoja na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa sekta zetu za elimu na afya.

Mhe. Mwenyekiti, michango yote ambayo kamati imetoa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, wizara yangu imechukua, maoni ambayo yametolewa vile vile wizara yangu imechukua. Kwa vile mwezi wa Septemba In Shaa Allah ni mwezi ambao tutakuja kuzijibu vizuri hoja za kamati, basi kwa zile ambazo sitozitolea ufafanuzi, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe waone kwamba nitazitolea ufafanuzi katika kipindi hicho kwa kina kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima la uchakavu wa majengo, kama ambavyo kamati na wajumbe wengi wamelichangia suala hili. Tunakubali kwamba majengo yetu mengi sio yote yamechakaa, na uchakavu huu unatokana na kwamba majengo haya yamejengwa katika miaka ya zamani. Kwa hivyo, bila shaka hata mtu kadiri miaka inavyokwenda anakuwa mkubwa habaki kama alivyo. Kwa hivyo, na majengo ingawa hayasemi nayo vile vile yanakuwa na umri chakavu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inafanya ukarabati kwa maskuli mbali mbali kadiri hali ya fedha inavyoruhusu. Tayari wizara yetu imeshafanya ukarabati katika majengo ya skuli za Forodhani, Tumekuja pamoja na Hamamni kwa upande wa Unguja. Vile vile skuli ya Fidel Castro, Utaani pamoja na Uweleni kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ukaratibu huu haujamalizika kama ambavyo nimeeleza awali kwamba inategemeana na upatikanaji wa fedha. Lakini tayari kwa sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeshafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango, na tayari makubaliano ya skuli tatu nyengine zitaingia katika ukarabati. Skuli ambazo zitapata ukarabati huo ni skuli ya Lumumba, Bembela pamoja na skuli ya Haile Sellasie. Kadiri hali ya fedha itakavyokuwa inaruhusu basi na skuli nyengine vile vile nazo zitaingia katika ukarabati huo, zikiwemo skuli za msingi, maandalizi na zote amabazo zinatuzunguka.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi walizungumzia suala zima la uhaba wa vifaa kwa skuli ya ufundi. Napenda niwaambie Waheshimiwa Wajumbe, kwamba wizara yangu tayari imenunua vifaa vingi tu kwa skuli ya ufundi ya Mikunguni, pamoja na skuli ya Kengeja. Katika kupeleka vifaa huko, tulipeleka vifaa mbali mbali vya umeme pamoja na kozi nyengine ambazo zinasomwa katika skuli hizo. Juzi tu siku ya tarehe 14 mwezi huu wa Februari, tulipokea msaada wa kompyuta 50 kutoka kwa ndugu zetu wa NMB benki, na katika kompyuta hizo tulichukua kompyuta 10 tukazipeleka katika skuli ya ufundi ya Mikunguni. Yote hii ni katika kuisaidia skuli yetu hiyo pamoja na ile ya Kengeja Pemba kuwa na vifaa vizuri kwa ajili ya kutoa elimu stahiki kwa wanafunzi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wizara yangu inajitahidi sana katika suala zima la ununuaji wa vifaa vya maabara, vitabu pamoja na vifaa vyengine ambavyo vinahitajika ndani ya maskuli, ili kuona usomaji na usomeshaji unafanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wawe na imani na wizara yangu, lakini vile vile na wao wasichoke kutoa mashirikiano yao ya hali na mali kwa kila jambo litakalokuwa na mustakabali mwema wa maendeleo ya elimu yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi vile vile walikuwa wanazungumzia suala zima la wingi wa wanafunzi. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo wajumbe wamezungumza tuna idadi kubwa sana ya wanafunzi hasa kwa upande wa skuli za msingi. Skuli ambayo imetajwa ya Kinuni sio peke yake zipo na nyengine nyengine nyingi, na hasa skuli za ukanda wa Magharibi ndizo ambazo zimetia fora kwa kuwa na wanafunzi wengi. Kinuni, Kijitoupele, Bububu na nyenginezo zina idadi kubwa sana ya wanafunzi. Serikali imeliona suala hilo na haijalifungia macho. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilitiliwa fedha kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madarasa, madarasa ambayo yako baadhi yalijengwa kwa nguvu za wananchi serikali imeweza kuyamaliza. Madarasa ambayo yaliweza kumalizwa katika kipindi cha shamra shamra za Sherehe za Mapinduzi matukufu ya Zanzibar yalizinduliwa zikiwemo skuli ya Magogoni, Chutama, Ghana, Binguni Maandalizi, Kihinani, Bwereo kama ambavyo Mhe. Ame hapa alivyotuthibitishia kwamba skuli yake imejengwa, nyengine zote ni jitihada ambazo serikali inachukua katika kupunguza tatizo la wingi wa wanafunzi.

Vile vile skuli ya Mgogoni, Chokocho, Jambangome na skuli mpya ya Mgonjoni ambayo serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilijenga skuli hiyo kwa nguvu zake kuona kwamba wananchi wa kule nao wao wanapata fursa hiyo. Kwa hivyo, ni kwamba serikali haijakaa kulitizama tu suala hili.

Vile vile juzi tu tulipata madarasa mawili kutoka kwa wahisani wa *Sea Cliff* katika Jimbo la Mahonda, Skuli ya Maandalizi ya Kiombamvua. Tunawashukuru sana kwa msaada ambao

wametupatia, na msaada huu pia utasaidia kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi wa maandalizi ambayo imetusakama.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha wanafunzi wa msingi wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu, wizara yangu imeanza ufanyaji wa mitihani ya darasa la nne ili kuhakikisha kwamba lengo la ubora wa elimu linapatikana tokea huko chini. Mhe. Mwenyekiti, napenda sana niwaambie wajumbe, najua wamesikia lakini naomba wajuwe kwamba wanafunzi wetu kwa mwaka 2016 walifanya mtihani wa darasa la nne na wapo ambao walifaulu vizuri sana, na hii ni katika kuwapima ubora wa ufaulu na kuona kiwango cha elimu kinaanza vizuri tokea elimu ya msingi.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tunawaomba sana katika majimbo yenu basi tuwahimize wazazi tukiwa na sisi wenyewe, kuona kwamba wanafunzi wanathamini kufanya mitihani ile ya darasa la nne, ili tuweze kuwapima vizuri sana na tuweze kuona ni namna gani tunaweza kuongeza jitihada nyengine pale ambapo pana mapungufu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uhaba wa walimu. Ni kweli walimu hawatoshi. Mhe. Said Omar Karatu alisema kwamba hata tukiwachukua walimu wote wa Unguja na Pemba tuwaweke katika Uwanja wa Amani, wataonekana ni wengi sana kwa ule wingi wao, lakini tukiwachukua walimu wale kila mwalimu tukamuweka katika darasa, basi tutakuwa tuna madarasa mengi sana ambayo hayatakuwa na walimu. Hii yote ni kutokana na idadi kubwa sana ya wanafunzi ambayo tunayo. Katika kulithamini hili serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar, tayari imeanza uajiri wa walimu wa sayansi na takriban walimu 195 mpaka sasa wameshaajiriwa, na bado wanaendelea katika mchakato huo na baada ya zoezi hili wataendelea kuajiriwa walimu wa *Art* hawatoachwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la dakhalia lilizungumzwa na kamati, lakini vile vile wajumbe wengi walilizungumzia. Dakhalia ni changamoto na sote tunafahamu kwamba mwanafunzi anapokuwa katika maeneo ya skuli anasoma vizuri zaidi kuliko anapokuwa nyumbani. Kwa upande wa Unguja tunayo dakhalia yetu ya Mazizini, dakhalia hii inatumika kwa wanafunzi wa kike hasa wanaotoka katika maeneo ya mbali ya vijijini. Lakini wanafunzi wengi kwa sasa naona hawapendi kwenda kukaa. Tunaomba sana tuwaambie wanafunzi kwamba dakhalia ya Mazizini ipo na kwa yeyote anayetaka kuja kuishi basi aje wizarani na atapatiwa sehemu hiyo na ataweza kuishi bila ya usumbufu wowote.

Kwa upande wa Pemba tuna dakhalia katika skuli ya Utaani, Fidel Castro, skuli yetu mpya ya Mohamed Juma Pindua, pamoja na skuli ya Kengeja. Skuli hizi zote zina dakhalia na wanafunzi wanakaa na wanasoma vizuri sana. Kwa hivyo, tuwaombe sana wanafunzi ambao wanaishi katika dakhalia hizi wazidi kusoma kwa bidii, lakini hata wale ambao hawaishi katika dakhalia, basi na wao vile vile wafanye jitihada za makusudi kusoma kwa bidii zote, kwa elimu ndio msingi wa kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kama pia ilizungumzia hoja ya ujenzi wa skuli ya Kibuteni kwamba umelala. Napenda nimuhakikishie Mwenyekiti wa kamati pamoja na kamati yake na wajumbe wote wa Baraza lako tukufu ujenzi wa Kibuteni haujalala. Haujalala kwa maana kwamba mkandarasi aliyekuwepo pale *United Builders* alishindwa uwezo wa kuendelea na ujenzi ule, baada ya kushauriana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tulivunja mkataba ule wa ujenzi. Katika

siku ya tarehe 8/9/2016, baada ya kuvunja mkataba ule wa ujenzi wizara ilifanya utaratibu wa kupata wakandarasi wengine, na walijitokeza wakandarasi kama saba, lakini baada ya mchakato wote kampuni nne ndizo ambazo zilikabidhi na zilikidhi vigezo na kupewa zabuni, baada ya kupewa zabuni kampuni mbili tu ndizo ambazo zilirudisha. Kampuni hizo zilikuwa ni *Rans* pamoja na *Salim's Construction*. Katika mchakato huo kampuni ya *Rans* ilibahatika kupata tender hiyo kutokana na kiwango chake cha fedha ambacho ni jumla ya shilingi bilioni 2,069,860,400 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa kumalizia skuli ile ya Kibuteni.

Kwa hivyo, waheshimiwa tuwe na imani wizara inafanyakazi na haijatulia ili kuona kwamba skuli ile inamalizika. Kama ambavyo imemaliza skuli ya Mkanyageni ya Mohamed Juma Pindua, basi In Shaa Allah na Skuli ya Kibuteni nayo itamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala zima la upatikanaji wa bajeti. Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru sana Wizara ya Fedha kwa utoaji mzuri sana wa bajeti kwa wizara yangu, najua na kwa wizara zote nyengine tunapata bajeti vizuri sana. Mhe. Waziri wa Fedha juzi alikiri kwamba makusanyo ni mazuri sana. Kwa hivyo, kutokana na uzuri wa makusanyo hayo, kwa hivyo hata zile *OC* zinavyoingia kwenye wizara zetu, zinaingia vizuri sana. Tunashukuru kwa hili na tunapenda sana kuipongeza Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la ujenzi wa ukumbi wa maafali ya *SUZA* ambao haukukwama kwa sababu fedha hazikupatikana. Ujenzi wa ukumbi wa *SUZA* ulichelewa kidogo kutokana na taratibu za kutafuta mkandarasi. Lakini tayari ujenzi huu hivi sasa umeanza na unaendelea, na sasa hivi wapo katika hatua ya kumalizia jamvi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala zima la utaratibu wa mitihani ya majaribio yaani *mock*. Napenda kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba, utaratibu mzuri wa mitihani ya *mock* wizara yangu utauzingatia, na ushauri wenu wote ambao mmeutoa basi tumeuchukua na tutauzingatia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la huduma ya chakula na malazi katika kambi ya usahihishaji. Mhe. Mwenyekiti, huduma ya chakula na malazi kwa kambi ya usahihishaji itaimarishwa kadiri ya hali ya fedha itakavyokuwa inaruhusu. Katika kulitekeleza hii, tunaangalia uwezekano wa kuweka kambi zaidi ya moja, kwa sababu wanafunzi wetu ni wengi sana, kwa hivyo ina maana tuwe na kambi tofauti ili tuweze kumaliza kwa wakati suala zima la usahihishaji. Kwa hivyo, tunapenda sana tuwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, suala hili tutalifanyia kazi vizuri sana na kambi zetu zitakuwa na mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, napenda vile vile nichangie katika suala zima la ufaulu wa wanafunzi. Mhe. Mwenyekiti, suala la ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2016, matokeo hayakuwa mabaya kama ambayo yalikuwa yanazungumzwa. Mhe. Mwenyekiti, skuli zetu za Zanzibar zilitajwa kwamba zilishika nafasi ya mwisho kati ya skuli kumi za mwisho kwa Tanzania nzima, lakini Mhe. Mwenyekiti, tunapoyaangalia matokeo ya skuli moja moja basi matokeo yale yalikuwa ni mazuri sana.

Kwa mfano katika Skuli ya Tumekuja asilimia ya ufaulu ilikuwa ni asilimia 87.93 na vile vile kwa skuli ya Tumekuja kwa mwaka jana walipata Division I nne kitu ambacho hakijawahi

kutokea huko nyuma, kwa hivyo hapo ni kwamba palikuwa na ufaulu mzuri sana ingawa tuliambiwa kwamba tuko namba ya mwisho.

Lakini vile vile kwa Skuli ya Mpendae kulikuwa na asilimia 75% asilimia ambayo haikuwahi kutokea katika miaka ya nyuma, kwa hivyo ufaulu ulikuwa ni mzuri.

Lakini hata kwa Skuli ya Lumumba Mhe. Mwenyekiti, Skuli ya Lumumba ilipata asilimia ambayo haijawahi kuipata katika miaka mitano ya nyuma iliyopita, hii yote inaonyesha kwamba skuli zetu zilifanya vizuri ingawa zilitajwa kwamba zilikuwa ni skuli za mwisho kitathmini kama ambavyo zilifanyiwa tadhmini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kidato cha nne matokeo yetu ya mwaka jana 2016 ufaufu umeimarika kwani skuli zetu zimefanya vizuri sana zaidi ya sana, Skuli ya Lumumba imechukua nafasi ya 44 kati ya skuli 4,224 za Tanzania nzima, na skuli ya Fidel Castro imechukua nafasi ya 98 kati ya skuli 4,224. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kitathmini tukisema zile Top Ten basi Skuli ya Lumumba inaingia ile *Top Fifty* inaingia kwa Tanzania nzima, kwa hivyo hiyo ni nafasi kubwa ya kistoria ambayo tumeweza kuipata. Na leo hii tumeshuhudia *Division 1* nyingi ambazo zilikuja, na zile zilizokuja zilikuwa za upande wa Unguja baadhi tu sio zote, kwa sababu Lumumba peke yake tu moja ilikuwa na *Division 1* - 54, ukiachia hizo skuli nyengine na kwa Zanzibar nzima tumepata daraja la kwanza 242 Mhe. Mwenyekiti, hatujawahi kupata matokeo kama haya kwa skuli zetu.

Lakini vile vile daraja la pili tumepata 879 ni historia kubwa sana kwa nchi yetu kupata matokeo kama haya na tunawapongeza sana walimu pamoja na wanafunzi wote ambao wamefanikiwa katika matokeo haya, vile vile na wanafunzi kwa upande wa Pemba ambao wamepata *Division* leo kwa bahati mbaya hawakuwepo, lakini wa wao ishaalla siku nyengine tutawaleta katika kikao chako kitukufu cha Baraza ili waonane na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilizungumzia suala zima la maslahi ya walimu lakini wajumbe wengi nao vile vile walichangia suala zima la maslahi ya walimu, tunapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari ina mpango wa kufanya marekebisho ya mishahara kwa watumishi weake wote wa umma, hivyo Wizara ya Elimu nayo itaingia katika mkumbo huo na wafanyakazi wote maslahi yao yatapata kuimarika.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la upatikanaji wa fedha za *SDL* Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali tayari suali hili tumelizungumza kwa pamoja na wenzetu Wizara ya Fedha wametuhakikishia kwamba, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha hizi za *SDL* zitaingia katika mfuko wa Wizara ya Elimu na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali itapatiwa asilimia 40, Elimu ya Juu itapatiwa asilimia 60 hizi zote ni juhudi za Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lilizungumzwa vile vile suala zima la mgogoro wa umeme wa Chuo cha Karume, mgogoro huo upo na bado haujamaliza tunaomba sana wenzetu wa *ZECO* suala hili tulimalie, kwa sababu sote tunajenga nyumba moja sote ni taasisi za Serikali sisi tayari pana umeme wa jua, kuwepo kwa umeme wa jua tunatarajia kwamba deni la umeme liweze kupungua. Lakini kinyume chake kila deni linapokuja kwa mwezi linaongezeka maradufu ambalo halishuki chini ya milioni 3,475,000/= kwa kila mwezi. Hichi ni kiwango kikubwa sana

kwa taasisi ile ya kielimu ambayo inatoa elimu kwa taifaletu, tunaomba sana *ZECO* suala hilo walizingatie na waone kwamba kuwepo kwa sola katika Chuo cha Karume basi ni kupunguza matumizi haya ya umeme na watufanyie kama vile ambavyo inastahiki, nina imani na *ZECO* kwamba kwa hili hawatotuangusha na tutakwenda nalo vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, lilizungumzwa suala la uhaba wa madawati Serikali yetu inatambua suala hili na inalithamini sana na katika hilo Mhe. Rais aliunda kamati maalum ya kitaifa ya kupambana na tatizo la madawati, kamati inafanya kazi zake vizuri na tayari kuna fedha zimeshaanza kupatikanwa lakini tunalishukuru sana Baraza lako la Wawakilishi kwa michangio ambayo imechangiwa na Wajumbe wote wa baraza hili. Michango ambayo wajumbe wameitoa itakwenda moja kwa moja katika ununuzi wa madawati na fedha hizi zimeingia katika kamati ya madawati na hazijaguswa na mtu.

Kwa hivyo fedha za wawakilishi, fedha ambazo wahisani wanachangia mbali mbali zipo katika account ambayo ipo chini ya Wizara ya Elimu lakini inalindwa katika kamati ya kitaifa amayo Mhe. Rais ameiunda kukusanya madawati na tunatarajia katika kamati itafanya harambee mbali mbali ili iweze kupata fedha zaidi kwa ajili ya kutanua mfuko huu, na Wizara ya Fedha itatoa fedha nyengine za kujalizia ili tuweze kuona kwamba tatizo la madawati kwa Zanzibar nzima linamalizika. Tunaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuungane mkono kwa hili kutatua tatizo la madawati. Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru vile vile Waheshimiwa Wabunge ambao nao wamechangia madawati kila mmoja ameleta madawati 100 vile vile tunashukuru kwa hili.

Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Mahonda nae katika jimbo lake amechangia madawati kwa Skuli ya Mahonda pamoja na skuli ya Kitope Msingi vile vile tunamshukuru na tunawashukuru wote ambao wamechangia madawati, wakiwemo ndugu zetu wa *NMB Bank* ambao wametupatia madawati 450 hizo zote ni jitihada za kuweza kutatua tatizo la madawati. Vile vile Huwawe wametuchangia madawadi kwa madarasa manne kwa skuli mpya ya Mgonjoni, Matemwe Bungalows wametuchangia madawati 50 kwa Skuli ya Kigomani. Lakini vile vile bibi Rahma wa Qatar nae ametuchangia madawati 91, kwa michango hii halijamlia tatizo lakini kwa jitihada ambazo Serikali inachukua basi karibuni tu tatizo hili nalo litamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, suala la vyoo ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba ni changamoto kwa sekta yangu hasa kwa skuli za maandilizi msingi pamoja na Sekondari. Mhe. Mwenyekiti, Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali inajitahidi sana katika suala zima la ukarabati wa vyoo na tayari tumeshafanya ukarabati wa vyoo katika skuli mbali mbali zikiwemo Skuli ya Langoni, Mtoni Kidatu, Koani, Bwefum, Welezo, Abdalla Sheria, vile vile Skuli ya Uwandani, Kisiwapana, Mwambe, Shamiani, Sisimizini, Ngomeni, Kinyasini, Kilindi, Micheweni, Makangale na Mkia wa Ng'ombe kwa upande wa Pemba.

Lakini kwa kushirikiana na ndugu zetu wa *ZAWA* kuna mradi maalum wa ujenzi wa vyoo na tayari vyoo hivi vinajengwa katika skuli mbali mbali ikiwemo Skuli ya Haile Selassie, Bembela, Hurumi, Kiponda, Nyerere, pamoja na Skuli ya Migombani. Hizi zote ni jitihada za kuondosha tatizo hili la vyoo, na kadri fedha zinavyokuwa zinapatikana basi tatizo la vyoo nalo litamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba tunawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi kwa michango yao mizuri ambayo wameitoa, michango ambayo ina lengo na nia ya kuijenga sekta yetu ya elimu na ishaalla tunawaahidi kwamba Wizara itakuwa nao bega kwa bega na haitowaangusha katika kuleta maendeleo na mafanikio ya elimu kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tunapenda tuwashukuru wafadhili mbali mbali ambao wanachangia huduma za elimu kwa nchi yetu ya Zanzibar, vile vile wazalendo ambao wanachangia Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na Wabunge ndani ya majimbo yao na viongozi wengine wote wanaochangia sekta ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti tunaomba sana ndugu zetu wa polisi tuwe na mashirikiano nao ya karibu sana hasa katika suala zima la kupambana na wizi wa vitabu ambavyo vinaibiwa katika maktaba zetu, tunaomba sana pale ambapo wezi wanakamatwa basi washirikiane na sisi ili adhabu kali kwa watuhumiwa wale iweze kutolewa na iwe ni fundisho kwa mwizi yule na kwa mwizi mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, napenda sana niwaambie Waheshimiwa wajumbe kwamba Zanzibar elimu yetu imepanda kwa kiwango kikubwa sana, katika mkutano ambao tumehudhuria mkutano wa Kiwizara katika kanda za nchi 13 za ukanda wa Afrika ya Mashariki, suala la elimu ya mwanamke wenzetu ndio kwanza wanaanza nalo katika mpango wa maendeleo endelevu wa SDG 4 *twenty thirty* katika mkakati huo ni kwamba wanataka mwanamke apate elimu ambayo ni bora na ya uhakika. Mhe. Mwenyekiti, kwa Zaznzibar tayari tumeweka skuli maalum za watoto wanawake kwa ajili ya kuona kwamba elimu ya mwanamke hasa ya Sayansi inapatikana vizuri.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba waheshimiwa Wajumbe wafahamu kwamba tuko vizuri sana tukijilinganisha na wenzetu basi Zanzibar imepiga hatua kubwa sana na kwa hili tunaomba sana tuungane mkono jitihada hizi, ili tumuunge nguvu Mhe. Rais ambae anasimamia sekta zetu zote za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda sana kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, nashukuru Kamati, nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na kutoa ufafanuzi ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na kwanza kabisa naona nichukue nafasi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa leo tukiwa tunachangia hotuba ya kamati hii ya Ustawi wa jamii, fursa ya pili naomba nichukue kumpongeza sana Mwenyekiti, pamoja na wajumbe wote wa kamati nilibahatika kuzipitia ripoti zote na naomba nikiri kwamba wamefanya kazi nzuri sana ya kuchambua maeneo mbali mbali ya kuyatolea maelezo maeneo mbali mbali, ya kutupa maagizo ya kutupa ushauri ya kutugonga baadhi nyengine sehemu nyengine baadhi yake na kutupa rai mbali mbali. Na mimi kwa unyenyekevu kabisa kwa kuwa hilo ni jukumu lao la kikatiba tunayapokea na tutayafanyia kazi yote haya na kama ilivyokuwa utaratibu wa Baraza la Wawakilishi, mnamo mwezi wa Septemba au Oktoba na sisi tutawasilisha majibu yetu ya ripoti pamoja na maoni yetu juu ya ripoti hii kikamilifu kutoka Wizara ya Afya kwa hivyo naomba nishukuru sana.

Lakini la pili, naomba niseme katika Wizara iliyokuwa na kurasa nyingi kuliko Wizara nyengine yoyote ni Wizara ya Afya, na yote kwa sababu ya umuhimu wake kwa wananchi moja kwa moja, sisi Mhe. Mwenyekiti tuna kurasa 20 hakuna Wizara nyengine yoyote iliyofika kurasa 20 katika ripoti, lakini yote hayo naomba niseme tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo.

Nikianza kutoa moja moja kwa leo muda hautotosha wala sitomaliza lakini nitagusa machache tu kwanza kabisa naomba niseme kwamba sijapata katika historia ya Zanzibar mimi mwenyewe kushuhudia mafanikio makubwa katika sekta ya afya kama haya nitakayoyataja, jumla yake yote

haya yako 28 lakini mimi leo nitayataja manane tu 20 nitaweka *pending* na yote hayo yametokana na Dkt. Ali Mohammed Shein yeye mwenyewe, maana ndio anayesimamia sekta hii yeye ni mtaalam aliyebobea katika sekta hii na anafahamu katika sekta hii na akatumia miaka 38 ya umri wake katika sekta hii. Kwa hivyo nitaomba nitaje baadhi ya mafanikio.

Mafanikio ya kwanza kabisa kufungua Hospitali nne mie naziita hospitali nne, ya kwanza Abdalla Mzee Mkoani Pemba hospitali ya kisasa ya aina yake hapajatokea mtu aliyefikiria kwamba Pemba kutakuwa na Hospitali kubwa na yenye vifaa vya kisasa kama ile leo ya Abdalla Mzee.

Lakini hospitali ya pili ni ile tuliyoshirikiana na wenzetu wa Norway nusu tulitoa SMZ nusu Norway ni hospitali ya watoto pale Mnazi mmoja.

Hospitali ya tatu ni ile ya Wazazi ambayo tumeshirikiana na wenzetu wa Uholanzi nusu wao nusu sisi Mnazi Mmoja na sasa hivi imeshafunguliwa kwa hivyo inafanya kazi hospitali tatu hizo.

Na ya nne ni ile aliyotaja Mhe. Miraji ile ya vichwa maji lakini uti wa mgongo pamoja na vichwa maji lakini uti wa mgongo pamoja na ubongo, ambayo juzi tumefikisha uperesheni 1000 kutimia pale kufanyika, na uperesheni hizi 1000 hapo awali kila uperesheni ilikuwa inagharimu si chini ya dola elfu nne hadi elfu tano hapo zamani, leo uperesheni zile zote zimeweza kufanyika hapa Zanzibar na kuweza kuokoa fedha zaidi ya dola milioni tano za Serikali na tutaendelea hivyo hivyo chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein tutaendelea hivyo hivyo na hayo ndio maagizo yake na haya ndio yaliyoelezwa kwenye kamati tutaendelea hivyo hivyo kuleta *specialist* nyengine ili wagonjwa wetu wapungue kutoka hapa na kwenda kutibiwa India au kwengineko tunaendelea hivyo.

Lakini jengine kwa mara ya kwanza tumepata fedha kwa serikali kuu moja kwa moja kwa wingi ya kununulia madawa kote kote dawa zimefika kenye vituo vyetu vya vijijini, PSU pamoja na Hospitali zote tulipata Bilioni 1.6 moja kwa moja kutoka Serikalini, pamoja na wafadhili walichangia za kwao kwa hivyo tukawa na stock kubwa ambayo haijapata kutokezea kwa namna hiyo kwa hivyo dawa hakuna upungufu wa dawa, tunatoa sisi *hundred drugs essentialist* dawa mia, hawa wanaofanya sauti hizo sisi tunatoa dawa mia *essentialist drugs list* ile ndio ipo katika *emendate* Wizara ya Afya ndio tunayotoa bure kwa wananchi na yale ya maradhi muhimu.

Kuna baadhi ya dawa kama vile za kensa n.k ambazo zile ziko ghali sana zile hatuwezi kutoa na hazipo lakini inapotokea tatizo basi Wizara ya Afya moja kwa moja kwa kushirikiana na wenzetu Wizara ya Fedha, Wagonjwa hao wanapatiwa mtibabu, wanapatiwa dawa hizo na wengine wanasafirishwa kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kupata matibabu.

Katika mwaka huu hadi sasa tumeshasafirisha zaidi ya wagonjwa 200 kwa hivyo hajarudishwa mwananchi haangaliwi uwezo wake haangaliwi chochote kile chengine, hajarudishwa mwananchi kwa ubagui wa aina yoyote ila anapatiwa matibabu na tunashukuru kwa Serikali yetu inaendelea kutoa huduma hizo kwa wananchi. Lakini mbali hayo uperesheni mbali mbali za kisasa zimekuwa zikifanyika katika kitengo chetu cha utiwa mgongo na ubongo kuna uperesheni moja imefanyika na ilitolewa kwenye TV bahati nzuri taarifa zake, haijapata kufanyika hata huko ulaya pamoja na wataalam wetu wanasema hata huko ulaya haikupata kufanyika

uperesheni kama hiyo. Kwa hivyo hiyo ilifanyika Zanzibar na kuweza kuokoa maisha ya yule mwanakijiji wa kijiji cha Chwaka anatokea Chwaka bahati nzuri.

Jengine tunaendelea kusomesha vijana wetu haijapata kutokezea katika historia ya Wizara ya Afya vijana zaidi ya 130 kuweko nje kwa wakati mmoja mwaka huu katika masomo mbali mbali ya *Specialist* mbali kwa hivyo hayo yanaendelea ili kuongeza ufanisi na taaluma pana zaidi katika Wizara ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni miongoni mwa mambo machache lakini hivi karibuni na tutawaalika Waheshimiwa Wawakilishi wote hivi karibuni tunategemea kuzindua MRI mashine ya kisasa inaitwa *Magnetic Resonance Imaging*, yenye uwezo wa kumuangalia binaadam mpaka mishipa yake midogo inayokwenda kwenye ubongo, kama kuna mkwamo wowote wa damu ambayo haifiki eneo linalotakiwa na linalohusika basi mashine hiyo ina uwezo wa kuona, sasa hivi ile mashine inafungwa, vijana wetu wanapatiwa mafunzo na Mungu akitujaalia inshaallah Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein mwenyewe atakuja kufungua na Wawakilishi wote wataalikwa ili waweze kushiriki ufunguzi huo. Yote hayo yanatokana na jitihada zake Dkt. Ali Mohammed Shein moja kwa moja.

Lakini mbali ya hilo tumefunga mitambo ya kisasa pale Mnazi Mmoja ambayo itakuwa inafanyakazi ya kuweka rekodi za wagonjwa wote wanaoingia wenye maradhi mbali mbali, wanakotokea n.k. Mitambo hiyo nayo itazinduliwa hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninachoomba wajumbe wengi wamechangia na nashukuru michango yao yote Wajumbe tumeipokea na yote tutaifanyia kazi, michango muhimu sana, wale waliotoa rai, waliotoa ushauri, waliokosoa ni haki yao, wale waliotugonga maeneo mengine ni haki yao na yote hayo tutayachukue na kuyafanyia kazi. Pia yale waliyotwambia ya kutuchonga ukali kidogo, kwa hiyo wasije wakalalamika tutakuwa wakali zaidi kwa watendaji, kwa sababu yale yaliyoelezwa mengine yanawahusu watendaji moja kwa moja, hatutosita kuwa wakali kwa watendaji.

Naomba bila ya kumtaja mjumbe mmoja moja niseme kwamba michango yao yote tumeipoke na tutaifanyia kazi ipasavyo. Niende katika yale mambo muhimu sana ambayo yametajwa, moja ni Mnazi Mmoja. Mnazi Mmoja imeguswa sana, ninachokuomba Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu nawaomba kuwaeleza kwamba pale tumepitisha sheria sio zaman sana ya Mnazi Mmoja na bodi mpya imeundwa, Mhe. Rais amemteuwa Mwenyekiti na amemteuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mnazimmoja, tuwapeni muda hawa wafanya kazi yao. Hivi sasa wanafanya kazi nzuri sana, wanafanya *transformation* wale wanaokwenda sana Mnazi Mmoja kama Mhe. Jaku Hashim watakuwa tayari wameshaona matron amebadilishwa kuna nafasi muhimu, yameshatokezea mabadiliko makubwa sana. Wamepanga mipango mizuri Wizarani wametushirikisha, wameshatuletea mipango yao tuwapeni kama miezi sita hivi waweze hizi nafasi mpya nyengine wanazitangatia, nyengine wanazoziwekea watendaji mbali mbali. Baada ya miezi sita tutaona mabadiliko makubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo kubwa limegusiwa ni kuhusiana na watendaji wetu, wafanyakazi wetu naomba niseme Wajumbe wote waliochangia mojwa kwa moja niliowapata miye idadi yao ni 15 na 5 wamenileta kwa maandishi. Naomba kuwashukuru sana Wajumbe walionileta kwa maandishi, wamenileta mambo mazito kweli kweli nafikiri mengine

hawakutaka kuyatamka kwa sababu ni mazito. Naomba niwaahidi na wao walioniletea kwa maandishi tutayafanyia kazi ipasavyo kwa sababu mengine yanawahusu watendaji moja kwa moja.

Afisa Mdhamini wa Pemba yupo hapa bahati nzuri ananisikia tutamchonga ukali zaidi. Kuna baadhi ya vituo kweli Waheshimiwa Wawakilishi wamewasilisha na ushahidi, vinachelewa kufunguliwa Pemba kweli. Natamka mbele yako Mhe. Mwenyekiti, kwenye Baraza hili tukufu, hilo tutalichukulia hatua kisheria bila ya kuwa na uvumilivu wowote. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi msije kuwaombea tena tutakaowachukulia hatua, Afisa mdhamini ananisikia watendaji wote wanasikia tutayachukulia hatua za kisheria ipasavyo na kutokana na sheria ya utumishi, hatutokubali.

Jengine ambalo limeguswa sana naomba niseme suala la *ambulance* katika baadhi ya hospitali Makunduchi, Kivunge, tumeshapata tayari *ambulance* sasa hivi na tayari zimeshafikishwa, tunachohangaika kutafuta ni bajeti ya kutosha ya kuweza kukidhi haja kwa ajili ya mafuta zile ambulance zetu kufanyia kazi. Lakini wakati huo huo Mhe. Mwenyekiti, kesho tukijaaliwa na Mwenyezi Mungu tuna ghafla rasmi ambayo wenzetu ambao tunashirikiana nao wanaitwa helth *improvement program* ya Zanzibar hawa ni taasisi kutoka Uingereza ambao wanashirikiana na sisi Wizara ya Afya moja kwa moja. Kesho tutakuwa na chakula cha hisani pamoja na kuchangishana kwa ajili ya hospitali ya Kivunge na ya Makunduchi. Tumetoa mialiko kwa Wawakilishi wote na kuna mchango ambao unatakiwa kuwasilishwa. Tunashangaa sana kesho nikiwa sijawaona Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaohudumiwa na hospitali hizi mbili moja wamesema ni ya Mkoa kabisa ni kweli inahudumia kama ya Mkoa ya Kivunge. Mgeni Rasmi ni Mhe. Rais Dkt. Ali Muhammed Shein ndiye mwenyewe. Itafanyika mnamo saa 2:00 katika hoteli ya kitalii ya kifahari Hayat pale Shangani katika ukumbi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na michango mbali mbali naomba niseme kwamba mengi kama nilivyoeleza hapo awali tumeipokea ya vituo hivi vyetu vya Afya kufanya marekebisho, matengenezo kuhusiana na wodi za watoto, upande wa paa, hospitali ya Chake Chake, Wete, hospitali zetu Kivunge, Makunduchi, ombi la Mhe. Zulfa naomba niseme nimelikubali maana amenileta ombi moja kwa moja amesema tutembelee pamoja namuahidi tutakwenda pamoja mote humo namuahidi tutakwenda kutembea pamoja kwenye wodi pamoja na hospitali.

Naomba niseme kwamba Pemba Hospitali ya Chake Chake kuna madaktari wawili pale wa macho yupo Dokta Siti na yupo nadhani Dokta Ali Rashid wapo pale, kwa hiyo naomba tuendelee kuwatumia na sisi tutawawezesha zaidi na tutaweka kambi pale itakapokuwa muda umekaribia wa ila kwambi yetu ya macho tutaweka pale kambi ya macho ili tuweze kutoa matibabu mbali mbali ya macho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo yote pamoja na yale yaliyowasilishwa kwa maandishi naomba niseme tumeyapokea tutaendelea kuyafanyia kazi na hili la hospitali ya Ubongo limeulizwa hili. Kwamba je, sisi tumejitayarisha vipi au tunawategemea wale wenzetu Wazungu tu. Naomba niseme vijana wetu wanane tayari wameshakwenda Spain Mji wa Valencia kwenda kupata mafunzo mbali mbali.

Mimi namshukuru Dkt. Ali Muhammed Shein nimebahatika kupata *trip* ya kwenda huko Spain mji unaoitwa Valencia na pale nimetembelea hospitali ile ambayo tunashirikiana nao, bahati nzuri vijana wetu wawili nimewakuta wamo ndani ya *operation theater*. Nimekwenda mimi mwenyewe kuwaangalia walikuwa ndani ya *operation* ya ubongo kichwa kimepasuliwa kizima kinatolewa kama bakuli linawekwa pembeni hili fuvu, wanafanya watu kazi yao halafu wanarudisha lile bakuli wanashona, huu mfupa baada ya muda fulani unaganda unakuwa na kovu kubwa. Mimi nilibahatika kuiona *operation* hiyo na nikakuta vijana wetu wawili mimi sikuweza kukaa mpaka mwisho kwa sababu mbali mbali. Lakini vijana wetu niliwakuta pale na bahati nzuri wamepongezwa na kusifiwa sana kazi wanayoifanya. Kwa hiyo kila baada ya muda wanakwenda wakirudi. Hivi sasa pale tuna wataalamu wanne ambao kile kitengo hata wao wanapokuwa hawa ndugu zetu wa Spain ambao wanashirikiana nao basi kina Dkt, Ustadhi Muhammed tunaendelea kushikiana nao.

Naomba nishukuru sana vikosi vya SMZ sana wengi hawajui lakini pale tunawafanyakazi hatutaki kuwataja maana wengine hawatajwi, tunaendelea kushirikiana nao wapo pale Mnazimmoja na Hospitali zao wa KMKM pamoja na jeshi la Bububu tunaendelea kushirikiana nao kwa karibu sana. Naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwao wao.

Kwa kumalizia kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Dkt. Sira kwa mchango wake ambao kachangia kuongezea baadhi ya maeneo ya sekta ya afya kwani yeye ni mtaalamu aliyebobea kama hamjui taaluma yake, taaluma yake ni *X-ray* yaani *Radiology* ndiyo taaluma yake. Katika hii ya mara hii inayofungwa pale anaendelea kutusaidia sana, tunamshukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba nishukuru tena Kamati nzima, Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wake wote kwa miongozo yao, changamoto, maoni tumeyapokea na tutayafanyia kazi na Ishaallah Mwenyezi Mungu akitujaalia mwezi wa Septemba tutawasilisha ripoti hapa Barazani. Naomba michango ya wale wote waliochangia 15 kwa kuchangia moja kwa moja na wale 5 waliochangia kwa maandishi jumla yao 20 yote nayo tutayajumuisha katika hiyo michango itakayowasilisha wakati huo Barazani Septemba na Ishallah wataridhika. Lakini tunaomba sana mashirikiano ya Waheshimiwa Wawakilishi mashikiano yao yanatuwezesha sisi kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, ni muhimu sana. Mashirikiano kati yetu ni muhimu sana, mimi nawashukuru wote hawa wanaotugonga gonga Mhe. Jaku Hashim, Mhe. Nadir Abdul-latif, kwa kweli mimi nawashukuru na nimeshafanya nao ziara na nawashukuru kwamba tunaendelea kushirikiana.

Muhimu sana unapoliona jambo kwa mfano juzi nilikuwa na Mwakilishi mmoja tumekwenda Msikitini kusali tumemkuta jamaa anauza madawa yale ya tiba asilia tunaziita dawa za sunna. Yule Mwakilishi akamuuliza mimi nilikuwa nipo ndani akamuulia je, wewe unakibali cha Bodi ya Tiba Asilia, kwa bahati yule bwana hakuwanacho kile kibali. Sasa ninachotaka kusema tunapiga marufuku kuuza dawa zote hizi za sunna Misikitini kama huna kibali cha Bodi Tiba Asilia marufuku kuanzia leo. Lakini tuendelee kushirikiana, juzi Mwakilishi aliwauliza wale kwa bahati yule bwana akawa hana kibali akaomba muongozo afanyeji mpaka apate kibali na mimi nikawa nipo pale nikamueleza haraka sana funga duka lako nenda kwa ndugu Haji Kundi ndio mrajisi wa Bodi hii ya Tiba Asilia kachukue kibali na bahati nzur zile Kanuni mimi nimeshatia saini kuna bei zake na kuna mrorongo wake.

Leo mkitumia dawa au wananchi wakitumia dawa zile ambazo hazina vibali tutakaoathirika ni sisi tena kwa sababu yule akiumwa kule nje anarudi hospitali, makosa yakitokezea kule yote yanarudishwa hospitali. Ninachotaka kusema lile ni jambo letu sote jamii namshukuru sana Mhe. Mwakilishi simtaji leo hapa kwa sababu alikuwa ameelewa ile sheria ya Bodi ya Tiba Asilia na ameweza kuchukua hatua hapo hapo. Kila Mwakilishi aliyekuwemo humu ndani anajukumu katika jamii hii ya Zanzibar.

Unapoliona jambo usisubiri wewe mpaka ripoti ya Dkt. Mwinyihaji ama kwenye Bajeti ya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo usisubiri, unapoliona jambo kama unatekeleza kweli wajibu wako kwa wananchi lichukulie hatua pale pale ukishakuchukulia hatua pale pale umekwama Mhe. Haji Omar Kheir yumo, vikosi vipo, sheria za ulinzi na usalama zipo, sisi Wizara ya Afya tupo, unalileta moja kwa moja tunalifanyia kazi pale pale. Tukisubiri hatujui athari gani itakayoweza kutokea kwenye jamii, tukisubiri hatujui athari gani itawatokezea vijana wetu au watoto wetu, hatujui kama mwisho wa siku kama yale maradhi yanaambukiza hataweza kutufika na sisi wenyewe. Hili ni jambo letu sote naomba sana mashirikiano ya Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda huu ulionipa nakushukuru sana na nakuahidi ripoti yetu Ishallah itakuwa nayo inakaribia ukurasa 20 mwezi wa Septemba. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa mara nyengine tena kunipa fursa hii yakufanya majumuisho juu ya ripoti ya Kamti yetu ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kuendesha kikao chetu kutwa nzima ya leo mpaka sasa hivi kwa utulivu. Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu waliouonesha pamoja na michango mizito waliyotupa katika hoja yetu hii. Lakini hasa niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wetu wawili kwanza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Mwenyekiti, hizi hoja Kamati imezipata kwenye ziara, yaani imezipata *field* kwa kuona na wafanyakazi kuona hali ya mambo ilivyo. Kamati haikuzipata kwengine popote kwa hivyo haya tuliyoyasema niseme ndiyo za *really picture* tuliyoipata kule *field*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawashukuru sana Mawaziri, tulipomaliza ziara tulifanya majumuisho na Wizara hizi mbili Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya na haya yote tuliyoyaeleza walitupa ufafanuzi mzuri kama Kamati na tuliridhika kabisa. Lakini kwa kufanikisha majukumu ya kazi za Kamati tuliwambia wazi wazi sisi lazima tutie kwenye ripoti,haya tuyaseme na halafu tupate hisia za Wajumbe.

Sasa hapa tunashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kweli wamepata zile hisia wameona kwamba kweli haya mambo yako kweli kwenye majimbo. Lakini tunashukuru zaidi mafanikio yaliyosemwa hasa alivyo *summaries'* Mhe. Waziri wa Elimu na Mhe. Waziri wa Afya na sisi kama Kamati tuna *acknowledge* kwa asilimia 100 serikali yetu imepita hatua kubwa katika sekta hizi mbili na ndio unapata changamoto, hupati changamoto kama hufanyi kazi, hupati changamoto kama hutendi, ukikaa tu changamoto husioni. Ndio maana changamoto zimetokea za hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nitoe utangulizi mdogo, lakini kama nilivyosema niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia, tumepata Waheshimiwa Wajumbe 41, Waheshimiwa 15 wamechangia ukumbini, na Waheshimiwa 26 wamechangia kimaandishi. Mhe. Waziri wa Afya kupitisha kwake walikuwa wengi wananiletea moja kwa moja. Lakini tutakaa pamoja Mhe. Mwenyekiti, na Wizara zote mbili tutasheha michango hii tuone *tha way forward* pia naamini yatawasaidia katika utendaji wao wa kazi hasa utayarishaji wa bajeti unaofuata mbali ya kuja kujizibu hoja.

Sasa kwa heshima kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue Waheshimiwa waliochangia hapa ukumbini.

1) Mhe. Suleiman Sarahan Said
2) Mhe. Mwantatu Mbarak Said
3) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4) Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf
5) Mhe. Dhulfa Mmanga Omar
6) Mhe. Ali Suleiman Ali
7) Mhe. Ame Haji Ali
8) Mhe. Panya Ali Abdalla
9) Mhe. Said Omar Said
10) Mhe. Miraji Khamis Mussa
11) Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
12) Mhe. Bihindi Hamad Khamis
13) Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
14) Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
15) Mhe. Waziri wa Afya.

Waliochangia kwa maandishi ni kama hawa wafuatao:

16) Mhe. Naibu Waziri, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
17) Mhe. Ali Khati (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
18) Mhe. Bahati Khamis Kombo
19) Mhe. Salha Moh'd Mwinjuma
20) Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
21) Mhe. Asha Mussa Abdalla Mussa
22) Mhe. Ali Khamis Bakari
23) Mhe. Abdalla Maulid Diwani
24) Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
25) Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
26) Mhe. Mussa Ali Mussa
27) Mhe. Hidaya Ali Makame
28) Mhe. Waziri wa Habari Utalii na Michezo
29) Mhe. Sada Ramadhani Mwendwa
30) Mhe. Ussi Yahya Haji
31) Mhe. Naibu Waziri Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais
32) Mhe. Tatu Muhammed Ussi,

33) Mhe. Zainab Abdalla Salum
34) Mhe. Abdalla Ali Kombo
35) Mhe. Hamida Abdalla Issa
36) Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
37) Mhe. Suleiman Makame Ali
38) Mhe. Khamis Juma Maalim
39) Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba,Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora,
40) Mhe. Mussa Foum Mussa
41) Mhe. Mohamed Said Mohamed
42) Mhe. Shehe Hamad Mattar (Mwenyekiti wa Baraza)

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema jumla walikuwa 26 na waliopata fursa kuchangia ukumbini ni 15 jumla ni wachangiaji 41. Kwa kweli kama tulivyosema tunathamini sana michango yao ambayo waliitoa kwa hamasa suala la elimu halina mjadala kila mmoja wetu ameona umuhimu wa elimu katika nchi yetu. Kama nilivyosema wataalamu wote chimbuko lake ni elimu bora. Na sisi kama Zanzibar tulifanikiwa kuvuka lile lengo la *millennium* yaani *Universal Primary Education* kabla ya wakati uliowekwa wa 2015, sasa awamu inayofuata ya hiyo ya *startenable development* na upande wetu sasa tuboreshe elimu ndio saula la msingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, bado changamoto ya vijana wengi umetoka mfano hapa darasa lina vijana 200 ni hatari! Lakini sasa tuwafanye nini, lazima waende shule tusiwaache nyumbani. Changamoto za kiutendaji ndizo zilizotokea. Lakini tunashukuru sana Mipango mizuri ambayo Wizara inayo kulikabili tatizo hili na Ishaallah Mwenyezi Mungu atatusaidia kama ulivyosema *resources* zikija tutafanikiwa vizuri .

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wamechangia wametoa maoni, wameuliza maswali kama awalivyosema Mawaziri wetu na mwisho wametoa maoni kwamba nini tufanye. Mimi sina haja ya kuyarejea tena, tumesikia wote na kama tulivyosema kwamba hansard zipo na sisi tumeshukua *notes*, tutakaa pamoja na Wizara na wao wenyewe watakaa na sisi pia tutawakumbusha tuone tunatengeneza *matrix* maalum, mchango wa Mheshimiwa fulani ulikuwa huu je, utekelezaji wake ukoje. Ili mwakani tukija tuone angalau tunatia tiki tunaona hili limekwendaje utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina zaidi ninachosema kwamba tunawashukuru sana Waheshimiwa wote na hasa wewe Mwenyekiti, Mawaziri wetu, Watendaji wote kwa ujumla, Makatibu wakuu, Wakurugenzi Wakuu, kazi tuliifanya ni kubwa sana. Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu, haya ni ma - *giant* na kwa kweli ma- *giant* yenyewe ni muhimu, hakuna anayetaka kuumbwa na hakuna anayetaka kukosa elimu. Dokta Sira kaeleza vizuri sana tunamshukuru sana. Mimi nimalizie kwa kuwashukuru sana na niseme asante sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Asante sana Mhe. Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwenyekiti, wanyooshe Mkono, wanaokataa waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa na kuamuliwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha kikao na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri pamoja na watendaji wao na imani yangu kwamba michango mliyoitoa Waheshimiwa Wajumbe wameipokea na wataifanyia kazi kwa vile sisi sote tunajenga nyumba moja na nina imani mwezi wa 9 basi tutaona mafanikio ya ripoti hiyo pamoja na ile michango yote ya Wajumbe iliyotolewa.

Waheshimiwa Wajumbe pia niwashukuru nyote kwa utulivu wenu na usikivu wenu, kwa kuniruhusu mimi kuendesha kikao hichi kwa umakini na bila ya nyinyi nina imani nisingefanikiwa. (*Makofi*)

Jengine kuna tangazo Waheshimiwa Wajumbe niwambie kuwa kamati ya ushindi ya Klabu ya Simba inataka Waheshimiwa wafuatao wakutane katika hoteli ya *C-Cafe* mara baada ya kikao hichi wajumbe wenyewe ni Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Ali Salum, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Salha Mwinjuma, Mhe. Mwantatu Mbarak, Mhe. Rashid Makame na Mhe. Shaib Said Ali, waonane na mratib Abdalla Maulid Diwani, kwa ajili ya mikakati ya ushindi. (*Makofi*)

Waheshimiwa nawashukuru sana nakhairisha kikao mpaka Jumatatu Ishallah saa 3:00 asubuhi.

(Saa 2:22 usiku Baraza liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu tarehe 27/2/2017 saa 3:00 asubuhi)